Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi - Tarehe 22 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 89

### Ukataji Miti Kwenye Maeneo ya Miji

**MHE. EDSON M. HALINGA (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi yetu ni jambo la nadra sana kwenye Miji kuwa na miti/bustani za miti kwa vile hata Miji ambayo ilikuwa na misitu watalaam wanapokuwa wakipima viwanja huagiza miti yote ikatwe:-

(a) Je, kwa nini Miji yetu ya Makao Makuu ya Wilaya/Mikoa katika mipango yake ya ujenzi huagiza miti ikatwe katika maeneo ya ujenzi wa makazi na upimaji wa viwanja kutozingatia upandaji wa miti mingine?

(b) Je, kwa nini Miji ambayo siyo ya viwanda bali ya kilimo hakuna upimaji wa maeneo ya *Green Belt* kama ilivyoandaliwa *Master Plan* ya Mji wa Dodoma wakati huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji suala la kupanda miti katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hizo linapewa kipaumbele na hairuhusiwi kabisa kukata miti hiyo iliyopandwa. Aidha, Sheria za Miji zinasisitiza suala la upandaji wa miti katika ngazi ya kaya ambapo kila kaya inatakiwa kuwa na angalau miti mitano. Kama nilivyoeleza hapo juu, Miji yetu ya Makao Makuu ya Wilaya/Mikoa haitoi agizo la kukata miti ili upimaji wa viwanja ufanyike.

Kinachoweza kutokea ni kwamba, kutokana na kupanuka kwa miji na mahitaji ya viwanja kwa shughuli mbalimbali, miti ya asili au miti iliyopandwa ambayo imeingia eneo hili hulazimika kukatwa. Wakati wa kampeni za kupanda miti kinachozingatiwa zaidi ni upandaji miti katika maeneo matupu. Hata hivyo, maeneo hayo hayahusiki na uendelezaji wa kiujenzi, maeneo yasiyohusika na uendelezaji kiujenzi huelekezwa kuhifadhiwa na miti yake.

(a) Mheshimiwa Spika, upimaji wa maeneo ya *Green Belts* katika miji ambayo siyo ya viwanda bali ya kilimo haufanyiki kwa sababu kila mji unao mahitaji mahsusi kwa ajili ya jamii inayoishi kwenye Mji huo. Katika maeneo ambayo ardhi ni haba, miji hiyo inalenga zaidi kuwapatia wananchi wake viwanja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi na mahitaji mengine.

Hata hivyo, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, miji inapaswa iangalie suala la upimaji wa maeneo ya *Green Belts* ambayo yanalenga zaidi katika kilimo, ufugaji na kuhifadhi mazingira kwenye hali yake ya asili.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba ukataji miti ni jambo baya hasa katika maeneo yanayotakiwa kuwepo miti. Je, anaweza kukubaliana na mimi kwamba watunge sheria kila anayepewa kiwanja mjini au sehemu yoyote iliyopimwa awekewe na idadi ya miti ya kupanda ili mazingira yasiharibike? *(Makofi)*

(b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kutoa tamko kwamba Mikoa na Wilaya mbalimbali kama Mbeya ilivyokuwa na miti mingi, sasa wanakata miti wanajenga nyumba, tabia hii isiendelee maana inaharibu mazingira? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika maelezo ya awali, Sheria za Mipango Miji zinasisitiza jambo hili la upandaji miti katika maeneo yote ya miji na inataka kwa kweli kila mkazi kwenye eneo lake angalau awe na miti mitano. Tatizo hapa ni utamaduni, wengi hatuna utamaduni wa upandaji miti na mimi napenda niseme hili hata kwa baadhi ya maeneo yetu tunayoishi mengine hayana miti mpaka leo. *(Makofi)*

Pili, kuhusu Mkoa kama wa Mbeya ambako miti inakatwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, kama nilivyosema katika maelezo sehemu kubwa ya tatizo hili inategemea mazingira ya kila eneo, upande mmoja ni dhahiri kabisa kwamba wananchi wanahitaji

kujenga nyumba na kama *level* yao bado ni ujenzi wa nyumba za miti ndiyo maana tunasisitiza sana ujenzi wa nyumba za matofali ya kuchoma. Kwa hiyo, mimi nafikiri tungesaidiana katika hili ili tuweze kuimarisha mazingira yetu.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa katika mipango miji yametengwa maeneo ambayo yanajulikana kama *open spaces,* lakini utakuta maeneo haya yote yamevamiwa na kujengwa majumba. Je Serikali, inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba hizi *open spaces* zinarudi kama zilivyokuwa mwanzo, ili kupatikane na hali ya kuhifadhi mazingira pamoja na viwanja vya michezo kwa watoto? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa ni kweli yapo maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya madhumuni fulani fulani katika maeneo yetu ya miji na baadhi ya maeneo hayo katika baadhi ya maeneo yamevamiwa kwa sababu mbalimbali. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, yeye mwenyewe anafahamu jinsi ambavyo Serikali imekuwa ikikemea tabia hiyo, kuhakikisha kwamba maeneo haya yanatunzwa kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. Lakini pili, naomba niombe Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane katika suala hili kwa sababu makosa hayo yanafanywa na Halmashauri zetu, kwa hiyo, mimi nadhani kalipio la kwanza lingeanza katika kila Halmashauri ili kuhakikisha kwamba tabia hiyo inakomeshwa. *(Makofi)*

Na. 90

**Uteuzi wa Madiwani**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa katika utaratibu wa zamani, Waziri aliyekuwa na dhamana ya Serikali za Mitaa alipewa uwezo wa kisheria wa kuteua Madiwani watano katika Halmashauri baada ya Uchaguzi wa Madiwani na kwa kuwa kwa utaratibu wa sasa Mheshimiwa Rais amepewa uwezo wa kisheria kuteua Wabunge kuingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizofanya utaratibu wa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa wa kuteua Madiwani watano kufutwa?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Rais, amepewa uwezo Kikatiba wa kuteua Wabunge kumi kwenye Bunge pia Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naye apewe uwezo kisheria wa kuteua Madiwani watano katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba awali Sheria Na. 7(35) na 8(26) za Serikali za Mitaa za mwaka 1982 zilimpa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, uwezo wa kuteua Madiwani wasiozidi watano. Kufuatia marekebisho ya sheria hizo hapo Machi, 1994 utaratibu huu uliondolewa kupitia Bunge lako Tukufu. Vile vile kwa mujibu wa vifungu 145 na 146 vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Serikali za Mitaa ni Serikali kamili zenye majukumu ya kisheria ya kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi na kuimarisha demokrasia na kuitumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ya kufutwa kwa uwezo wa kisheria wa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kufanya uteuzi wa Madiwani ulitokana na mahitaji ya Kikatiba ya kupeleka madaraka zaidi kwa wananchi ili kuwawezesha wananchi wenyewe kuchagua viongozi wao wanaowapenda ikiwa ni pamoja na Madiwani. Marekebisho haya yalifanyika ili kuimarisha ushirikishaji wa wananchi na viongozi wao katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli zao za maendeleo katika maeneo yao pasipo kuonekana kuingiliwa na Serikali Kuu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, ninaelewa nia ya Mheshimiwa Mbunge ya kutaka Halmashauri ziimarishwe kwa njia hii ya kumrejeshea uwezo wa kisheria Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ateue Madiwani watano kwa kila Halmashauri, lakini tukifanya hivyo itakuwa ni kufanya kinyume na matakwa ya Kikatiba yaliyomo katika ibara ya 145 na 146 na vilevile Sheria Na. 7 na Na. 8 za Serikali za Mitaa na hivyo kuua demokrasia chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa ambayo kwa kweli kwa sasa ni dhahiri kabisa kwamba ina umuhimu wake. *(Makofi)*

Madiwani hawa wa kuteuliwa ni dhahiri hawatakuwa wamechaguliwa kwa ridhaa ya wananchi na kwamba hali hii itakuwa mojawapo ya sababu za kuwepo kwa migongano ya kutoelewana kati yao na Madiwani wa kuchaguliwa. Kwa sasa tuliomba Bunge Tukufu liendelee kuiunga mkono Serikali katika dhamira yake ya kuendelea kudumisha demokrasia katika ngazi za chini kwa utaratibu uliopo. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuteua hao Madiwani, demokrasia itakuwa kwamba wananchi hawatakuwa wamewachagua wale Madiwani. Sasa je, Wabunge wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais, hiyo demokrasia inawaruhusu wao tu Madiwani haiwaruhusu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imepitishwa na Bunge lako Tukufu hili hili. Marekebisho ya Sheria ya Mwaka 1994 yamefanywa na Bunge lako Tukufu hili hili. Mimi ninachosema tu ni kwamba, kwa

mazingira kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa iko tofauti ambayo imewekwa pale kwa makusudi. Serikali Kuu inalo Baraza la Mawaziri, ina Mawaziri ambao wanatunga sera na kuhakikisha zinasimamiwa. Katika ngazi ya utekelezaji tunachofanya ni kutekeleza sheria na sera na ndiyo mfumo wa kumweka Waziri kuteua Madiwani, hauwezi ukalingana na uwezo wa Rais wa kuteua Wabunge katika ngazi ya Taifa ambapo anapenda kuhakikisha kwamba wanaisaidia Serikali, kuweza kushughulikia shughuli zake vizuri. *(Makofi)*

Na. 91

**Matatizo ya Watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Kifua Kikuu Kibong'oto**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alipoitembelea Hospitali ya Rufaa ya Kifua Kikuu iliyopo Kibong'oto alipata fursa ya kuongea na wafanyakazi wa hospitali hiyo na miongoni mwa mambo waliyoyazungumzia ni pamoja na *promotions* zao na marupurupu ya aina mbalimbali zikiwemo *risk allowances,* naye aliahidi kuyafuatilia matatizo hayo kwa karibu:-

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi ambao wamekwishapatiwa *promotions* zao na wangapi bado hawajapatiwa?

(b) Je, ni *allowances* zipi zimelipwa na ziligharimu kiasi gani cha fedha na ni wafanyakazi wangapi wamelipwa na wangapi hawajalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, jumla ya watumishi 22 wa Hospitali ya Kibong'oto walipandishwa vyeo kama ifuatavyo: Maafisa Wauguzi 2, Wauguzi/Wauguzi Wakunga 3, Wahudumu wa afya 11, Tabibu 1, Dobi 3, *Medical Technician* 1 na mtunza kumbukumbu za afya 1.

Mheshimiwa Spika, posho zilizokuwa zikilipwa kwa watumishi wa afya hapo awali ni kama zifuatazo: Posho ya taaluma, posho ya kufundishia, posho ya kufanya kazi katika mazingira magumu, posho ya afya na posho ya kuitwa kazini *(On Call Allowance).* Hata hivyo, posho hizi zilijumuishwa katika mishahara wanayolipwa watumishi wa afya kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 1995 isipokuwa posho za matukio ya kuitwa kazini *(On Call Allowance)* na upasuaji maiti kwa uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, posho pekee zinazolipwa kwa sasa ni posho za kuitwa kazini *(On Call Allowance)* na upasuaji maiti *(Post Mortem Allowance).* Katika mwaka wa

fedha wa 2002/2003 kiasi cha shilingi 36,371,000/= kililipwa kama *on call allowance* Sasa hivi Hospitali ya Kibong'oto haidaiwi posho yoyote na wafanyakazi wa hospitali hiyo. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Afya, Mheshimiwa Anna Abdallah, kwa kunipokea katika ofisi yake na kuwa tayari kufika katika hospitali hii ambayo ninaizungumzia.

Ningependa kujua kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu suala la *risk allowance* kwa sababu wale walioko pale wanawahudumia wagonjwa wa *TB* na *TB* ni ugonjwa unaoambukiza sana. Je, ni kwa nini mpaka sasa hivi hawa wahudumu wa Hospitali ya Kibong'oto hawajapata *risk allowance* kama alivyosema kule nyuma kuwa itashughulikiwa na Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ya kwamba *risk allowance* si kwamba imefutwa bali imejumuishwa katika mishahara ili hatimaye wafanyakazi wanapostaafu waweze kupata kiinua mgongo ambacho ni kikubwa zaidi. Lakini hata hivyo, Serikali inatambua ya kwamba, mazingira wanayofanyia kazi sasa hivi ni magumu na si upande wa risk tu bali hata ile posho ya mazingira magumu vyote kwa kweli vinahitajika. Kwa hiyo, tulichosema ni kwamba, Wizara yangu imeunda Kamati ya kuchunguza namna gani ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa afya ili hatimaye tuifikishe Serikalini na endapo itapita basi wafanyakazi wa afya wataweza kupata posho zilizo nzuri zaidi.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa kuna maeneo ambayo miundombinu bado si mizuri, barabara hakuna, simu hakuna, maji hakuna na wauguzi wengi wanatakiwa waende huko, sasa kwa jinsi hali ilivyokuwa ngumu hawapendi kwenda. Je, wafanyakazi wa wa afya walioko kwenye maeneo kama hayo hawawezi kufikiriwa wakapata walau hiyo posho ambayo inaweza kusaidia katika hali hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, posho hii ndiyo ile ambayo nimeitaja ambayo tunaiita posho ya mazingira magumu. Ni kweli kwamba, kuna baadhi ya maeneo ya nchi yetu si wafanyakazi wengi wa afya ambao wanapenda kwenda katika maeneo hayo. Sasa lengo ni kuweka posho kwa ajili ya kuvutia watu katika maeneo kama hayo. Lakini kama nilivyosema, hili ni suala ambalo sasa hivi linafanyiwa kazi na Kamati tuliyoiteua ili kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kuboresha posho hizi ikiwemo hii ya mazingira magumu na ile ya *risk allowance* ili tuweze kuzirudisha tena.

Mheshimiwa Spika, lazima nisisitize kwamba, huo bado haujakuwa ni uamuzi, ni Kamati tu imeteuliwa ili itafute njia bora kabisa ya kuboresha maslahi na endapo itapitishwa posho hizi ndipo zitakapoweza kurudi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu mazuri ambayo amekwishayatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya ni moja ya sekta muhimu sana katika kuondoa umaskini kwa Watanzania. Vile vile ni kweli kwamba, kuna maeneo ambayo ni pembezoni na kwa hiyo, mazingira ya kufanyia kazi hasa watumishi wa sekta ya afya ni magumu na kwa hiyo, suala la Waheshimiwa Wabunge kuona kwamba ni muhimu kutoa posho ya mazingira magumu ni muhimu sana. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ni suala ambalo linafanyiwa kazi.

Lakini hata hivi sasa kuna hatua ambazo zimechukuliwa za kuhakikisha kwamba, madaktari na watumishi wengine wa sekta ya afya wanapohitimu wanapelekwa moja kwa moja kwenye maeneo mbalimbali na kila tunapopata jambo zuri kama mafunzo, tunatoa kipaumbele kwa wale ambao wako pembezoni. *(Makofi)*

Na. 92

**Magari ya Zimamoto**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa Miji mingi hapa nchini haina magari ya zimamoto ikiwemo Manispaa ya Mbeya na kwa kuwa hali hiyo inahatarisha maisha na mali za wakazi wa Mijini hasa unapozuka moto mkubwa kwa sababu zozote zile:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kulitatua tatizo hilo ambalo ni la muda mrefu?

(b) Kwa kuwa vikosi vya zimamoto havina nyenzo thabiti za kutendea kazi, je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inavunja ari ya watumishi wa vikosi vya zimamoto katika kutekeleza majukumu yao?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba miji yetu mingi hapa nchini haina magari ya zimamoto na hata miji yenye magari hayo, idadi ya magari ni ndogo na mengi kati ya hayo ni machakavu. Kutokana na umuhimu wa magari ya zimamoto, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la upungufu wa magari ya zimamoto ikiwa ni pamoja na hatua zifuatazo:-

(i) Serikali imeendelea kununua magari ya zimamoto kwa awamu hadi yatakapopatikana ya kutosha kwa mfano katika mwaka wa fedha wa 2002/2003, Serikali

ilitenga Sh. 1.5 bilioni kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto kwa ajili ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali imetenga Sh. 1.5 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa magari ya zimamoto kwa Manispaa yaTemeke, Ilala, Kindononi, pia Manispaa ya Ilemela na Nyamagana kwa Jiji la Mwanza. Taratibu za ununuzi wa magari haya zimekamilika. Mwaka ujao wa fedha pia Serikali imetenga Sh. 2,450,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa magari haya kwa Miji ya Tanga, Mtwara, Songea, Iringa, Mbeya, Tabora na Kigoma; *(Makofi)*

(ii) Tunaendelea kuzihamasisha Halmashauri za Manispaa na Miji kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kununua magari ya zimamoto na pia kutafuta wahisani;

(iii) Kuendelea kuzihamasisha sekta za umma na watu binafsi kuweka vifaa vya kuzimia moto kwenye majengo ili vitumike kuzima moto pale unapotokea;

(iv) Kuwahamasisha wafanyabiashara kuuza vifaa vya kuzimia moto sehemu mbalimbali nchini, ili wananchi waweze kuvinunua kwa urahisi wanapovihitaji; na

(v) Kutoa elimu ya kuzima moto kwa wananchi ili waweze kujua namna ya kutumia vifaa vya kuzimia moto pindi moto unapotokea.

Pamoja na jitihada hizi za ununuzi wa magari ya zimamoto na zana za kuzimia moto, pia juhudi zinafanywa za kuwanunulia askari wa zimamoto zana za kinga *(Protective Gear),* pia kuwaendeleza kimafunzo ili kuongeza ari na ufanisi wao wa kazi. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri na juhudi nzuri za Serikali, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa kitengo hiki cha zimamoto bado kina hadhi ya zimamoto kiasi ambacho hakipewi nafasi ya kuhudhuria hata kwenye vikao vya *MMT.* Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kukiinua kitengo hiki sasa kifikie hadhi ya kuwa idara kamili ili mkuu wao ahudhurie katika vikao vya *MMT* ili aweze kuyafikisha mahitaji ya askari wa zimamoto? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya ni miongoni mwa Halmashauri kubwa ambayo haina gari la zimamoto, Waziri atakuwa tayari sasa kuipa Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya, *priority* ya Ilemela na Temeke ili tuweze kutatua matatizo hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali inatazama upya suala la zima moto kuliwekea sera mpya, kuliwekea sheria mpya na muundo mpya. Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge, itazingatiwa katika kutazama mfumo mzima wa zimamoto ambao sasa hivi zoezi hilo linaendelea.

Kuhusu Mji wa Mbeya kukosa gari la zimamoto kwanza si sahihi kwamba Mji wa Mbeya hauna kabisa gari la zimamoto kwa sababu pale *airport* ya Mbeya kuna gari la zimamoto, ni dogo lakini linafanya kazi. Vile vile Manispaa ya Mbeya imefanya utundu mzuri tu wa kutumia gari la maji machafu, wamelirekebisha kwa kuliwekea *pump* liwe gari la zimamoto, kwa hiyo, lile gari linabeba lita 9,000 za maji baada ya kuwekewa *pump,* sasa linafanya kazi ya zimamoto na tunapongeza kusema kweli kwa utundu huo. *(Makofi)*

Mwisho, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Bunge hili wiki chache zijazo tutaliomba lipitishe shilingi bilioni 2.450 kwa ajili ya kununulia magari ya zimamoto kwa Manispaa mbalimbali ikiwemo Manispaa ya Mbeya. *(Makofi)*

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, kwa vile magari haya ni ghali na ni *product* maalum na kutokana na umuhimu wa hili tatizo la moto sasa hivi kwa nini Serikali isitiliane Mkataba na *suppliers* magari haya yakawa yanaletwa kwa awamu ili kila Halmashauri iweze inapata magari haya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli magari ya zimamoto ni ghali sana, yanaanzia shilingi milioni 300 na kuendelea kwa gari moja. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Serikali inajihidi kila mwaka kutenga fedha za kununulia na vile vile tunapenda kuzishukuru nchi mbalimbali ambazo zimekuwa vile vile zinatoa uhisani wa kusaidia magari ya zimamoto. Sasa kuhusu suala la kukopa kwa *suppliers,* ni wazo zuri, tutalitazama utekelezaji wake. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kama ifuatavyo: Kwa vile kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, magari mapya ya zimamoto ni ghali sana, lakini yapo magari ambayo ni *recondition* ambayo yanafanya kazi kama mapya na yanauzwa kwa bei rahisi sana. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba, badala ya kununua magari mapya tununue haya ambayo ni *recondition* na je, yuko tayari nimpe *catalogue* inayoonesha magari hayo na bei zake? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, inawezekana magari yaliyotumika yakawa na bei rahisi lakini sijui bahati mbaya au bahati nzuri, tulipitisha sheria sisi wenyewe humu humu katika Bunge hili, kuikataza Serikali kununua mitumba. Kwa hiyo, sheria ile ya manunuzi kusema kweli inatukataza tusinunue magari haya yaliyotumika.

Na. 93

**Mfuko wa Elimu kwa Watoto Yatima**

**MHE. STEPHEN M. KAZI (k.n.y. MHE. DR. BATILDA S. BURIAN)** aliuliza:-

Je, ni watoto wangapi kutoka katika kila Wilaya nchini wanaofaidika na Mfuko wa Elimu kwa ajili ya watoto yatima?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa kugharamia elimu ya sekondari kwa watoto wenye uwezo kimasomo, lakini wanaotoka kwenye familia zisizo na uwezo kiuchumi, ulianza rasmi mwaka wa masomo wa 2003. Katika mwaka wa kwanza Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 ambazo zilitosha kugharamia wanafunzi wa kidato cha kwanza 6,019 kwa nchi nzima. Karibu Halmashauri zote zilifikia lengo lao na kuwasilisha Wizarani kwangu majina ya watoto wa aina hiyo, isipokuwa Wilaya za Ilala na Temeke, ambazo kwa ujumla nafasi 58 hazikujazwa. Jumla ya shilingi 1,072,980,000 kwa ajili ya kusaidia watoto 5,961 zimekwishalipwa kwa ajili ya Halmashauri zote zilizoleta majina.

Mheshimiwa Spika, idadi ya walionufaika na mpango huu mwaka 2003na fedha zilizotengwa kwa kila Halmashauri zilionyeshwa kwenye jedwali ambalo liligawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote, wakati nilipotoa Kauli ya Serikali katika Bunge hili Aprili, 2003 wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge kuhusu mgawanyo wa fedha za kusaidia kugharamia Elimu ya Sekondari kwa watoto wa familia maskini. Mgawanyo hufuata uzito wa asilimia ya watahinikwa wa Darasa la VII wa kila Wilaya. Utaratibu huu umeendelea kutumika mwaka huu wa shule (2004) ambapo jumla ya Sh.2.5 bilioni zimetengwa kwa ajili hiyo. Mpaka wakati huu, wamelipiwa wanafunzi 6,034 wa kidato cha kwanza.

Kwa hiyo, jumla ya watoto 11,995 wamenufaika na Mfuko huu mwaka 2003 na mwaka huu wa 2004. Idadi ya wanafunzi kwa kila Wilaya kwa mwaka huu inameonyeshwa katika jedwali lililomo kwenye jibu la swali hili alilopewa Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa, katika bajeti ya 2004/2005 chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009), fungu kwa ajili hii limeongezwa mara dufu. Kwa hiyo, kuanzia mwaka 2005 watagharimiwa elimu ya sekondari watoto wa familia maskini 12,000 kwa mwaka. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, ambayo kwa kweli yameniridhisha, nina swali moja la nyongeza. Tatizo hili, linatugusa sana sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo yetu, watoto wanaohitaji msaada ni wengi sasa je, Wizara pamoja na mipango ambayo imeonyesha kwamba itaongeza namba ya watakaonufaika na mfuko huu, je, imejaribu kuainisha na kuona ni

maeneo yapi ambayo tatizo hili ni kubwa ili iweze kupeleka msaada zaidi kule kufuatana na hali halisi ya msaada wenyewe?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli si rahisi kusema tatizo hili la watu wasio na uwezo liko zaidi katika sehemu gani kwa sababu kwa kweli limezagaa katika nchi nzima. Kwa hiyo, Serikali imechukua hatua mbili, hatua mojawapo ni ile niliyoisema, kuongeza namba ya wale wanaosaidiwa kila mwaka kuwa 12,000 na naomba Waheshimiwa Wabunge waelewe kwamba, tukisema 12,000 kila mwaka maana yake kwa miaka minne kidato cha kwanza mpaka cha nne watafika 48,000 na kuna wanaoendelea mpaka kidato cha sita.

Kwa hiyo, namba hiyo ya 12,000 inabidi uipeleke mpaka mara sita. Kwa hiyo, ni fungu kubwa ambalo limewekwa katika jambo hili. Lakini hatua ya pili, ni ile ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, alilitaarifu Bunge hili katika hotuba yake ambayo ndiyo inajadiliwa hivi sasa aliposema kwamba, Serikali imedhamiria kupunguza ada. Kwa hiyo, kwa kuchukua hatua hii ya pili, upunguzaji wa ada utakuwa kwa nchi nzima, kiwekwe kiwango cha ada ambacho watu wengi wa kipato cha chini wataweza kuwapeleka watoto wao. Kwa hiyo, hili nitalifafanua hapo baadaye. *(Makofi)*

Na. 94

**Sekondari ya Wasichana Kondoa**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa ina vyumba vya madarasa, maktaba, maabara, nyumba za walimu za kutosha, mabweni na majengo mengine muhimu na kwamba kwa sababu hizo na nyingine inazo sifa za kutosheleza utaratibu wa kuanzisha kidato cha tano hadi cha sita:-

(a) Je, ni sifa zipi zinazotakiwa ili kuanzisha kidato cha tano na cha sita katika shule?

(b) Je, shule hiyo inazo sifa hizo na kama zipo, je itakubaliwa kuwa na kidato cha tano na cha sita?

(c) Kwa kuwa Serikali ilitoa ahadi ya kuondoa tatizo la maji shuleni hapo, je, ahadi hiyo imetekelezwa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili shule ya sekondari iweze kuanzisha kidato cha tano na cha sita mambo muhimu yafuatayo huangaliwa:-

(i) Yawepo majengo ya kutosha kama vile mabweni, maktaba, madarasa, nyumba za walimu na maabara kwa shule itakayofundisha masomo ya sayansi;

(ii) Wawepo walimu wenye sifa stahili au uwepo uwezekano mkubwa wa kuwapata walimu hao wa kufundisha masomo husika;

(iii) Shule iwepo katika eneo linalofaa kwa kuzingatia mchepuo wa masomo yatakayofundishwa ili iweze kuzinufaisha shule nyingine za sekondari katika eneo husika; na

(iv) Kuwe na idadi ya wanafunzi wa kutosha katika shule za sekondari za kawaida zilizoko jirani au katika kanda hiyo, ili shule inayoanzishwa iweze kuwapokea wanafunzi wapya watakaojiunga na shule hiyo bila kusafiri mwendo mrefu na kwa gharama kubwa, pia iwe kivutio kwa wanafunzi wanaohitimu shule za sekondari za kawaida kwenda kusoma pale.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa inazo sifa za kuanzisha kidato cha tano, Wizara yangu imepanga kuanzisha mikondo miwili ya kidato cha tano mwaka huu kwa mchepuo wa masomo ya sayansi. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka wa 2003/2004 imeipatia Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Kondoa jumla ya shilingi 10.1 milioni kwa ajili ya kurekebisha mfumo wa maji shuleni hapo. Kiasi hicho ndicho kilichokisiwa kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa majibu yake mazuri katika swali langu la msingi. Nilipotembelea Shule za Kwapakacha, Dereko, Mtela, Amani Karume iliyopo Pahi na ile Kondoa Wasichana, nilikuta kuna walimu walioajiriwa Januari, 2004 mpaka leo hawajapata mishahara. Je, ni kwa nini na Serikali inasemaje?

Pili, kwa kuwa hapa Kondoa ni kilomita 160 tu na Taasisi hizi zinamhitaji sana Waziri siku moja atembelee kule na hasa katika kipindi hiki tunapokuwa hapa Bungeni, je, Waziri anasema nini na wenyewe wasikie kama ahadi hiyo ataitoa?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu walimu aliowakuta katika Sekondari alizozitaja hawajalipwa mshahara, kwanza nasikitika sana kwa hali hiyo aliyoikuta. Wizarani tunafanya jitihada maalum kulipunguza hili tatizo, lakini tatizo hili lina muunganiko wa watu wanaotakiwa kuchukua hatua. Hatua ya kwanza inatakiwa ichukuliwe pale pale shuleni, kujaza fomu maalum ili kuweza kuonyesha kwamba mwalimu yule amekwishafika. Hii ni juhudi ya kuondoa walimu hewa. Lazima tuhakikishe kwamba, mwalimu amefika na *Headmaster* asaini kwamba amempokea. Wakati mwingine hatua hiyo inachelewa kuchukuliwa.

Halafu baada ya hapo fomu zinakuja Wizarani kwangu, lazima tuwasiliane tena na Idara Kuu ya Utumishi. Kwa hiyo, kuna mlolongo kidogo ambao unacheleweshа. Lakini kwa jitihada zilizofanywa napenda kumhakikishia kwamba, sasa tuko nyuma kwa karibu miezi miwili na tunaendelea kuongeza ufanisi katika kusimamia jambo hili ili tuweze kulimaliza kabisa la kuchelewa kulipa mishahara.

Kuhusu mimi kwenda Kondoa ni mwaliko mzuri kutoka kwa Ndugu yangu, Mheshimiwa Khalid Suru na tutapanga mara tukipata nafasi tuweze kwenda mara moja. Kwanza, sisi Wahehe na hawa ndugu zetu Warangi tuna undugu wa tangu enzi za Mkwawa, utani ule wa kuviringishana. Kwa hiyo, nitafurahi kufika huko. *(Kicheko/Makofi)*

Na.95

**Madeni ya Tanzania Kabla ya Mpango wa HIPC**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA (k.n.y. MHE PHILIP A. MAGANI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Benki ya Dunia na *IMF* sasa zimekubali Tanzania iwe miongoni mwa nchi maskini za kufutiwa madeni *(HIPC)* baada ya kukamilisha vigezo vyote vinavyotakiwa:-

(a) Je, madeni ya Tanzania yalikuwa kiasi gani kabla mpango wa *HIPC* haujaanza?

(b) Je, ni madeni kiasi gani yamefutwa mpaka leo?

(c) Je, madeni ya Tanzania hadi sasa ni kiasi gani yakijumuishwa yale yaliyobaki baada ya kuingizwa katika mpango wa *HIPC?*

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Philip Magani, Mbunge wa Ruangwa, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, 4 Aprili, 2000 Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* walifikia uamuzi wa kuipatia Tanzania unafuu wa madeni chini ya Mpango wa *Enhanced HIPC Initiative.* Uamuzi huo pia uliridhiwa na kundi la Paris hapo 14 Aprili, 2000 ikiwa ni katika kutambua juhudi za Serikai ya Tanzania katika kufufua uchumi na kupiga vita umaskini.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha msamaha wa madeni kilichotegemewa ni Sh. 1.6 trilioni, sawa na Dola za Kimarekani bilioni 2 kwa thamani ya sasa *(Present Value Terms).* Msamaha huu unatoka Benki ya Dunia jumla ya Sh.960 bilioni, *IMF* jumla ya Sh. 121.6 bilioni na *Paris Club* jumla ya Sh.880 bilioni. Utaratibu huo unatarajiwa

kupunguza takribani nusu ya deni ambalo Serikali ingetakiwa kulipa katika mwaka 2000/2001 - 2002/2003 na hatimaye kupunguza theluthi moja ya kiasi ambacho kingetakiwa kulipwa baada ya hapo.

Hata hivyo, Serikali ilipewa masharti ambayo yangetekelezwa ili kuiwezesha Tanzania kufikia hatua ya mwisho *(Completion Point)* katika mpango huu wa *Enhanced HIPC.* Masharti hayo yanajumuisha kuendeleza sera nzuri za uchumi na fedha na Utawala Bora. Serikali iliweza kuyatekeleza masharti hayo na kufanikiwa kufikia hatua hiyo Novemba 27, 2003.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philip Magani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Tanzania iliingia katika Mpango wa *HIPC* Aprili, 2000 na wakati huo kwa takwimu za Juni, 1999, Serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh.7,076.8 bilioni na kati ya deni hilo, Sh.3,795.1 bilioni ni deni la Asasi za fedha za Kimataifa, Sh.2,209.7 ni deni la Kundi la Paris, Sh.957.7 bilioni ni deni la kundi lisilo la Paris na Sh.3,958.7 bilioni ni deni la Asasi za Kibiashara.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa Machi, 2004 madeni ya jumla Sh.3,269.1 bilioni yalikwisha samehewa. Kati ya fedha hizo Dola za Kimarekani 2,665.9 milioni ni kutoka nchi 12 kati ya 13 za Kundi la Paris ambazo tayari zimeshasaini Mkataba na Serikali na Dola za Kimarekani 195.4 milioni toka Asasi za fedha za Kimataifa. Tanzania pia imepata misamaha ya madeni toka nchi wahisani ambao si wa Kundi la Paris zinazofikia Dola za Kimarekani 88.1 milioni. Nchi hizo ni India, Misri na China. Hata hivyo, kiasi hicho cha msamaha hakihusishi thamani ya msamaha kwa madeni yaliyoongezewa muda wa malipo *(Rescheduled Debt)* na madeni yanayosamehewa chini ya utaratibu wa kupevuka kwa madeni *(Debt Service Reduction)* kwa sababu madeni haya yataendelea kusamehewa hatua kwa hatua kadri yanavyopevuka.

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya deni la nje hadi kufikia mwishoni mwa Machi, 2004 lilikuwa Sh.7,990.1. Hata hivyo, deni hili ni kubwa kuliko ilivyokuwa kabla ya *HIPC* kwa sababu zifuatazo:-

(i) Serikali inaendelea kukopa ili kutekeleza miradi mbalimbali ya uchumi ambayo haiwezi kutekeleza bila mikopo ya nje. Hata hivyo, mikopo ambayo imekuwa ikiombwa ni ya masharti nafuu kama mkakati wa kusimamia deni la Taifa unavyoagiza na kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu tarehe 8 Juni, 2004;

(ii) Unafuu wa madeni unaotolewa kwa njia ya kupevuka kwa deni *(Debt Service Reduction)* hasa ule unaotolewa na Asasi za Kimataifa utaonekana tu pindi kipindi cha kupokea msamaha huo kitakapomalizika. Kwa maana hiyo, msamaha uliotegemewa haujakamilika ili deni liweze kupungua; na

(iii) Nchi ya Brazil ambayo ni Kundi la Paris bado haijasaini Mkataba chini ya *Paris Club VII* kati yake na Serikali, pamoja na nchi ya Japan ambayo haijatoa msamaha kamili. Hivyo, bado inachangia kwa kiasi fulani kutopungua kwa deni la nje.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kufuatana na majibu ya Waziri wakati akijibu hoja za Wabunge kwenye bajeti yake ya mwaka huu alisema kwamba, tusiogope kukopa vizazi vitakuja kulipa baadaye. Je, utaratibu wa kukopa, kulipa na kusamehewa ni zoezi la kudumu?

Pili, Waziri haoni kwamba wale wanaotusamehe wanapoona tunaendelea kukopa baadaye watakuwa na mashaka kwa kudhani kwamba wanaweka maji kwenye debe lililotoboka?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, hao hao waliotukopesha na ambao ndiyo hao hao waliotusamehe, ndiyo hao hao wanatukopesha leo. Kwa hiyo, wanaelewa tunachofanya.

Pili, niliposema kwamba wajukuu watalipa, nilitaka kuondoa wasiwasi kwamba, tunakopa leo na kulipa leo leo kama ilivyo kwenye benki. Ukikopa fedha leo kuendesha mradi wako, utatakiwa ulipe upesi upesi. Lakini mikopo hii ya Kimataifa inalipwa miaka mingi baadaye, miaka 40 na zaidi na mara nyingine unaanza kulipa miaka 10 au zaidi baada ya kukopa. Kwa hiyo, ni muda mrefu wa kujiandaa na kwa maana hiyo, miaka 40 kuanzia leo wengi hapa tutakuwa na wajukuu wenye uwezo wa kufanya kazi na kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Na. 96

**Mfuko wa Pembejeo**

**MHE. ABU T. KIWANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeshindwa kuandaa fungu la kutosha kwenda kwenye Mfuko wa Pembejeo kwa sababu Mfuko huo haukuweza kuzungusha fedha iliyomo ndani yake kikamilifu kwa marejesho hata baada ya kukabidhi taratibu za ukopeshwaji kwenye Benki binafsi kama vile *Exim Bank Tanzania Limited:-*

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kukuza Mfuko huo kutoka shilingi bilioni moja nchi nzima hadi kufikia angalau shilingi bilioni kumi na tatu ambazo ni takribani nusu bilioni kwa kila Mkoa hasa ile iliyo na uwezo wa kukuza sekta hiyo na kukasimisha madaraka hayo kwenye Ofisi za Kilimo za Mikoa ili kutoa mikopo hiyo kupitia *Sub-Treasury?*

(b) Kwa kuwa taratibu zilizojionyesha kwenye kukabiliana na baa la njaa mwaka 2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilionyesha kuyumba sana juu ya suala la akiba ya kutosha kwenye *National Strategic Grain Reserve (SGR),* kiasi cha kuwa na matumizi yasiyotosheleza mahitaji ya nchi hata kwa siku moja. Je, Serikali ina mpango

gani wa kuhakikisha kuwa *(SGR)* hapo baadaye itakuwa na akiba isiyopungua mahitaji ya nchi angalau ya miezi mitatu au zaidi sambamba na uwezo wa *imports* kwa miezi mbadala kama ilivyoainishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mazingira yaliyoifanya Serikali kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na madhumuni ya Mfuko huo, yalilenga kuondoa tatizo la ukosefu wa utaratibu na mikopo ya kuwezesha pembejeo kumfikia mkulima ambalo ni moja katika matatizo mengi yanayodumaza kilimo. Kwa kutambua tatizo hilo, mwaka 1994, Serikali iliamua kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ambao ungewapa wasambazaji wa pembejeo *(Stokists),* mikopo ambayo ingewawezesha kumfikishia mkulima pembejeo na Mfuko haukukusudiwa kutoa mikopo kwa mkulima mmoja mmoja.

Hadi mwaka 1998/99, Serikali ilikuwa imeupa Mfuko wa Pembejeo wa Taifa jumla ya shilingi bilioni 5.8. Mfuko ulikumbwa na matatizo ya wakopaji wengi kutokutumia mikopo kwa madhumuni yaliyokusudiwa, kutokurejesha mikopo kwa wakati na baadhi yao kutorejesha kabisa.

Katika jitihada za kupunguza tatizo hilo, mwaka 2001, Serikali iliamua kutumia mabenki na vyombo vingine vya fedha kutoa mikopo hiyo. Aidha, kati ya mwaka 2002/2003 na 2003/2004, Serikali imeupa Mfuko jumla ya shilingi bilioni 6.1 na katika mwaka wa 2004/2005, Serikali italiomba Bunge lako Tukufu kuuongezea Mfuko shilingi bilioni 3.0. Kadri uwezo wa Serikai utakavyoongezeka ndivyo Mfuko wa Pembejeo utakayoongezewa uwezo wa kutoa mikopo. Serikali haikusudii kukasimu madaraka ya kutoa mikopo ya pembejeo kwa Sekretariati za Mikoa kwa kuwa Sekretariati hizo hazina ujuzi wala uzoefu wa kutoa na kusimamia mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Waziri wa Fedha katika Hotuba yake ya Bajeti ya 2004/2005, Serikali inakusudia kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo itasimamia mikopo kama ile inayotolewa na Mifuko mbalimbali hivi sasa ili kuondoa matatizo mengi yaliyopo.

(b) Lengo la Hifadhi ya Chakula ya Taifa ni kuhifadhi chakula kitakacholiwezesha Taifa kukabiliana na dharura zinazoweza kutokea kwa muda ili kuipa Serikali nafasi ya kuagiza chakula kwa wingi kutoka nje. Haikusudiwi na wala haiwezekani kuwa na hifadhi ya chakula itakayotosha kuwalisha Watanzania wote kwa kipindi cha urefu wowote ule.

Katika mwaka wa 2004/2005, Serikali inakusudia kununua kiasi kikubwa cha nafaka kuliko ilivyowahi kutokea katika miaka iliyopita kwa lengo la kuwapatia wakulima soko la nafaka hizo na kuwa na chakula kingi zaidi kitakachotumika ikitokea

dharura. Ufafanuzi zaidi utatolewa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2004/2005.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa sababu tumeshaona matokeo ya mikopo hiyo kwenye benki ambazo zimekabidhiwa kazi hiyo ni kuwa mikopo hiyo haikutolewa au kama kiasi kinatolewa ni kidogo zaidi. Je, Serikali ina azma gani juu ya kiasi hicho cha mikopo kinachobaki kwenye benki hizo ambazo hazikopeshi watu?

Pili, kama kuna riba hiyo riba inakwenda wapi, inasaidia kukuza Mfuko huo ili watu wengi waweze kukopeshwa zaidi pamoja na kutambua kuwa kitu kimoja kinachosababisha kutokukopesha mikopo hiyo ni kwa benki hizo kutumia *Valuers* wao wenyewe kutathmini thamani ya zamana za kukopea? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwa taarifa zilizopo mikopo yote iliyotimiza masharti na kuthibitishwa inatolewa na kwa sasa hivi kuna benki au utaratibu wa Taasisi za Fedha kama tano. Kuna *Exim Bank, SCCULT,* yaani muungano wa *SACCOS, Mufindi Community Bank, Kagera Co-operative Bank* na *Kilimanjaro Co-operative Bank.* Sasa inawezekana kati ya hizi zitakuwa na matatizo fulani fulani. Sasa kwa kuwa haikuainishwa nina shida kuyashughulikia. Lakini wote walioomba na wakatimiza masharti kwa kawaida hupata mikopo. Halafu wapi inaenda hiyo *interest,* sehemu kubwa inarudi kule lakini baadhi ya *interest* inatumika katika uendeshaji wa benki yenyewe kwa sababu kuna gharama, makaratasi na Maafisa wanaoshughulikia mikopo hiyo, hiyo riba huenda huko. *It is proud* lakini nyingine inatumika. *(Makofi)*

Na. 97

**Umeme Kijiji cha Malya**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Nishati ni kuhakikisha kuwa Vijiji vinapatiwa umeme na kwa kuwa Miji ya Ngudu, Bukwimba na Malampaka ina umeme lakini Kijiji cha Malya kilichozungukwa na miji niliyoitaja hapo juu hakina umeme:-

(a) Je, ni kitu gani kinachosababisha Kijiji cha Malya kisipate umeme?

(b) Je, ni lini kilio cha wakazi wa Kijiji hicho kitamalizika?

(c) Kwa kuwa wananchi wa Malya wana fedha zao za kuchangia gharama za umeme, je, Serikali inasemaje kuhusu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikishughulikia suala la umeme wa Malya kwa pamoja na Sumve ambako pia hakuna umeme kama ambavyo Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Richard Ndassa, amekuwa akiuliza Bungeni na kufuatilia. Kutokana na mpango huo wa pamoja wa umeme wa Sumve na umeme wa Malya, Serikali iliahidi kupeleka umeme kwa awamu, kwa kuanzia na Sumve na baadaye Malya, kwa kadri fedha zinavyopatikana. *(Makofi)*

Utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Sumve umeshaanza rasmi tarehe 14 Juni, 2004, baada ya kupatikana vikombe 1,000 kutoka Dar es Salaam na hivyo kukamilisha orodha ya vifaa vilivyokuwa vinahitajika. Hadi sasa nguzo zaidi ya 50 zimeshapelekwa sehemu za kazi na mashimo yameanza kuchimbwa kuanzia Sumve. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa genge la mafundi linalofanya kazi huko Sumve ndilo hilo hilo litakatofanya kazi Malya, inabidi kazi ya kupeleka umeme Sumve ikamilike kwanza na halafu kazi ya kupeleka umeme Malya ndio ianze. Aidha, kazi ya kupeleka umeme Malya itaanza kutekelezwa baada ya maandalizi ya kupima njia ya umeme pamoja na ununuzi wa vifaa vya kujengea laini ya umeme kukamilika. Kazi hii inatarajiwa kuanza mwaka huu huu wa 2004 na kukamilika mwaka 2005, ambapo tunatarajia kilio cha Wakazi wa Malya kupatiwa umeme kitamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha walizonazo Wakazi wa Malya za kuchangia gharama za umeme, kwanza, Serikali inawapongeza wananchi hao kwa kutenga fedha. Shirika la Umeme *(TANESCO)*, limeshaweka kazi ya kupeleka umeme Malya katika programu yake ya kazi ya mwaka 2004, kama ambavyo nimeshaeleza. Hata hivyo, ikiwa michango ya wananchi wa Malya ni ya kuwasaidia *TANESCO* katika kujenga laini ya umeme wa Malya, basi hilo linazungumzika na litaiwezesha *TANESCO* kutumia bakaa itakayotokana na Mradi wa Malya kupeleka umeme mahali pengine. Aidha, ikiwa wananchi wa Malya wameweka fedha za kulipia gharama za kuunganishia umeme katika majengo na nyumba zao, ambao ni wajibu wao wa kisheria, kwa kila mtu atakaye fungiwa umeme na sio mchango, basi Serikali inaomba wananchi wa Malya watunze michango yao hadi wakati wa kulipia gharama hizo utakapofika.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru sana Wizara hii katika ufuatiliaji wa kuhakikisha kwamba wanatekeleza sera yao ya kuhakikisha vijiji vinapata umeme. Lakini naomba tu nichukue nafasi hii labda nimwulize swali dogo tu la nyongeza. Katika jitihada hizo kama sekta ya elimu na afya zilivyofanya kuanzisha Mifuko kwenye afya na elimu katika kuhakikisha wananchi wanachangia maeneo yao kwa kujenga maboma. Je, kwa nini Sekta hii basi isianzishe angalau Mfuko ambao utakuwa wa dharura wa umeme ili kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na kianzio chao zoezi hilo litakapofikia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika sekta ya nishati, Serikali imeandaa mpango kamambe wa kuanzisha Mfuko wa Umeme Vijijini na taasisi ya kushughulikia umeme vijijini. Tumeshawahi kufanya semina hapa Bungeni kuhusu masuala haya. Nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kuwa, wavute subira kidogo mpaka wakati ambapo Mfuko huo utaanzishwa rasmi.

Na. 98

**Umeme Wilaya ya Bukombe**

**MHE. ROBERT K. MASHALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango kamambe wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote ambazo hazina umeme nchini ikiwemo Wilaya ya Bukombe na kwa kuwa wananchi wa Bukombe hawajui jitihada zinazofanywa na Serikali ikishirikiana na Mbunge wao kuhakikisha kuwa umeme unafika Wilayani humo kabla ya mwaka 2005 kama Serikali ilivyoahidi kwenye swali Na.48 lililojibiwa tarehe 5 Feburari, 2001.

Je, Serikali inasema nini juu ya hatua zilizofikiwa za kupeleka umeme kwenye Mji wa Ushirombo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe na Miji Midogo ya Masumbwe, Uyovu na vijiji vingine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Kaji Mashala, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Serikali imekuwa ikitekeleza mpango kamambe wa kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Mpango huo wa Serikali umetokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, ambayo katika Ibara ya 51(iii) imeahidi, napenda kunukuu: "kutoa kipaumbele katika usambazaji umeme katika Miji Mikuu ya Wilaya iliyobaki."

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000, Wilaya 18 wakati huo hazikuwa na umeme na hadi sasa Wilaya 13 kati ya hizo 18 za mwaka 2000 ama zimepata umeme au ziko njiani kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ushirombo, Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe ni moja ya miji ambayo haijapata umeme. Kama nilivyosema wakati najibu swali Na.124 la Mheshimiwa Parseko Kone katika Bunge lililopita, kazi ya awali ya kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Machi, 2004, Kampuni ya Mgodi wa Dhahabu ya Kahama iliingia Mkataba na *TANESCO* wenye awamu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu Kampuni ya Kahama kulipia gharama zote za kujenga kituo cha umeme chenye ukubwa

wa *MVA* 10, cha kupunguza umeme kutoka msongo wa *kV* 220 hadi *kV* 33 kwenye eneo la machimbo ya dhahabu ya Bulyanhulu Wilayani Kahama na kusafirisha umeme huo mpaka kwenye makazi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Kahama ya Bugarama na Ilogi. Hivi sasa Mkandarasi wa kujenga kituo hicho cha umeme amekwishaanza kazi. *TANESCO* inajiandaa kutekeleza sehemu yake ya makubaliano ambayo ni kujenga njia ya umeme wa kilovoti 33 kwenda makazi ya Ilogi na Bugarama kutoka Mgodi wa Kahama.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili na awamu inayofuata, ni kufikisha umeme Ushirombo kutokea Ilogi. Hivi sasa Serikali inafanya mashauriano na wafadhili kwa ajili ya kupata fedha za kukamilisha awamu hii ya pili ya kuufikisha umeme Ushirombo pamoja na kusambaza kwenye miji ya jirani na vitongoji vyake kama vile Masumbwe na Unyovu. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni tatu. Ni matumaini ya Serikali kuwa fedha hizi zitapatikana haraka ili Mradi utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, kwa ushirikiano wake na Serikali na juhudi zake za kufuatilia utekelezaji wa Mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri na yenye kutia matumaini ambayo kwa kweli nadhani wananchi wa Bukombe wameyasikia lakini napenda niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa awamu ya kwanza imeanza na awamu ya pili itaanza hivi karibuni, je, awamu hii ya pili itachukua muda gani na lini zoezi la kupeleka umeme Bukombe litakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza katika jibu la msingi, Serikali iko katika mashauriano na wafadhili kuhusu kupatikana kwa fedha za Mradi huu. Napenda niseme kwamba, yapo matumaini makubwa kwamba fedha hizi zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muda gani utatumika katika kujenga njia hii ya umeme, kwanza awamu hii ya kwanza ambayo ni muhimu sana bila awamu hii ya kwanza hata awamu ya pili haiwezi kutengenezwa, awamu hii ya kwanza tunategemea itachukua karibu mwaka mzima huu tunaokwenda nao na baada ya mwaka mmoja tunategemea taratibu hizi zitakuwa zimekamilika na pesa zitakuwa zimepatikana ndio tutaanza awamu ya pili ambayo pia tunategemea ifikapo pengine mwaka 2005 au 2006 Mradi huu wa umeme utakuwa umekamilika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa.

Matangazo ya vikao vya leo, Kamati mbili zimepangiwa kukutana leo ya kwanza ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane mara baada ya kipindi cha maswali na majibu katika chumba cha Kamati Na.227, ghorofa ya pili. Kamati nyingine ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa

George Lubeleje anaomba Kamati hiyo ikutane saa saba mchana kwenye ukumbi Na.131, ghorofa ya kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, lingine nimekuwa nikipata maswali kutoka kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliojiandikisha kuchangia wakisema kwamba, mbona katika orodha ya leo hawapo. Sasa maelezo ni kwamba, kama nilivyosema jana maombi yalikuwa 58 na Wizara hii au Ofisi ya Waziri Mkuu imepangiwa siku tatu yaani jana, leo na kesho, kwa hiyo, ilibidi tuwapange katika makundi matatu kundi la jana, la leo na kundi la kesho. Sina hakika kama wote 58 watapata nafasi lakini jibu kwa wale wanaouliza mbona hawako kwenye orodha ni kwamba, bado mjadala utaendelea kesho. Kwa hiyo, tuvute subira.

Mpango ni kwamba, hiyo kesho itabidi Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake wa Nchi, wachukue nafasi ya kipindi cha mchana kujibu hoja zilizowekwa mbele ya Bunge katika mjadala huu. Mara nyingi mimi nawasikia Mawaziri wakisema tumesikia ushauri, ushauri huu tutaufanyia kazi, hiyo inaashiria kwamba, hata ile michango ya maandishi nayo inathaminiwa na Serikali. Kwa hiyo, ni vizuri ukikosa kuchangia kwa mdomo usikate tamaa bado unaweza kuchangia kwa maandishi na Serikali itaufanyia kazi mchango wako na michango ya maandishi inaingia kwenye *Hansard* sio kwamba inatupwa kapuni.

Mwisho wa matangazo, Katibu tuendelee na *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 - Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo imetupa maelezo mengi sana ya jitihada ambayo ameifanya kwa kipindi cha mwaka mzima kuhusiana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Moja kwa moja naiunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nitumie nafasi hii kuwapongeza wana Bariadi Mashariki wote, kwa kumrejesha ndugu yetu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kura nyingi sana na za heshima. Nampongeza kwa sababu maelezo ambayo ameyatoa juzi na jana yametudhihirishia kwamba, huyu alikuwa ni mwana-CCM kweli ila hapa katikati ndio maisha yalivyo alitoka lakini amerudi katika kundi la wana-CCM wenzake. Tunakukaribisha kwa moyo mkunjufu na tutaendelea kushirikiana nawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwapa pole Wabunge wenzetu ambao walipata maafa na majanga mbalimbali, Mwenyezi Mungu, aendelee kuwapa kila la kheri wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, pia nawapongeza Mawaziri wetu wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao nzuri walizozitoa. Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ndugu yetu, Mheshimiwa Athumani Janguo, pamoja na Kamati nzima kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuchambua Muswada na Hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wa Nchi, Katibu Mkuu, pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ina vitengo vingi. Safari hii nitavizungumzia vitengo vichache. Katika hotuba ya mwaka 2003 nilimwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, waangalie uwezekano wa kupunguza baadhi ya vitengo. Waziri Mkuu ni kiungo kikubwa na msimamizi wa shughuli zote za Serikali. Hatutegemei awe na vitengo vingi ambavyo wakati mwingine vitamharibia hata heshima yake. Vitengo vinapokuwa vingi vinapoharibu anayelaumiwa ni Waziri Mkuu. Ndio maana huwa tunapenda angalau vitengo vingine kama afya viende kwenye Wizara ya Afya, kama ni madini viende kwenye shughuli za madini ili Waziri Mkuu afanye kazi yake vizuri ya kuangalia utendaji wa kazi katika Wizara zote kuanzia Wizarani mpaka Mikoani. Hii itampa nafasi nzuri ya kufanya kazi kuliko kushughulikia matatizo mara ya njaa. Wakiiba chakula wanasema Ofisi ya Waziri Mkuu imeiba chakula. Kwa nini tunamfikisha Waziri Mkuu wetu katika hali hiyo? Naomba hilo liangaliwe katika sura hiyo mpya ya kumsaidia Waziri Mkuu afanye kazi yake vizuri, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kutumia nafasi hii kuwapongeza wasaidizi wa Waziri Mkuu wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tarafa na Makatibu Kata, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maeneo yao. Naelewa Waziri Mkuu hawezi kufanya kazi peke yake, wasaidizi wake wanamsaidia na sisi ambao tulishawahi kufanya kazi ya Ukuu wa Mikoa, tunajua matatizo ya kuwa Mkuu wa Mkoa. Mkiona nchi imetulia kuna watu wanafanya kazi msidhani yanatokea tu. Kuna watu hawalali wanafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuna ulinzi na usalama. Lakini utakuta watu wanalalamika hatuoni faida ya watu wengine. Ngojeni yawatokee ndio mtaona faida yao. Mimi siombi yawatokee kwa sababu naona umuhimu wa viongozi hawa kuwepo. Kama kuna matatizo tutawasaidia kurekebisha matatizo hayo na kazi ya Bunge ni kuwaambia ukweli hapa mmevuruga, hapa mmefanya kazi. Mheshimiwa Waziri Mkuu endelea kuwapa kila *encouragement* ili wasaidizi wako wakufanyie kazi yako vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mengi ya kuchangia na bahati mbaya mimi kwa sababu niko katika Kamati ya *PAC* yako mengi ambayo nashughulikia kwa mfano, matatizo ya TVT, chakula cha njaa na *TACAIDS.* Siwezi kuyazungumzia kwenye kikao hiki kwa sababu Kamati yetu tunajaribu kuchunguza kuona matatizo yako wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja nitazungumzia suala zima la sera. Kwanza nikupongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kutuletea Sera ya Uwezeshaji. Ni kati ya sera ambazo nimefurahishwa sana. Nimefurahishwa nayo kwa sababu kubwa

mbili. Mwaka 1997, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka mimi nikiwa Waziri wa Kilimo alituagiza tuandae Sera ya Uwezeshaji. Sera ya Uwezeshaji kama ni *sample.* Tuliiandaa tangu mwaka 1997. Tulijiuliza hivi uwezeshaji maana yake nini. Tukatoa tasfiri, maelezo yake na tulitaka kuhakikisha kweli tunapozungumzia uwezeshaji kilimo kisiwe cha watu wa vijijini peke yao bali na wataalam wajiingize katika kilimo. Tulitoa mapendekezo hata baadhi ya vijana ambao wanamaliza Vyuo Vikuu suala sio kutafuta ajira. Waingie katika shughuli za kilimo. Kama ni wataalam wa mifugo waingie katika shughuli za mifugo, tusiache zikaonekana ni kazi za babu zetu. Hao vijana ambao wanakuja na utaalam, tunawafundisha kwa nini wasianze kuingia katika kilimo tukasema tuanze. *(Makofi)*

Bahati nzuri kwa taarifa yako Mheshimiwa Spika, tulipata *support* kubwa sana kutoka *World Bank* na *World Bank* kupitia Sweden wakakubali kwa kuanzia wangeweza kutoa dola milioni mbili kwa wataalam wa kilimo watakaotaka kuingia katika shughuli za kilimo ili kuwawezesha. Tulikuwa hatuna Mfuko, wakasema tunaweza kuanzisha. Wataalam wa mifugo nao wachukue baadhi ya mashamba ili uwe ni mwanzo wa kuwezesha tuone tutafanya namna gani. Bahati mbaya nadhani ilichelewa kidogo na uwezeshaji sisi tulitaka uende katika hali ambayo naona imebadilika kidogo katika sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yako sisi katika *empowerment process* tuliandika hivi: *"Without any kind of fear or shyness, the Government should urgently put into place a deliberate transparent and bold policy on empowerment of indigenous Tanzanians to formulate strategies and legal framework that which shall enable implementation of the policy."* Tunapozungumza juu ya *empowerment,* kuwawezesha wananchi, lazima yafanyike makusudi mazima bila woga, bila kumwogopa mtu yeyote tunaamua kuwasaidia Watanzania, sasa tunamwogopa nani? Tuliona tuanze nayo hiyo. Sera imeandikwa vizuri sana nimefurahi tutakuwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji na mimi ninachoogopa muda hatuna, muda uliobaki ni kidogo lazima *speed* iongezeke ndio maana nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo matatu. *(Makofi)*

Kwanza, kama inawezekana tuhakikishe kwamba, sasa sheria inatungwa na kama inawezekana ije isomwe hata mara ya kwanza kwenye kikao cha Novemba, 2004. Tunataka Mheshimiwa Waziri Mkuu hata ukiondoka baada ya kipindi chako tutakuombea Mungu ukusaidie uendelee kuwa kiongozi lakini uhakikishe kwamba, kazi uliyoanzisha ya *empowerment of the indigenous Tanzanians* unaitekeleza katika kipindi chako hiki. *(Makofi)*

La pili, tunaomba fedha zitafutwe kwa njia yoyote, ili utaratibu wa kuandaa kwanza mikakati ya utekelezaji kuwe na chombo kitakachosimamia utekelezaji. Nimejaribu kuangalia katika *vote* yako sikuona mahali popote ambapo *empowerment* imepewa hata senti tano labda kama itaingia katika *general administration*. Ni vizuri zikatafutwa fedha. Najua zamani tulikuwa na mpango wa kutumia fedha za ubinafsishaji tukawa na fungu maalum zitakazotumika kuwasaidia wananchi ili kuwawezesha lakini bahati mbaya nadhani fedha hizo zilitumika kwa dharura na shughuli nyingine lakini tungeweza kutafuta njia yoyote ya kupata fedha hizo na sio tatizo, Serikali ikiamua itazipata tu, nataka tuwe na Mfuko wa kusaidia kufanya kazi hiyo.

Mwisho, kama inawezekana naomba tuanze kufikiria kwa makusudi kabisa tukianzisha Baraza hilo liwe tena si la Serikali, la kuingiliwa na Serikali kila wakati hatutafika mahali popote. Kiwe ni chombo kama mlivyoanzisha kwa mfano, *TRA* ikawa *independent*, haimwogopi mtu, kodi imekusanywa vizuri sana. Nina imani kabisa tukiwa na chombo ambacho kitasimamia mambo ya *empowerment* bila kuingiliwa na Serikali kitafanya kazi yake vizuri sana. Ni vizuri tukatafuta watu wenye uwezo, wenye uchungu na nchi hii, wenye msimamo na mwelekeo wa kibiashara watusaidie. Nasema hilo kwa sababu naona muda wenyewe umekwisha, hatuna muda wa kusubiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, tazama namna ya kuharakisha chombo hiki tukianzishe haraka kwa kisheria. *(Makofi)*

Lingine ni sera ambayo inahusiana na akina mama na watoto. Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka kukuambia kwamba, katika Afrika akina mama kufa kwa uzazi limekuwa kama ni jambo la kawaida. Tanzania zaidi ya akina mama 520 kati ya 100,000 wanakufa kwa tatizo la uzazi maana yake ni akina mama 15,000 wanakufa, hivi kweli tunakubali? Profesa mmoja wa *World Bank* anaitwa Profesa Zai anatoka Ghana alisema siku hizi akina mama wanaweza kufanya kazi zozote ambazo mwanaume anafanya na tume-*prove* hivyo. Wape nafasi, wape elimu watafanya. Lakini anasema akina mama wanaweza kufanya kazi zaidi kuliko hata zile ambazo mwanaume anaweza akatoa mfano, *which is very clear,* akasema kitu ambacho mwanamke anaweza kufanya mwanaume hawezi ni kwamba, mwanamke ana uwezo wa kubadilisha *cell* moja kikaja kutokea kiumbe, *cell* moja tu ikaingia, akaitengeneza ikatokea kiumbe. Ni mwanaume gani anaweza kazi hiyo?

Akasema hiyo tunaisema makusudi kwa sababu kazi ya akina mama ni kutengeneza na kutuzalia watoto na ndio wanaojenga Taifa hili. Hivi kwa nini tunashindwa kuwasaidia ili wazae watoto ambao wana afya na maendeleo mazuri. Ni kiwanda ambacho peke yake kinahitaji chakula bora tu. Ni vizuri tukaliangalia hilo kama imewezekana tulikuwa na Mradi wa MMEM kwa nini tusiwe na Mradi wa MMAM ni Maendeleo ya Mama na Afya ya Mtoto. Ukija katika maeneo yetu vijijini, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi hali ya hospitali zetu, zahanati zetu, vituo vyetu vya afya, kwa kweli viko hoi, akina mama wanapata shida kubwa sana na hili ndio Taifa lenyewe, wanatujengea Taifa la kesho. Ni vizuri tukaliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, nina maombi karibu manne. Kwanza, naomba Sera ya Idadi ya Watu tuanze kuitekeleza sasa, ni karibu miaka 12 tangu itolewe haijafanyiwa kazi yoyote. Kamisheni iliyosemwa kwamba itaanzishwa haijafanya kazi na ndio maana mzigo wote unakuja Ofisi ya Waziri Mkuu. Matatizo yakitokea ni Ofisi ya Waziri Mkuu. Kamati yetu na Umoja wa Wabunge ambao wanashughulika na idadi ya watu kila wakati wamekuwa wakiomba hii Kamisheni kwa nini isianzishwe? Tuko zaidi ya Wabunge 150 ili kushughulikia suala hili tusaidiane na Serikali ili kufanikisha ili hata azma ya maendeleo ya watu wetu ipate msukumo kutoka nje kidogo kuliko kutegemea utaratibu wa Bunge kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi la pili, mtandao wa ulimwengu wa Soko Huria na utandawazi, utatuletea matatizo makubwa. Kuna umuhimu sana wa kuzungumzia *Migration Policy*, sasa hivi watu wanaingia nchini ovyo ovyo. Tuna hatari tusipojiandaa vizuri, tukawa na sera ambayo inasema wazi utaratibu upi tutautumia, tutashtukia sasa hapa ni *center* ya vichaka vya kila aina ya watu. Lazima tuwe waangalifu tuanze kuifikiria hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba Mkoa wa Rukwa safari hii kwa vile tuna chakula cha kutosha *SGR* waje mapema sana kununua chakula Mkoa wa Rukwa. Mwaka huu bado tuna matatizo, Mheshimiwa Waziri Mkuu umesema mwenyewe tutakuwa na matatizo ya chakula. Mkoa wa Rukwa una chakula cha kutosha na majirani sijui wamepata chakula, tununue chakula cha kutosha tuache tabia ya kuendelea kuombaomba kwa wageni. Nilishangaa tumeomba chakula Zambia, tumeomba Ethiopia ambapo wao ndio wana njaa karibu kila mwaka kwa nini tunafikia hapo? Tununue chakula chetu na Mikoa yote ambayo imezalisha tununue tuwe na chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni haki za msingi za wananchi. Naomba sana vyombo vya habari vipatiwe nafasi ili kupunguza gharama zao kama kuna haja ya kupunguza kodi katika vyombo vya habari ikiwezekana karatasi wafikiriwe sana kwa sababu kupata habari ni haki ya Kikatiba ya kila nchi. Tukiweka kodi kubwa wengi watashindwa hata kununua magazeti. Leo tumeambiwa Waafrika ni wavivu sana kusoma wakati mwingine sio wavivu kwa sababu gazeti hilo wanataka wasome watu 20 kwa sababu *they can't afford.* Siku hizi magazeti yaliyokuwa ya Sh.100 mengine yamefikia Sh.150, hii ni kutokana na gharama za kuendesha shughuli zao. Mtu wa Rukwa akitaka kuleta *information* kwa kutumia *fax* gharama yake ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii.

Awali ya yote, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, ambao walichaguliwa kushika nafasi mbalimbali. Pongezi za pekee zimwendee Mama yetu, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mfupi naomba nikimbie, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake ambayo ameitoa, hotuba ni nzuri, imeandaliwa kwa makini, kwa uangalifu, kwa umahiri na ufundi wa hali ya juu sana. Hii yote inaonyesha upeo alionao katika uongozi wake. Nampongeza sana pamoja na wataalam wake na wale wote ambao walishiriki katika kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki. Mahali popote pale duniani uchaguzi unapofanyika huwa unatimiza maagizo ya Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, ukisoma

katika Biblia, Kitabu cha Methali, Sura ya 16:33 inasema hivi: “Kura hupigwa kujua yatakayotokea lakini uamuzi ni wake Mwenyezi Mungu”. Vile vile ukisoma Sura ya 18:18 unasema: “Kura hukomesha ubishi, huamua kati ya wakuu wanaopingana”.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Danhi Makanga, umepatikana kwa kupitia mistari hii ambayo nimeisoma hapa, hakuna kitu kingine ambacho wewe unapaswa kujivunia, unapaswa kujivunia kwamba, Mwenyezi Mungu amekuruhusu kuingia humu, fanya kazi yako ipasavyo, watumikie watu kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hotuba hii ni nzuri na ya pekee na Wabunge tumekuja hapa kueleza matatizo yanayowasibu wananchi wetu, inabidi niseme yafuatayo: Nitajielekeza sana katika suala la ujenzi wa barabara vijijini na napenda niigusie TAMISEMI. Kwa kweli hakuna utaratibu mzuri wa kutengeneza barabara za vijijini. Katika Jimbo langu tangu utaratibu wa kujenga barabara za vijijini uwepo, nina barabara ambazo zina kilomita zipatazo 198 kati ya hizo zilizokwishatengenezwa ni kilomita 21 tu.

Kwa mfano, barabara ambayo ni muhimu na ya pekee inayotakiwa kujengwa haraka iwezekanavyo ili kuwaokoa watu wanaoishi huko ni barabara yenye kilomita 34.5 ya kutoka Kabindi - Nyamigogo - Kasozibakaya - Mkungo. Unapopita pale kwa kweli unashangaa kama kweli kuna utaratibu wa kutengeneza barabara kwa nini wasifanye uchambuzi na kuwa na utaratibu maalum wa kujenga barabara hizi? Hiyo ni barabara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya pili ni ya Nyantakara - Namavota ina kilomita 20 na ni muhimu sana. Barabara nyingine ni ya Katoke - Chantamwete ina kilomita 5. Barabara hiyo ina historia ya pekee.

Mheshimiwa Spika, nazitaja barabara hizi ili kuonyesha umuhimu wake. Baada ya kuzitaja, nitaiomba Kamati ya Miundombinu ije itembelee Wilaya ya Biharamulo na kuangalia kwa nini hizi barabara hazijajengwa tangu tunaanza utaratibu wa kujenga barabara hizi. Je, hivi Wilaya ya Biharamulo kwa nini haina utaratibu wowote ule ambao unaeleweka wa kujenga barabara hizi matokeo wananchi hawaelewi kinachoendelea? Nazitaja barabara hizi ili Kamati ya Miundombinu kabla hatujamaliza kikao hiki ihakikishe inapanga utaratibu wa kuja kutembelea Wilaya yangu vinginevyo mambo mengine yatatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ni Biharamulo - Kiruruma yenye kilomita tano, barabara nyingine ni Biharamulo - Chankende - Rugondo yenye kilomita 22. Barabara nyingine ni ya kutoka Nyabusozi - Nemba - Nyampakala yenye kilomita 43 na barabara nyingine ya umuhimu yenye historia ni ya Nyarubungo - Katoke - Kasuno yenye urefu wa kilomita tisa na ya kumalizia kabisa ni barabara ya kilomita 22 ya Lunazi - Kisuma na Katahoka. Hizi barabara zote zina umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda hautoshi, naomba niishie hapo. Ningeweza kuelezea kwa nini nimezitaja na nimezichambua na hii *fax* nimeipata jana maana yake majibu ya mara kwa mara yanayotolewa na Serikali yanasema hivi ni vipaumbele vya Halmashauri. Mimi ni Mbunge tangu 1995, mimi nakaa Jimboni kwangu, sitaki kusikia majibu ya kusema kwamba nikawasiliane na Halmashauri, nimeshawasiliana na ndiyo maana nimepata hii *fax* na nimepata jana kutoka kwa Mhandisi wa Wilaya.

Kwa hiyo, majibu ni kwamba, Kamati ya Miundombinu iende kutembelea halafu kuwepo na mpango mahsusi wa kuzitengeneza hizi barabara. Hayo ndiyo maombi niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda nikizungumzie ni kuhusu ndugu zetu Wapinzani ambao hawatambui Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya nini na imeshafanya kitu gani. Kuna mtaalam anasema: *"One of the most dangerous forms of human error is forgetting what one is trying to achieve." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshafanya kila linalowezekana kuhakikisha inawaondolea adha na matatizo wananchi wa Tanzania na mtu yeyote ambaye anajidai kwamba anaweza kuja kufanya zaidi ya hapa kwa kweli ni mtu ambaye wanasema ni mtu mwenye tabia ya maneno mengi, ambaye anatimiza ule msemo unaosema *"words without ideas are like sails without wing."* Sasa wewe unasema tu lakini ukiingia ni sawasawa na wacheza mpira, kama wewe ni shabiki unaweza kustukia hata umeshampiga mwenzako lakini ukiingia uwanjani hata mpira utakuwa unakupita pembeni. Kwa hiyo, ndugu zangu Wapinzani mnapaswa kuangalia na kuthamini na kutambua kazi ambayo imeshafanywa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu vyombo vya habari. Vyombo vya habari vinafanya kazi zake vizuri, vinatimiza wajibu na walio wengi wana taaluma safi na nawapongeza sana tena sana kwa namna wanavyowaelimisha watu. Lakini tupo katika safari ya kuelekea katika Uchaguzi Mkuu, nawaomba sana tena sana msije kutumiwa na baadhi ya watu ambao watakuwa wanajivisha ngozi ya kondoo kumbe ni chui katika kutafuta uongozi, watawatumia kwa namna yoyote ile kuchafua sifa za watu ambao wanastahili kuwa viongozi. Mtaalam mmoja anasema ninyi pamoja na kusoma, taaluma mliyonayo na elimu mliyonayo wanasema kwamba, naomba ninukuu msemo wa Mhenga mmoja aliyesema hivi: *"Sleeps and snores in libraries but wisdom is everywhere, wide awake learning on tiptoe".*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu Waandishi wa Habari, tumieni hekima na busara katika kutupokea sisi, maana yake sasa hivi kila mmoja anazunguka awe wa kutafuta Urais au Ubunge anazunguka, atatumia Waandishi wa Habari kwa namna yoyote kumchafulia mwingine. Tumieni hekima na busara, msije mkatumia haya yote mliyojifunza katika kuwachafulia watu wengine. Tunataka watakaochaguliwa wawe ni viongozi wa umma. Wawe ni viongozi wa wote, wasiwe ni viongozi wa kuwagawa watu kwenye makundi kwa sababu hela inaweza kutumika katika kuhakikisha anapatikana kiongozi asiyefaa na matokeo tutagawanyika kutokana na

kalamu ya Mwandishi wa Habari. Kwa hiyo, nawaomba Waandishi wa Habari, tumieni kila liwezekanalo katika uzoefu wenu kuhakikisha kwa kweli mnaandika yale yanayostahili kuandika ili msipotoshe umma kwa ajili ya kuchagua watu wasiostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu wakimbizi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake ameligusia. Suala la wakimbizi bado ni tatizo na kwa kweli nasikitika kwa namna ya pekee kwamba, Bara la Afrika bado ni kiwanda cha kutengeneza wakimbizi na hicho kiwanda kinaendelea kutengeneza wakimbizi hapa na pale. Nawaomba tufanye kila liwezekanalo kuhakikisha hiki kiwanda kinaharibiwa na hii yote ni kutokana na kutokuheshimiana katika mipaka ya kila nchi. Angalia *DRC* na Rwanda sasa hivi wanaanza kupingana bila sababu. Kwa hiyo, naomba kwa namna ya pekee hili suala la wakimbizi litafutiwe ufumbuzi wa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika Kata ya Nyakahura wakimbizi wote ambao wamekuwa wakitoroka kwenye makambi wanajificha kule, matokeo wameshawaingilia wananchi pamoja na kuwanyang'anya kila aina ya mali waliyonayo. Wananchi wa Nyakahura sasa wamekuwa wakimbizi katika nchi yao, sasa hivi hawaishi tena kwenye nyumba zao na nimeshamjulisha Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba, aje mwenyewe *physically,* ahakikishe hilo tatizo tulilonalo ili tuweze kulitafutia ufumbuzi kama ni kuwapatia ulinzi wa kutosha wapatiwe ulinzi wa kutosha. Wananchi hawa wa Nyakahura hawana uwezo wa kujifanyia kazi za kujitolea, hawana uwezo wa kujifanyia kazi za kujitegemea, matokeo sasa wamekuwa ni watu wenye shida, adha na dhiki ya hali ya juu. Ukifika pale kama unakwenda Ngara na wao vile vile wamejipanga barabarani na wanakaa kwenye nyumba kama za mahema, utafikiri ni wakimbizi na ukifika pale salamu unayoipata kwa kweli ni vilio. Kwa hiyo, naomba hili suala la wakimbizi kwa namna ya pekee kabisa lishughulikiwe vinginevyo ndugu zangu wananchi wale wa Nyakahura wataendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu walimu. Kwa kweli tumelisemea sana, mimi naomba hii Kamati ya Huduma za Jamii ambayo imeundwa, ihakikishe inafuatilia kwa karibu sana kuhusu malipo ya ndugu zetu walimu. Walimu wanaishi katika mazingira magumu na kutokana na mishahara midogo waliyonayo halafu uendelee kumnyima stahili yake, haki yake, kwa kweli ni kumkosea haki.

Kwa hiyo, kinachotakiwa hii Kamati ambayo ni ya huduma za jamii, ifuatilie na itupatie jibu, tunataka tujue hatima ya malipo ya walimu. Mimi sielewi kwa nini ucheleweshaji huu unafanyika wakati inajulikana kwamba, mwalimu anaishi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Nimesimama ili niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake wote, kwa hotuba nzuri, imetueleza ahadi zilizotolewa katika bajeti iliyopita na utekelezaji na mambo mengi mazuri tumeyasikia na nina imani Mheshimiwa Waziri Mkuu, angepewa zaidi ya saa mbili alipozungumza hapa jana, kuna mengi ambayo ameyaacha ambayo tungeweza kuyasikiliza. Ningependa niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inashangaza kwamba, kuna wengine wanaibeza hii hotuba, mimi ninachoweza kusema ni kwamba, wangejicheki labda wamekaa kiti cha nyuma, watakapokwenda kiti cha mbele wataona kwamba hii ni hotuba ambayo inastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wabunge wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa wenzetu waliofiwa na wapendwa wao na vile vile kwa Wabunge wenzetu waliopata shida wakati wanakuja Bungeni kwenye kazi waliyotumwa na wananchi, waliopata ajali nawapa pole nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie suala la ugawaji wa Majimbo ya Uchaguzi. Tume inayohusika ipo moja kwa moja chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nilitaka nitoe mchango katika hotuba hii. Kabla ya uhuru nchi ya Tanganyika ilikuwa na Majimbo manane. Miaka miwili iliyopita Mkoa wa Arusha uligawanywa ukazaa Mikoa miwili ya Arusha na Manyara. Mkoa utakaofuata katika zoezi la kugawa Mikoa itakuwa ni Mbeya kwa sababu ndiyo Mkoa unaofuata kwa ukubwa. Lakini sababu ya kugawa haya Majimbo ni kwamba, viongozi waweze kusimamia mipango ya maendeleo kwa urahisi zaidi. Kazi ya viongozi, tukiwemo sisi Wabunge, ni kusukuma gurudumu la maendeleo, tunategemewa kuhamasisha, kubuni, kuelekeza, kusimamia na kuongoza shughuli nzima za maendeleo katika maeneo yetu. Maeneo tunayoyaongoza na kuyawakilisha yanatofautiana kwa ukubwa na idadi ya watu. Kwa hiyo, unaweza kuwa na uongozi ambao safu yake ni nzuri, mahiri, wana uelewa na pia wanajituma lakini kutokana na ukubwa wa maeneo wanayoyasimamia na watu ambao wanahitaji huduma zao utakuta nguvu zao zinadundulizwa hapa na pale na *impact* haitaonekana.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano wa Jimbo la Rungwe Magharibi ambalo lina Kata 19, Vijiji 112, Vitongoji 700 na kwa mujibu wa sensa ya idadi ya watu ya mwaka 2002 wakazi wa Jimbo hilo ni 220,000. Waliowahi kufika katika Jimbo hilo watakubaliana na mimi kwamba, jiografia ya Rungwe Magharibi ni ngumu, kuna milima mingi na mabonde. Kijiji jirani kinaweza kikawa ng'ambo ya pili lakini kufika pale ni lazima uende kilomita saba na saba nyingine kuweza kukifikia. Hakuna madaraja, hatuna barabara nzuri, mahitaji yetu sasa hivi ni madaraja 72. Nitoe mfano wa huduma nyingine zinazomhitaji Mbunge, tunasimamia shule za msingi 132 na kila Kata inajenga sekondari na kwa taarifa tu mwaka huu tumefungua shule za sekondari saba. Sasa yote haya yanataka usimamizi wa Mbunge. Halmashauri ilitafakari matatizo yote haya na ikaamua hilo Jimbo ligawanywe na taratibu zikafanywa mpaka ikafika kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Lakini kauli zimekuwa zikitolewa na viongozi wa ngazi ya juu kwamba, hilo zoezi la kugawa Majimbo limesitishwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 Majimbo mapya yaliundwa na nakumbuka kuna mengine yaliunganishwa na hii ni kwa mujibu wa sheria. Watu wengi tulitegemea kwamba, mwaka 2005 ambayo ni miaka kumi baadaye, hili zoezi lingefanyika tena na kwa vile halitafanyika kutokana na kauli zilizotolewa sielewi kama huo ni uvunjaji wa sheria au uvunjaji wa Katiba. Sababu hazijatolewa kama ni sababu za kifedha, lakini nilitaka niliseme hili kwa sababu najua kwamba, mimi nimelalamikia Jimbo ambalo nalifahamu sana lakini kuna Wajumbe wengine ambao pia wangepata nafasi wangelizungumzia hili. Ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu itupe jibu kwa sababu wananchi hawajaambiwa lolote, nimesoma hiki Kitabu cha Hotuba kwenye shughuli za uchaguzi halijagusiwa, ningependa itolewe kauli ili watu tujue tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na suala la Majimbo vile vile kumekuwa na kauli zinazosema kwamba, mwaka 2005 tutakuwa na Wabunge wengi zaidi. Sasa hivi tupo 295 lakini wakati wa uchaguzi mwaka 2005 tunataka kujaza viti 350. Nilikuwa naangalia kazi za Wabunge, mojawapo ni kwamba, tunakuja hapa Bungeni kupitisha na kutunga sheria na kuishauri Serikali katika mambo mbalimbali. Hizi sheria tunazozitunga zinawalenga wananchi, nia yetu ni kusukuma gurudumu la maendeleo ili kuboresha maisha ya wananchi. Kwa hiyo, kutunga sheria ni kitu kimoja lakini ni lazima sisi wenyewe twende huko ambako kuna wananchi tuweze kuzisimamia. Sasa tunapozungumzia uwiano inakuwa kama nia yetu ni kuongeza idadi ya Wabunge ili waje hapa Bungeni kwa ajili ya mijadala. Je, tatizo letu kweli ni mijadala hapa Bungeni? Nimeona kwamba kuna Wabunge wengi ama kwa kutaka wenyewe hawajawahi kuchangia hapa Bungeni, lakini wengine pia wanaweza kutaka kuchangia kutokana na nafasi ilivyo ndogo hawapati nafasi ya kuchangia. Kwa hiyo, Wabunge tuna jukumu la kuhudhuria hivi vikao lakini tukitoka hapa tunakwenda Majimboni ili yale tuliyopitisha hapa tuweze kuyasimamia. Kwa hiyo, nina imani kwamba Jimbo ambalo ni kubwa likigawanywa ina maana huduma zinazohitajika za Mbunge zitapungua kwa maana kwamba, watu watakuwa wachache zaidi na *impact* itakuwa kubwa zaidi kwa wale ambao ni walengwa wetu. Hivi Serikali imewahi kufikiria kwamba Majimbo yakiongezwa hata hawa watu ambao tungependa waingie hapa Bungeni nao watapata fursa zaidi kwenda kugombea haya Majimbo mapya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafikiria kwamba, mwaka 2005, *Inshallah* Chama changu kitaniteua kugombea tena katika Jimbo langu. Lakini vile vile kama ilivyokuwa mwaka 2000 nilikuwa na Wapinzani wanne. Sasa naweza mimi kushinda, lakini hawa wenzangu wa kutoka Upinzani wao wakapita kwa huu mkondo wa uwiano na wenyewe wakaja hapa Bungeni. Sasa wao watarudi Jimboni kifua mbele na kuwaambia wapiga kura walionichagua kwamba, ninyi mlininyima kura sasa mmefanya nini na mimi ni Mbunge pia. Kwa hiyo, hili nalo ni suala ambalo nilitaka nililete hapo mbele ingawa halijaletwa rasmi lakini kwenye kitabu halipo na nimeona kwamba, muda unakwenda na mwaka 2005 ndiyo ilikuwa tujue kama haya Majimbo yanagawanywa au vipi na kulikuwa na maswali mengi kama huo Muswada utaletwa hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishie hapo na kama nilivyosema awali naiunga hoja hii mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMIS J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu siku ya leo. Lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mzazi wao. Mwenyezi Mungu, ailaze mahali pema roho ya marehemu. Naomba pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Parmukh Hoogan Singh, kwa kufiwa na binti yake na Mungu ailaze mahali pema roho ya binti huyo. Naomba pia niwape pole wale wote waliopata ajali wakati wakija hapa Bungeni ili kuja kuungana nasi na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, aliyevamiwa na majambazi, pia nampa pole sana.

Mwisho, naomba nimpe hongera Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi aliotuletea. Hii ni heshima kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba sasa nijielekeze katika hotuba hii katika kuchangia. Kwanza, naomba kabisa kwa heshima na taadhima, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na usimamizi mzuri wa Serikali yetu kwa muda wa mwaka huu tangu tulipompa makadirio ya mwaka 2003/2004. Tumeshuhudia mengi yaliyofanywa na Serikali hii katika usimamizi wake pamoja na Mawaziri wake katika ofisi yake, watumishi wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, wanastahili pongezi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa maana hiyo, naomba basi bila kuchelea niunge mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo la kwangu la kwanza ambalo nataka nichangie katika hotuba hii ni ukame na upungufu wa chakula na hasa tatizo lililotupata mwaka 2003 na mapema mwaka huu ambalo kwa kweli bado hatujasahau. Njaa na vyote vinavyofanana na hilo havina heshima. Njaa kwa kweli haina heshima. Inaweza kukudhalilisha kwa kila hali. Kwa hiyo, njaa iliyotutokea mwaka 2003 na mwaka huu wa 2004, ilikuwa ni hali moja ngumu, lakini naipa hongera Serikali kwa namna ilivyolishughulikia suala hili la njaa. Hali ilikuwa ngumu tulikuwa tunafikiria kwamba ni upungufu wa kawaida wa chakula lakini baadaye jinsi hali ilivyokuwa inakwenda na hasa mvua ilipochelewa hali ikabadilika na kuwa njaa kali ambayo kwa kweli ilifadhaisha watu wetu wengi sana lakini kwa mipango ya Serikali ya kuwaandaa wafanyabiashara kwa ajili ya kununua chakula ambacho kiliwafikia wananchi na mipango ya Serikali kwa ajili ya kupeleka chakula kupitia kitengo chake cha *SGR* ambacho kiliweza kupunguza makali ya njaa katika Vijiji vyetu, kwa kweli viliweza kusaidia na kufanya hali angalau ionekane kwamba ni afadhali.

Mheshimiwa Spika, lakini wafanyabiashara mimi nashauri kwamba, katika mchango huu hawakuweza kuchangia kwa haraka na ndiyo maana kwa kipindi kirefu baada ya kutokuchangia na kutofikisha chakula hiki maana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo walitueleza hapa kwamba, wafanyabiashara watashauriwa au kuwezeshwa ili waweze kununua chakula na hatimaye kukipeleka kwa wananchi waweze kununua na walikuwa wamesamehewa kodi ambazo zinaambatana na ununuzi wa hicho chakula ili chakula kiwe rahisi. Lakini chakula hicho hakikufika mapema kwa wananchi mpaka hali ya chakula ikapanda kiasi ambacho ikawa ni hali

ngumu sana. Hii inawezekana ni tabia ya wafanyabiashara, maana mfanyabiashara tabia yake ni kutaka faida kubwa pamoja na kwamba amesamehewa kodi lakini alitaka kwanza a-*create vacuum* ili baadaye akija kupeleka chakula basi kiwe na bei kubwa. Bei zilipanda mpaka kiasi cha kufikia debe moja shilingi elfu tano au elfu sita, hiyo ilikuwa ni hatari wakati mtu ambaye alikuwa na njaa na hakuwa na uwezo wa kununua chakula, sasa bei ikawa imefikia hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa shukrani za pekee kwani nilifika katika ofisi yake baada ya Jimbo langu la Singida Mjini kuwa halikupata chakula cha msaada, kile chakula cha bei nafuu cha shilingi hamsini, tuliambiwa sisi tupo Mjini na kwa hiyo, Mjini tungetengewa au kupatiwa chakula cha kununua tu sokoni. Lakini nafikiri walisahau, ofisi ilisahau kwamba katika Jimbo langu kuna Vijiji kumi na tisa ambavyo ni Vijiji kama Vijiji vingine vya kawaida vya Singida Vijijini na kwa hiyo, vile Vijiji navyo vikaambiwa vipo Mjini haviwezi kupata chakula. Lakini hali ilivyokuwa inaendelea kuwa mbaya niliondoka kwenda ofisini kwa Waziri Mkuu, ilikuwa niende kwa Waziri wake anayeshughulika na maafa, kwa bahati mbaya hakuwepo, alikuwa amekwenda Kenya kutafuta chakula, lakini kwa bahati nzuri nikamkuta Waziri Mkuu ambaye nashukuru sana kwa kunipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipomweleza juu ya tatizo hili na wakati ule kweli nilikuwa nimeacha mahindi Mjini Singida yalikuwa yanauzwa shilingi elfu tano mpaka sita kwa debe. Nilipomweleza hakusita na hapo hapo akainua simu na kumwagiza Katibu Mkuu wa Kilimo aweze kupata mahindi na kupeleka Singida Mjini kwanza ya kununua na baadaye kufuatiwa na mahindi ya msaada. Namshukuru sana maana baada ya muda mahindi hayo yalikwenda na mahindi pia ya msaada tuliweza kupata, kwa hiyo, namshukuru sana kwa kitendo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, njaa ni vita na kwa hiyo haitakiwi kuwa na urasimu mkubwa. Yeye hakuwa na urasimu wowote, nilipofika ofisini kwake, kwa kweli alinitekelezea yale yote. Lakini ndugu zangu haya yote yametufunza, mwaka huu tunasema kwamba, tumevuna lakini bado tuna njaa. Hali ya hewa bado si nzuri, wananchi wetu walianza kula wakati bado kipo mashambani na kwa hiyo tutakuwa na upungufu wa chakula si muda mrefu. Nashukuru kwamba, Serikali inatathmini hali hiyo sasa hivi lakini ningeomba basi yaangaliwe mapungufu yaliyojitokeza wakati uliopita kwa wafanyabiashara watakaopewa idhini ya kununua chakula na kukileta pamoja na Serikali yenyewe iangalie mipango yake ili lisije kutokea tatizo lililojitokeza tena.

Matatizo haya yote yanajitokeza kwa nini? Yanajitokeza kwa sababu kilimo chetu bado siyo endelevu. Kilimo chetu bado tunawategemea hawa ambao siku zote tunajivunia asilimia 80 ya wakulima, hivi tuendelee kujivunia kwamba tuna asilimia 80 ya wakulima ambao wanategemea mvua na pindi mvua ikitetereka tunajikuta tuna njaa? Mimi nafikiri tusiendelee kujivunia asilimia 80 ya wakulima, kwanza bado sasa hivi wanaendelea kupungua siyo asilimia 80 kwa sababu vijana sasa hivi hawataki kufanya kazi ya kilimo, wanaobakia ni wazee na akina mama, kwa hiyo, asilimia hii 80 inapungua. Naishukuru Serikali kwa kuja na mpango wa sasa hivi wa kusaidia wakulima

wa kati na wakulima wakubwa ambao watatuwezesha kutukwamua katika matatizo haya ya chakula. Naomba tulivalie njuga hili. Kama Serikali muda wote ilikuwa hailioni hili kwamba ni tatizo na tutajikwamua vipi katika tatizo la chakula, sasa ilione hili na kuweza kusaidia mapema.

Mheshimiwa Spika, kilimo kwa kweli bado hakifurahishi na bado pamoja na misemo yote ya kukienzi kilimo lakini bado hakijaonyesha *impact* tunayotaka ionyeshwe na kilimo. Yapo maeneo mengine ambayo sasa hivi tumeanza kuona mambo ambayo yamefanywa, kwa mfano, maeneo ya maji, elimu na barabara, tunaona hali halisi ambayo inafanywa, hivi tunashindwa nini kuonyesha hali halisi pia katika kilimo ili kiweze kuonekana hasa na tunaona kabisa ni uti wa mgongo wa uchumi wetu? Punde tunapotetereka katika kilimo tunajikuta tunapata matatizo, uchumi unashuka, vitu vyote vinakwenda ovyo. Sasa kwa nini tunashindwa kuzingatia kukienzi kilimo ili tuweze kuona kwamba tunafanikiwa?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi biashara hizi ndogo ndogo na biashara za kati, zimepewa motisha na kuweza kuwafanya watu washiriki katika biashara na wazalishe ili biashara iende juu. Sasa ningetegemea pia katika kilimo pamoja na kwamba hao wakulima wadogo wadogo ambao bado wanaendelea kutulisha sasa hivi tunawaona wanapata tabu lakini pia pamoja na kuwasaidia hao wa kati na wakubwa, basi tuwasaidie na hao wengine wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba pia nichangie kidogo kwenye elimu. Naipongeza Serikali pia kwa kuja na Mpango wa Kuboresha Elimu ya Sekondari, ambapo inahitaji kuzijenga shule za sekondari ili kujikwamua katika tatizo hili.

Lakini ningeomba kama azma ya Serikali inavyosema kwamba, ipendelee Mikoa ile ambayo haina shule za sekondari nyingi, hivi Mkoa kama wa Singida shule za sekondari za Serikali ni mbili tu, unategemea kweli na sisi tuonekane huko juu kama wasomi? Shule mbili za sekondari tangu tupate uhuru, halafu shule za wananchi ambazo wamejitahidi kuzijenga pia sijui tunazo tatu au sijui ngapi. Sasa kwa makusudi kabisa naiomba Serikali iangalie maeneo kama hayo. Yawezekana ni kwa sababu ya uchumi wetu ndiyo labda pengine tukawa na hali kama hii, sasa Serikali hebu iangalie pamoja na kwamba lazima kwanza wananchi wafanye juhudi ya kujitolea halafu baadaye ndiyo wapate hali hii lakini inawezekana kwamba tusiwe na uwezo wa mara moja wa haraka wa kuweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sasa Serikali kama imeamua basi ituone pamoja na uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii kama ulivyoipangia shughuli zake inasimamia Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Afya, Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, lakini yote haya katika Wizara zote hizi mambo ni mazuri, yanatupeleka vizuri, tunazisifu sana Wizara hizo zote tatu. Lakini moja linalotukwaza na ambalo limezungumziwa sana hapa katika Bunge lako ni suala la walimu. Hivi katika maboresho yote haya tunayoyafanya ya Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari, tunategemea kuyafanya maboresho yote, lakini mwalimu tunategemea kuendelea kumwacha hivyo hivi tunategemea kweli tutajikwamua katika elimu? Unaendelea

kumwacha mwalimu na mshahara wake huo lakini pamoja na kuendelea kumwacha na mshahara wake huo alikuwa hajalalamika, sasa unamwacha kumtimizia yale mengine ambayo unamtuma afanye, unamhamisha humpi fedha za uhamisho na marupurupu yake na anakwenda likizo humpi nauli yake. Sasa unafanya haya yote halafu unamtegemea akutolee kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika katika hili tunaiomba Serikali hebu iwalipe walimu stahili zao wanazostahili. Sisi hatutaki vile vya nyongeza vya namna gani kile wanachostahili. Katika Kamati yetu tumeunda Kamati Ndogo na kwa kweli tunataka tujigawe tu hata katika ile Kamati tushughulikie Mikoa yote tuone, maana tumeona pale kuna matatizo tunayoambiwa. Zipo *Pay Roll* ambazo zinatayarishwa mbili mbili, *Pay Roll* nyingine ya kutafutia fedha na *Pay Roll* nyingine ya kwenda kulipa, ya kutafutia fedha ndiyo *Pay Roll* yenye fedha nyingi, yenye kusema kwamba wanakwenda kulipwa pamoja na marupurupu yao, lakini kumbe yale marupurupu yanaingia kwa wale wanaojijua wenyewe. Sasa tunataka tuone hayo. Tunaiomba Serikali itusaidie hii Kamati ya Huduma za Jamii ili tuweze kufikia azma hiyo tunaisaidia Serikali siyo kwamba tunakwenda kufanya nini, tunaisaidia Serikali ili kufahamu mambo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia hayo, bado na Wizara zingine nazo zipo nimesema tunasimamia Wizara tatu, lakini ipo Wizara ya Afya pia yenyewe haina tatizo kama hilo nililolizungumza hapa, lakini yenyewe ina tatizo bado la upandishaji wa vyeo hasa wale manesi pamoja na mishahara yao unaweza ukakuta amepandishwa cheo, lakini haoni mshahara wake kupanda miaka mitatu au unaweza kumkuta mwingine aliyeajiriwa juzi anashughulikiwa vizuri zaidi kuliko yule aliyeajiriwa miaka mingi iliyopita anakuja anapitwa mshahara na huyu aliyeajiriwa juzi sasa tunafanya nini? Hebu Wizara ya Afya nayo iende na wakati iangalie ili iweze kuona watumishi wote hawa wanakwenda sambamba kila mmoja anpata stahili yake anavyoweza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo ambayo nilikuwa na kiu ya kuyazungumza, naomba tena niishukuru Serikali na nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri na kwa usimamizi mzuri wa Serikali yake ambao umetufikisha hapa katika utekelezaji mzuri wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli naomba niunge tena mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia katika mjadala huu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema chochote, nataka nikiri kwamba, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kipindi chote umekuwa unaliongoza hili Bunge vizuri. Nataka nikuambie ukweli kwamba, kila unavyokomaa kuendelea kuliongoza Bunge ndivyo linavyoendelea kukuhitaji. Waswahili wanasema: "Mwenyezi Mungu hakupi mzigo akakunyima kata." Kiswahili kikubwa kidogo. Maana ule mzigo pamoja

na kata vyote vinakuwa mzigo juu yako, lakini ile kata inakusaidia kidogo lakini hawezi kukupa mzigo akakunyima busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mabunge mengine duniani Wabunge wanapigana, Wabunge wana kauli za kutisha na Wabunge hawaelewani, lakini katika Bunge la Tanzania hali ni shwari na sababu ni wewe Mheshimiwa Spika. Mwenyezi Mungu, amekupa mwili mkubwa na urefu lakini ni tofauti kabisa wewe na tabia yako. Mlango wako katika ofisi umeuacha wazi, Mbunge wakati wowote anaweza kukuona akakueleza analolitaka na hapa Bungeni umetupa demokrasia nzuri, tunajieleza vizuri na unatupa maelekezo mazuri. Naomba nikuombee kwa Mwenyezi Mungu na sote tukuombee uendelee na busara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na mimi nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamechangia na waliompongeza kwa dhati Mheshimiwa Danhi Makanga. Kule katika mapambano Mheshimiwa Danhi Makanga alipewa jina la Simba wa Vita. Kusema kweli Mheshimiwa Danhi Makanga, alikuwa ni biashara inayojiuza yenyewe, yeye mwenyewe alikuwa *Candidate* mzuri lakini pia na Chama alichokuwa nacho kilikuwa kizuri. Namtakia kila la kheri na fanaka katika ushindi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtoa hoja. Mimi nilisikiliza kwa makini sana hoja yake na nimebahatika kusikiliza hoja za Mawaziri Wakuu katika miaka 18 ndani ya Bunge hili. Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu , ilijieleza vizuri na imewasaidia sana Watanzania. *(Makofi)*

Waziri Mkuu, tuliyekuwa naye ni Waziri Mkuu aliyevunja rekodi ya kukaa katika Bunge hili kwa mfululizo kwa miaka minane. Sidhani kama kuna Mbunge humu ndani ya Bunge anayekataa kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu huyu hana nidhamu, ni Waziri Mkuu mwenye nidhamu na msikivu kwa Waheshimiwa Wabunge, wakati wote Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa mwadilifu, anawasikiliza Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya wananchi na bila shaka anawasikiliza wananchi, namtakia afya njema na kazi nzuri. Ofisi ya Waziri Mkuu ina Mawaziri wawili na wao pia wanafanya kazi nzuri, Katibu Mkuu na watumishi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nijielekeze katika suala zima la Vyama vya Siasa. Tangu kuasisiwa mambo ya Vyama Vingi vya Siasa sasa tunakaribia au tuko katika miaka karibu kumi na tuna Vyama vya Siasa vingi nadhani ni zaidi ya 13 lakini Vyama hivi vya Siasa kama hatutaangalia vingine vitakufa *automatically* na sasa Watanzania wengi wameanza kuvipuuza hivi Vyama na siyo lengo la Serikali wala lengo la sisi viongozi, sisi tunapenda viwepo Vyama Vingi vya Siasa lakini Vyama vyenye uwezo wa mambo ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza hivi sasa Tanzania viko Vyama ambavyo vinaashiria kuvunjika kwa amani. Sheria ya Vyama vya Siasa imenyamaza kimya, kuna Vyama vya Siasa vinaandaa majeshi, kuna Vyama vya Siasa vina kauli za kumwaga damu, nataka niulize tu kwamba Serikali inachukua hatua gani? Hatuwezi tukaendelea hata siku moja na Vyama vya Siasa vya namna hiyo na kama hatuwezi

tukaendelea na Vyama vya Siasa vya namna hiyo, Serikali imefanya utafiti kwa kiasi gani, maana katika kipindi cha mpito tumewavumilia kwa kiasi cha kutosha. Sijui tutamwaga damu, Vyama vinaandaa mabomu, Vyama vinamwaga tindikali kwa watu, hayo tumeyavumilia kwa kiasi cha kutosha cha miaka kumi, sasa hivi tunahitaji Vyama vya Siasa vyenye uwezo wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Vyama vya Siasa pengine vinaashiria kuvunja Muungano kwa makusudi. Sasa nilikuwa naomba kwamba, Serikali ni vizuri ifanye utafiti wa kutosha na imsaidie Msajili wa Vyama vya Siasa kwa sababu Msajili na yeye kwa upande mwingine meno hana hata yanapotokezea haya mambo anasema tu, lakini sheria pengine iko kimya hata akisema akifukuze Chama au akifute pengine bado kitabakia kina mamlaka kitakwenda Mahakamani kiendelee. Sasa nilikuwa naiomba Serikali ifanye utafiti wa kutosha na utafiti ambao utalisaidia Taifa kuliweka katika hali ya amani na utulivu, utafiti ambao utasaidia kuendeleza Muungano tuliokuwa nao na utafiti ambao utaendeleza Vyama hivi vya Kisiasa viwe bora. Nimeyasema haya kwa sababu nina wasiwasi kwamba, Vyama vingine vitajifuta vyenyewe kwa sababu vitapuuzwa na vitakuwa havina watu.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nizungumzie suala la *Radio Tanzania* na TVT. Nataka nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana watumishi wa *Radio Tanzania* na TVT. Kwa kweli kazi wanayoifanya watumishi wa *Radio Tanzania* ni nzuri na ndiyo chombo pekee ambacho kinasikika karibu katika sehemu kubwa ya nchi yetu, vyombo vingine pengine havisikiki, lakini unapokwenda *Radio Tanzania* pale ukiwaona watumishi wake walivyo na maslahi wanayopata, unawaona unyonge wao. Watumishi wa *Radio Tanzania* wanafanyakazi karibu usiku kucha, saa 24, na wanatoa habari katika nchi nzima na wanashindana na vyombo vingine binafsi na taaluma zao na za watumishi wa vyombo binafsi ziko sawa, lakini cha kushangaza na kusikitisha ni kwamba, wale watumishi ambao wanafanya kazi katika vyombo binafsi wana mishahara mizuri, wana marupurupuru mazuri na wanapata mikopo mizuri. Sasa nilikuwa naiomba Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano, chombo kinachohusika kuanzia sasa waangalie maslahi ya Watumishi ya *Radio Tanzania* na TVT. Waangalie uwezekano wa kuwakopesha vyombo vya usafiri watumish wa *Radio Tanzania* na TVT, waangalie uwezekano wa kuwapatia nyenzo za kufanyia kazi na waangalie uwezekano wa kuwapatia motisha. Naliomba hili liangaliwe kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu sikuona uwezekano mzuri katika bajeti hii uliojieleza. *(Makofi)*

Jambo lingine ambalo nitalizungumzia linahusu Muungano hasa hali ya uchumi na hasa litahusu *Tariff* za *Custom* baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Sasa hivi *Tariff* za *Custom* ni moja na zinatumika Zanzibar na zinatumika Tanzania Bara. Wafanyabiashara wote ambao walikuwa wakishushia mizigo yao Zanzibar sasa hawaishushii tena mizigo yao Zanzibar wanaishushia Dar es Salaam. Kwa maana hiyo, hali ya uchumi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sasa hivi ni ngumu sana hata hiyo bajeti iliyopitishwa ya shilingi bilioni 50 kule Zanzibar imepitishwa tu, lakini hakuna kitu. Nataka niseme hawana fedha na hawatapata fedha kwa sababu wafanyabiashara wote hivi sasa wanateremshia mizigo yao ama Tanga au Dar es Salaam. Sasa nilikuwa naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar, itafute uwezekano wa makusudi wa kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala la kiuchumi ili Serikali ile ijiendeshe la sivyo hivi sasa wenzetu baadhi yao wanakaa karibu miezi mitatu hawajapata mishahara kule. Naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilitakalolizungumzia linahusu suala la kuwaka moto. Nimeshuhudia siku za nyuma kwamba, Benki Kuu ya Tanzania iliwaka moto, likafuata Jengo la *NASACO* nalo likawaka moto, ikafuata Wizara ya Mambo ya Ndani nayo ikawaka moto kuanzia ghorofa ya nne kwenda juu ikawaka moto, ikafuata Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Wizara ya Nishati na Madini ikawaka moto na juzi iliwaka moto Ikulu. Kote huko tunaambiwa ni hitilafu za umeme lakini na Makao Makuu ya JKT na yenyewe iliwaka moto, Ubungo kwenye mafuta kukawaka moto na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iliwaka moto. Sasa nataka nielezwe na Serikali hivi ni kuwaka moto kwa kawaida au kuna mkono wa mtu au ni hujuma. Kwa muda wa miaka kumi Serikali imenyamaza kimya na kila siku tunaambiwa hitilafu, hitilafu hizo ni za namna gani, ziko kwenye majengo ya Serikali tu ya watu binafsi hayapo. Naiomba Serikali ifanye uchunguzi wa kutosha na ichukue tahadhari za kila namna katika suala la moto. Kwa sababu tumechoka na hujuma ama mkono wa mtu upo.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kuna mihimili mitatu lakini Serikali imeikumbatia Bunge na Mahakama hawafurukuti. Nataka niseme kama kweli tunaheshimu Katiba na kama kweli tunataka kujenga Utawala Bora, tunataka Ofisi ya Bunge au Bunge lenyewe lipewe madaraka yake na uhuru wake na Mahakama ipewe madaraka yake. Bajeti ya Bunge inakuja leo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nadhani ndiyo maana Mheshimiwa Spika, anapeperusha bendera ya Serikali pale maana yake ni sehemu ya Serikali. Spika siyo sehemu ya Serikali, Spika ni Spika wa Bunge, anatakiwa apeperushe Bendera yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kuanzia sasa itenge asilimia maalum kwa ajili ya huduma za Bunge na Bunge lifanye makisio yake siyo Bunge liende likanyenyekee kwenye Serikali, wala siyo Mahakama iende ikanyenyekee kwenye Serikali. Majaji wanatazama Bunge kwa jicho la husuda kwa sababu hawana uhuru, chombo chao kimekumbatiwa na Serikali na Serikali imekuwa pale sijui niseme kitu gani. Naiomba sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hili jambo ilitatue haraka iwezekanavyo. Mabunge mengi duniani yanajitegemea, yanaandaa bajeti yake na wanawekewa *percentage* maalumu. Leo hii hivi tukipungukiwa fedha ndiyo Mheshimiwa Spika aende akamwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba ninahitaji fedha. Jaji Mkuu aende akamwambie Waziri wa Fedha, maana yake katika Mahakama za Tanzania tumepungukiwa na kompyuta. Ninaiomba Serikali hili liondolewe haraka iwezekanavyo. Nasikia kuna Utawala Bora, kuna Mheshimiwa Waziri kazi yake kusimamia Utawala Bora, anausimamia vipi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nataka nilinde muda, naomba kutamka kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na mzungumzaji aliyemaliza sasa hivi kwa sifa kemkem alizokumiminia wewe na Waziri Mkuu basi na mimi niseme kwamba wewe ni Spika *grade one* na yule ni Waziri Mkuu *grade one* kama zipo *grade* za namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pole kwa ndugu zetu ambao walipata misiba na mikasa mbalimbali. Vilevile nitoe pongezi kwa ndugu zetu ambao walichaguliwa katika nyadhifa mbalimbali za Kitaifa na za Kimataifa. Lakini kwa pekee kabisa nimpongeze ndugu yetu, rafiki yetu na mwenzetu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurejeea tena Bungeni. Ninatumaini yeye mwenyewe anatambua kwamba ile miaka saba aliyoitumia katika Upinzani, alipoteza muda mwingi mno sasa hivi angekuwa mbali.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri ambayo imeongezea kwa zile zilitolewa na Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ambazo tayari zimeshapitishwa. Kambi ya Upinzani waliona kigugumizi sana kuunga mkono Hotuba ya Bajeti au Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2004/2005. Lakini kama maneno haya hayataudhi mimi ningesema kwamba, ni unafiki kwa sababu najua kwamba Julai Mosi watakuwa mstari wa mbele kwenda dirishani kupokea posho. *(Makofi/Kicheko)*

Maendeleo ni mchakato kwa maana kwamba si kitu unachoweza kufanya basi ukamaliza ukasema nifanye maendeleo. Kwa kuwa unapotatua tatizo moja basi unaunda mengine. Hata barabara iwe nzuri namna gani inapotengenezwa basi baadaye itahitaji matengenezo baada ya kutumika na kuharibika hapa na pale. Vilevile majengo tunayojenga ya shule hata nyumba zetu sisi wenyewe basi tunapozijenga ni lazima ujue kwamba tutafanya matengenezo. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba maendeleo ni mchakato. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ndugu zetu wale ambao hawaoni kwamba Serikali imefanya kitu waelewe hivyo. Mambo mengi yamefanyika wote tunaona barabara, shule, hospitali na mambo mengi sana ambayo yameelezwa katika hotuba nzuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini mimi nilikuwa naomba nizungumzie Mikoa iliyo pembezoni au iliyo mbali na Makao Makuu ya nchi kwamba hii Mikoa na iliyo mingi yote ni Mikoa ile tunayoita Mikoa maskini na umaskini huo unasababishwa na mambo mbalimbali. Kwa sababu Mikoa hiyo haina miundombinu ambayo inaweza kuisaidia kuendelea, haina mawasiliano ya uhakika na haina umeme wa uhakika, kwa hiyo, utakuta kwamba mambo mengi yanakwama kwa sababu hizo. Kwa mfano, sasa hivi Sekta ya Mawasiliano imejitahidi kupeleka hata simu za mikononi katika maeneo hayo, lakini kwa sababu hakuna umeme si watu wengi wanaoweza kutumia simu hizo. Sasa simu hizo watazichaji wapi kwenye mkaa au kwenye kuni? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili suala linatakiwa kuangaliwa ili Mikoa hii iangaliwe iweze kupatiwa umeme wa uhakika na iweze kufanya maendeleo, waanzishe

viwanda vidogo vidogo na iweze kufanya mambo mengine mbalimbali yanayotegemea umeme.

Mheshimiwa Spika, bei za bidhaa katika Mikoa hii ni ghali sana na tunasema kwamba, umaskini una vigezo mbalimbali, lakini kigezo kimojawapo ni nyumba bora. Watu katika maeneo haya si wengi wanaoweza kujijengea nyumba bora na hasa wale wa vijijini kwa sababu bei za bidhaa zinakuwa ni ghali sana. Wakati Dar es Salaam mfuko wa sementi unaweza kununuliwa kwa shilingi 7,000 mpaka 7,500/= Wilayani Ngara au Biharamulo mfuko huo wa sementi unauzwa kati ya shilingi 11,000/=, shilingi 13,000/= na wakati mwingine shilingi 15,000/=, sasa mniambie ni mwananchi gani wa kawaida anaweza kumudu bei hizo? Utakuta Dar es Salaam wakati wananunua mabati yale ya geji 30 ambayo ni ya kawaida kwa bei labda ya shilingi kama 5,000/= au shilingi 6,000/= kwa bati moja, sasa katika maeneo hayo niliyoyataja unaweza kununua mabati hayo kwa shilingi 8,000/= mpaka shilingi 9,000/=. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ifanye mkakati wa makusudi ili kuweza kusaidia Mikoa hii iliyo pembezoni na iliyo mbali na sehemu za Viwanda au Makao Makuu ya nchi. Kwenye viwanda vingi basi waweze kununua bidhaa kwa bei ya kawaida, kuwepo na namna ya kuwafidia ili nao waweze kupata fursa ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba nizungumzie umeme unaosambazwa sasa hivi katika Wilaya za Biharamulo na Ngara. Tunashukuru kwa hatua hiyo lakini kwa Wilaya hizi ambazo zimekosa umeme na ni Wilaya za zamani tangu enzi za Mjerumani, sasa unaziletea umeme wa *generator* tena *second hand,* je, kweli hawa watu umewasaidia? Kwa hiyo, nilikuwa naomba mpango wa makusudi ufanyike ili Wilaya hizi ziweze kupata umeme wa uhakika na kuunganishwa katika umeme unaotoka Uganda kwa sababu hatujaweza kutumia sehemu yote ambayo tunaweza kuitumia. Kwa hiyo, ili uweze ukasambaa katika sehemu nyingi, umeme huu katika baadhi ya maeneo utaleta ugomvi. Kwa mfano, Wilaya ya Ngara mimi nisingependa kuzungumzia historia au siasa yetu ya Wilaya ya Ngara, lakini najua kutakuwa ni matatizo kidogo. Umeme huo kuishia Ngara Mjini usiweze kupelekwa Rulenge, Rulenge nayo pia ina sehemu nyingi nyeti kuna hospitali kubwa ya *Mission* na kuna shule za sekondari nyingi tu sasa zinajengwa, kwa hiyo ningeomba ufanywe utaratibu au mkakati wa kuweza kutusaidia ili umeme huo uweze kufika Rulenge.

Mheshimiwa Spika, lakini pia juzijuzi Mheshimiwa Mbunge wa Ngara, alizungumzia sehemu ya Rusumo ambayo iko mpakani mwa nchi yetu na Rwanda. Upande wa pili wao wana majengo mazuri wana hata umeme lakini sisi kwetu hakuna. Hii naona inazidi kuidhalilisha nchi yetu, kwa hiyo, ningeomba umeme huo basi ufikishwe Rusumo pia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie maktaba ya Mjini Bukoba. Ni maktaba kwa jina. Jengo lake ni bovu kabisa, linavuja, vioo vya madirisha vimeshapukutika vyote, kwa hiyo hata ndani sakafu imeanza kubanduka na hata vitabu vilivyomo ndani basi ni vitabu jina tu kwa sababu vyote vimejaa vumbi na si rahisi kwa kweli hata watumishi wanaofanya kazi humo kuweza kufanya zaidi ya wanavyofanya kutunza usafi. Mimi nasema niwapongeze na kuwapa pole kwa kufanya kazi katika mazingira magumu.

Kama tunavyojua maktaba ni sehemu au ni nyenzo muhimu katika kuelimisha. Kwa hiyo tulitarajia kwamba maktaba kama hii ya Bukoba Mjini ingeweza kuwahudumia watu wanaopenda kujiendeleza katika nyanja mbalimbali. Siku hizi kuna Vyuo Vikuu Huria na Shule za Sekondari. Kwa hiyo, maktaba ni mahali ambapo watu wanaojiendeleza au wasomi mbalimbali au wananchi wa kawaida ni sehemu za kuweza kupata rejea mbalimbali katika masuala yanayohusu mambo ya utandawazi, utawala bora na hata uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu katika maktaba ya Bukoba hata Katiba ya Nchi haipo. Mimi nilipofika pale nilipoongea na wafanyakazi wa pale basi wakaniomba kama ninayo Katiba au kama naweza kuwatafutia Katiba ya Nchi, basi ilibidi niwaachie Katiba yangu ili iweze kuwasaidia wananchi wanaopenda kufahamu mambo mbali mbali.

Mheshimwa Spika, lakini pia mara nyingi hizi sheria zinazotungwa katika Bunge hili haziwafikii wananchi na si rahisi kila mwananchi kuweza kupata nakala ya hizi sheria maana na sisi Wabunge hatuna. Lakini kama ungefanyika utaratibu wa makusudi kuweza kupeleka nakala za sheria mbalimbali tunazotunga zikawa ndani ya maktaba kama hiyo ya Bukoba ambako wananchi wangeweza kujielimisha na kuweza kufahamu sheria zinasema nini. Tuna sera mbalimbali zinazotungwa kama sera ya uwezeshaji ambayo imezinduliwa juzi, sera ya maafa na mambo mbalimbali basi vitu kama hivi natumaini vingekuwa ni muhimu sana kwenye maktaba hiyo.

Lakini nitoe ombi kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni kwa sababu nimejaribu kuchunguza chunguza sikuona sehemu yoyote ambayo inaonyesha kwamba kutakuwa na marekebisho au matengenezo ya sehemu kama zile za maktaba. Basi kwa kweli ajitahidi sana kuiangalia maktaba ya Mjini Bukoba ili iweze kufanyiwa matengenezo na ikiwezekana afikirie kujenga maktaba mpya kubwa ambayo watu wengi wanaweza kupata sehemu za kukaa na kujisomea na kuweza kujielimisha katika mambo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu mimi nina nidhamu sana mbele yako *Speaker Grade One* naomba niunge mkono hoja na nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu.

Naomba nianze kwa kuwapa pole Mheshimiwa Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwa kuwapa pole kwa msiba mkubwa ambao umewapata wa kupoteza mzazi wao. Vile vile nimpe pole Mheshimiwa Hoogan kwa kifo cha binti yake aliyempoteza hivi karibuni. Nitoe pole kwa wenzangu ambao walipata ajali mbalimbali tulioungana nao na mimi. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri kwa faraja na salamu za pole mlizonipa wakati wa ajali ambayo imenikuta wakati nasafiri kuja hapa Dodoma. Kwa kweli shukrani zenu na salamu zenu pamoja na marubani madereva wa Waheshimiwa

Wabunge ambao wamenisaidia kwa kiasi kikubwa wakati nilipopata ajali kuweza kunisaidia nisiweze kuibiwa hata kitu kimoja na hatimaye kufikishwa nyumbani salama.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia. Kwa kweli ni hotuba nzuri yenye mwelekeo ambayo inaonyesha utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Alipoiwasilisha jana kwa masaa mawili na mimi nilipata woga kwamba kwa muda mrefu aliosimama kwa kweli asingeweza kuhimili muda wote wa masaa mawili, lakini nampongeza kwa nguvu alizopata kwa sababu anafahamu wajibu wake ni nini. *(Makofi)*

Lakini vile vile niwapongeze askari wa miamvuli. Nafikiri kwa uongozi wake mzuri Mawaziri wamekuwa msitari wa mbele katika kutekeleza yale ambayo sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiwaomba. Mimi kwa nafasi ya pekee kwa niaba ya wapiga kura wangu wa jimbo langu la Mbarali naomba niwapongeze wale Mawaziri pamoja na kutusikiliza humu Bungeni ndani lakini wamethubutu kwenda kutembelea jimbo langu rasmi na kujua yale ambayo yanatokea katika jimbo langu. Naomba nipoteze angalau dakika 2 kwa kuweza kuwataja kwa majina ili waweze kuingia kwenye *hansard.*

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu Frederick Sumaye, Mheshimiwa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Joseph Mungai, Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Naibu Waziri Festus Limbu akiwa Naibu Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Harith Bakar Mwapachu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko. Mheshimiwa Gedion Cheyo, Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Mheshimiwa Pius Ngjnwandu, Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuja kwao kumekuwa ni faida kubwa kwa njia moja au nyingine katika kutembelea jimbo langu. Nimeweza kupata mawasiliano ya barabara na simu. Mahakama zinajengwa, vituo vya Polisi vimefunguliwa kwa hiyo nawapongeza sana na mambo mengine mazuri ambayo yamefanywa. Kwa pongezi hizi nyingi mimi nasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo tuna haki ya kuwapongeza wenzetu walioko mbele yetu.

Lakini nina hoja ambazo kweli zinahitaji kushawishi au ningependa kuiomba Serikali iweze kuzikamilisha. Wale wenzetu ambao wamepewa dhamana ya kusimamia Sera za Chama cha Mapinduzi wanatakiwa wayafanye. Kwanza ni kauli za Mawaziri ambazo zinatolewa humu Bungeni. Wanapotoa kauli na sisi kwa kauli moja Waheshimiwa Wabunge tukienda kwenye Majimbo yetu tunakwenda kuendeleza yale ambayo wametamka rasmi. Kwa mfano nilipouliza swali la nyongeza juzi kuhusu *TASAF,* Waziri wa Umaskini kwa kweli alijibu na mimi nikaridhika bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini juzi wakati Mbunge wa Mbeya Mjini akiuliza ni sababu zipi zilizofanya TVT isiende Mbeya kama ilivyotangazwa ndani ya Bunge lako Tukufu. Sasa cha ajabu Waziri anapojibu kwamba si mradi imefika au subiri mradi itafika, inatutia unyonge. Kwa sababu kule tunapokuwa majimboni tunakuwa tunaeleza na tunaulizwa maswali tunayajibu kwamba TVT itaanza awamu ya pili. Lakini inapokuja inatokea vinginevyo kwa kweli inatupa huzuni. Tunaomba wenzetu mnapotoa kauli kama kuna sababu za msingi zinazofanya ile kauli ibadilishwe ni vizuri kuitoa humu ndani ya Bunge ili na sisi tuweze kuwafikishia wapiga kura wetu. Hiyo ilikuwa ni kero yangu ambayo nilikuwa nimeipata kwa kweli sikujisikia vizuri sana wakati Waziri mhusika mwenye dhamana na habari alipotujibu hili kwa kweli tulipata huzuni kidogo. Naona ni vizuri nikatoa kauli hii ili ieleweke vizuri. Naomba nichangie upande wa habari hasa vyombo vya habari. TVT na Redio Tanzania wanajitahidi sana kwa sasa na kazi inakwenda vizuri. Hivyo wanahitaji sana kuboreshewa sehemu zao za kazi. TVT wamepata mtambo mzuri wa kisasa ambao ni kivutio, lakini ukifika pale mazingira yake yale majengo ambayo yana miaka zaidi ya 3 hayajakamilika mpaka sasa.

Mtambo mzuri wa kisasa unakaa kwenye majengo ambayo kwa kweli si mazuri. Nilivyokuwa napitia kwenye Bajeti nimeona bajeti ya shilingi milioni 700 sasa sikujua hizi gharama zitatumika tu kwa ajili ya kueneza TVT kwenye mikoa iliyotajwa au ni kwa ajili ya kukamilisha majengo. Kwa hiyo nitamwomba Waziri Mkuu wakati wa kukamilisha hoja yake atuambie yale majengo ana mpango nao upi ili kuweza kuyakamilisha na hatimaye tuwe na kituo kizuri cha televisheni yetu ya Taifa. Lakini kwa upande wa Redio Tanzania tunapata taarifa vizuri, mawasiliano mazuri hilo sina tatizo nalo kwa hiyo nahitaji kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa vile vile kuchangia kuhusu ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe Mbeya. Sisi Wabunge wa Mkoa wa Mbeya tunashukuru kama Wabunge kwa pamoja kwa jitihada kubwa ambazo Serikali imekuwa ikizifanya. Bahati mbaya au nzuri wakati Waziri wa Fedha anatoa hotuba yake ya bajeti sikuweza kupata nafasi ya kuchangia. Lakini mimi napongeza kwa jitihada. Lakini wasi wasi wangu nilioupata hapa fedha iliyotengwa ni shilingi bilioni moja, lakini mkataba ulioingiwa na Serikali ni shilingi 4,800,000,000. Sasa napata wasi wasi hizi fedha zingine za kukamilisha huu mkataba zitatoka wapi. Kwa sababu tumekuwa tukipata matatizo kwanza itaongeza gharama usipolipa kwa wakati ule ambao unatakiwa kulipwa inaongeza ile *delaying time* kwa hiyo gharama itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, sasa labda kwa nafasi hii Waziri wa Fedha kama atatoa jibu kupitia hotuba ya Waziri Mkuu tujue vipi tutapata hizi fedha ingawa walisema kuna mpango wa fedha za kutoka nje kupitia fedha za madeni. Masharti yao yanakuwa makubwa sana inawezekana masharti yasikamilike mpaka pale ambapo mkataba utakuwa umefikishwa kulipa. Kwa hiyo tunaomba kama kuna jitihada zingine ambazo zingeweza kufanywa ili kusudi hizi shilingi bilioni 4.8 ziweze kupatikana mapema mara baada ya mkataba au awamu ya pili ya kazi hii itakapokamilika na ziweze kulipwa kuondokana na Serikali kushtakiwa kwa kutokulipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mheshimiwa Mbunge ambaye nawakilisha makundi mawili katika jimbo langu wakulima na wafugaji. Lakini vile vile kilimo kinachopatikana Wilaya ya Mbarali kingeweza kulisha mikoa hata zaidi ya kumi kama Serikali ingeweza kutilia mkazo kuliendeleza lile bonde pale la Usangu. Kwa sababu ni fedha nyingi sana zimewekezwa pale katika miradi ya umwagiliaji.

Nina miradi minne mikubwa. Mradi wa kwanza ni wa Madibira wa kilimo ambao umeigharimu Serikali shilingi 24 bilioni na unaweza kuzalisha kama utalimwa kwa asilimia mia kutoa karibu tani 12,500 za mpunga. Sasa je ukiangalia na ukienda pale kwenye sehemu ya mradi wataalamu waliowekwa pale kutoka Wizara ya Kilimo ni tisa kazi wanayoifanya ni ya kusikitisha kwa kweli. Yale majengo tangu wale watu wa Afrika Kusini walipoondoka hali imebadilika. Wapo pale hawatoi ushauri wowote na wala hawasimamii au kuangalia cho chote kinachotawala na kufanyika ili kuendeleza kilimo.

Kwa hiyo hili ningependa niiombe Serikali kama kweli tuko serious kuhakikisha kwamba hatutahitaji kuomba au kununua chakula kutoka nje, tusimamie hii miradi ambayo tumeshawekeza fedha zetu. Fedha nyingi sana zimepotea kwenda hapo ili tuweze kupata chakula cha kujitosheleza wenyewe. Lakini kama vile haitoshi tuna mashamba ya aina mbili Kapunga na *Mbarali Rice Farm* ambazo zilikuwa chini ya *NAFCO*. Mwaka 2001 kwenye hotuba ya Wizara ya Kilimo, Waziri alitamka hapa kwenye hotuba yake kwamba Serikali imeamua kubinafsisha mashamba ya ngano kule Hanang.

Lakini mashamba haya mawili la Kapunga na Mbarali litagawiwa kwa wakulima wadogo wadogo katika sehemu za hekta nne nne. Wananchi wakasubiri kwamba hilo tatizo litashughulikiwa. Lakini mwaka 2001 umepita, 2002 umepita, 2003 na mpaka sasa tupo mwaka 2004 ni lini Serikali itatoa tamko lake rasmi kuhusu yale mashamba ili yaweze kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kama ni kutafuta mbia nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu na yeye ni mdau na yeye ana mashamba yake kule Hanang basi aseme mashamba ya Mbarali yano sasa yanatafuta mbia au hayatafuti mbia. Kama yatatafutiwa hili agizo litatekelezwa lini kuanzia mwaka huu au kuanzia mwaka kesho ili hao wananchi wajue ni nini ambacho watakifanya. Kwa sababu sasa hivi pori limekaa halishughulikiwi chochote, majengo yaliyoachwa na wale wafanyakazi wa *NAFCO* Wachina mengi yenye thamani kubwa yameoza yanaanguka ovyo, miundombinu inakufa haina mtu ambaye wa kuiendeleza.

*NAFCO* wamebakizwa wafanyakazi kama 47 ambao labda watalipwa na *PSRC.* Lakini wataishi hapo mpaka lini na hawana shughuli nyingine ambayo wanailetea faida Wilaya ya Mbarali kuiletea nchi nzima. Sasa haya mashamba yote manne kama yangeweza kuendelezwa ninaamini kabisa Wizara ambayo iko chini ya Waziri Mkuu hatutapata tatizo la maafa ya chakula kwa kweli tutapunguza kwa kiwango sana matatizo ambayo yanaletwa na kuagiza chakula kutoka nje. Ninaomba Serikali itilie mkazo

kuhakikisha kwamba mashamba yaliyoko Mbarali iwe ni kipaumbele kusudi zile fedha ambazo zimewekezwa pale zisipotee na hatimaye tuweze kuondokana na janga hili la njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hiyo naizungumza kwa uchungu sana na wananchi kule wanasubiri ni lini Serikali itasema sasa. Baada ya miaka mitatu kukaa kimya na kutokuona maendeleo yoyote ambayo yanafanyika.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa nizungumzie kuhusu mifugo. Kama nilivyosema mifugo laki 600 iko Wilaya ya Mbarali na inatoka sehemu mbalimbali. Mara nyingi sana wakati wa kiangazi wanajipeleka kule kwenye hifadhi ile *Game Reserve* ambapo ndiyo chanzo cha maji ambayo yanazalisha umeme huku Mtera. Sasa mkoa umetoa agizo muhimu kwamba wale wafugaji inabidi mwezi Novemba wawe wameshaondoka na kumetoka mvutano mpaka sasa waende wapi. Tunawarudisha Shinyanga, Mwanza au wapi? Waziri Mkuu alishatoa agizo kwamba baada ya kutoa ushuru wa mifugo isionekane Wilaya inawafukuza hawa wafugaji. Sasa ningeomba Serikali iangalie sisi ni Wilaya ya pili Tanzania kuwa na mifugo mingi na mingi inatoka katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wako kule Wamasai, Wabarbaig, Wasukuma, kwa hiyo ninaomba wote tushirikiane tuungane pamoja Wabunge kuhakikisha kwamba wale wafugaji hawaleti tena matatizo katika Wilaya ya Mbarali, hatuleti tena msuguano kati ya Serikali na wale wafugaji. Kwa sababu lazima wakati wa kuwaondoa katika maeneo hayo kutatokea mvutano mkubwa na hata mauaji yanaweza yakatokea. Naomba kwa hili kwa kweli Serikali iweze kutusaidia kwa karibu sana. Mkisema Halmashauri ya Mkoa ifanye nyenzo watazipata wapi. Halmashauri hazina kipato kingine cha kusaidia kuhamisha hawa wafugaji. Naomba ushirikiano kwa kweli wa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikupongeze wewe mwenyewe kwa kazi nzuri ambazo umekuwa ukizifanya hapa Bungeni. Kwa kweli umetufanyia kazi nzuri sana na hata watoto wakisikia kipindi cha maswali wakisikia ukisema Mheshimiwa fulani simama wanasema mbona hatumfahamu kwa sura tunasikia sauti yake tu. Kwa hiyo, wanafurahi sana kusikia au wakuone ukitembelea sehemu zingine wajue Spika wetu yuko hivi badala ya kukuona hapo. Ahsante sana na naomba niunge mkono asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, mimi nataka nianze na shukrani. Napenda nitumie nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukaa kwenye Bunge letu hili Tukufu tukiwa na hali ya uzima, amani na maelewano. *(Makofi)*

Napenda niungane na mwenzangu Mheshimiwa N'hunga kwa sifa zote zile alizokupa. Kwa kweli sifa hizi zinastahili kusifiwa. Ni zako wewe mwenyewe binafsi na mimi naungana naye kuongezea zaidi kukusifu. Pia nataka nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii iliyopo mbele yetu ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia pamoja na wananchi wenzangu wa Kiwani kwa kutoa mkono wa rambirambi kwa wale Waheshimiwa Wabunge wetu wote waliofikwa na msiba na maafa wakati walipokuwa wakijitayarisha kuja Bungeni. Nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awapunguzie maumivu na awape moyo wa kusubiri. *Inshallah.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nichukue nafasi hii nimpongeze mwenyewe Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote wawili Mheshimiwa Muhammad Seif Khatib na Mheshimiwa Lukuvi pamoja na wataalamu wao wote kwa hotuba yao nzuri waliyotuwakilishia hapa Bungeni ambayo imegusia nyanja zote kwa kweli. Naamini kwamba itatuletea mafanikio mazuri kwenye bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niungane na Wabunge wenzangu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge Danhi Makanga na Madiwani wake wote kwa ushindi wao mkubwa waliochaguliwa kwenye uchaguzi mdogo na hasa kwa kuipa heshima ya Chama cha Mapinduzi kurudi tena kuwa na wao ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Kama mwenyewe jana alivyozungumzia kwamba chama hiki ndiyo chama pekee chenye kuwatetea wanyonge na chenye amani na utulivu. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka niendelee kama nilivyosema hotuba hii haina haja ya kuchangiwa sana lakini kuna baadhi tu ya sehemu na mimi itabidi niitilie mkazo au nivitolee ushauri. Nataka nianze na ukurasa wa 4 kwenye hali ya siasa ya nchi yetu. Nakubaliana na hotuba hii kwamba ni kweli ukilinganisha hali ya siasa ya nchi yetu ilivyo hivi sasa na tunakotoka ni kweli hivi sasa ni shwari.

Lakini nataka nisema kama ilivyosema hotuba hii bado kuna baadhi ya viongozi wanajaribu kuuchochea Muungano wetu na wanajaribu kuichafua amani yetu na utulivu, hii Mwenyezi Mungu aliyotupa. Mimi ningeiomba sana Serikali kama ilivyosema kwamba atakapotokea kiongozi yoyote atakayefanya mambo kama haya basi Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali wamshughulikie kiongozi huyo. Vinginevyo wamdhibiti kiongozi huyo au tutafika mahali turudie pale pale Mwenyezi Mungu atunusuru.

Mheshimiwa Spika, lingine nataka nizungumzie hii Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kuna daftari la wapiga kura. Kwa kweli daftari ni zuri lakini wasiwasi wangu kama alivyoongelea Mheshimiwa Mbunge mmoja jana hapa ni kwamba kwa kweli wananchi wetu hawajakuwa na utaalamu mzuri wa daftari hili.

Tunahitaji sisi viongozi kuwaelimisha zaidi wananchi wetu. Mimi naamini kama daftari hili kama litafuata kama lilivyo basi litaondoa kile kisingizio cha kusema siku zote tunaibiana na wala mwizi hakamatwi. Lakini wasi wasi wangu ni kwamba hili daftari bado hatujakuwa na utaalamu nalo kwa wananchi wetu na muda wa kuwaelimisha wananchi wetu haupo. Kwa kweli mimi ningeiomba Tume hii hapa palipobakia isilale

ijitahidi kwa kuelimisha sehemu mbalimbali za wananchi wetu ili tufanikiwe tufikie lengo lile tulilolikusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nielekee kwenye shughuli zetu za bunge. Bunge letu kwa kweli tunaendesha shughuli zake vizuri na mimi nataka niipongeze kupitisha makadirio ya matumizi ya Serikali yetu, kuihoji Serikali yetu, kuuliza maswali na kujibiwa. Lakini mimi nataka niseme dosari moja tu. Sisi Wabunge nasema ni watumishi wa wananchi. Tunapokuja hapa wananchi wetu mara nyingi huwa wanatusikiliza na kutupa maagizo. Jamani mkifika huko katuulizieni hili na hili ili na sisi tupate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kusikitisha tukifika hapa tunapeleka masuala yetu kwenye Mawizara utajistukia pengine suala lina mwaka mzima halijawekwa kwenye *order paper.* Sasa sijui matatizo haya yako wapi. Pengine suala lile likiwekwa litakuwa limeshapitwa na wakati. Hata pengine kama wale waliokutuma wakisikia wataona aah ni kazi bure tu.

Mimi ningeomba Mawaziri kwa hili suala wakalifanyie marekebisho angalau tu kama likikosekana kama limepelekwa Bunge hili basi angalau kikao kijacho au kinginecho kifuatie basi suala hili liwekwe. Lakini mwaka mzima ndio liwekwe kwenye order paper. Mimi naona hii naomba hapa Mawaziri bado wafanye marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine hapa lililozungumzwa kuimarisha ofisi zetu za Majimbo hasa kwa Majimbo ya Tanzania Zanzibar. Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema atawasiliana na Ofisi ya Waziri Kiongozi kuhusu kuimarisha ofisi hizo. Mimi hapa kidogo nilitaka nishauri kwamba mimi naamini kwamba sisi Wabunge tunayo ofisi yetu ndogo ya Bunge Zanzibar kwa nini hatuwezi tukapitishia kule uimarishaji wetu wote ili na wewe mwenyewe ukawa ndio unaoshughulikia suala hili.

Kulikoni kuipeleka kwenye Ofisi ya Waziri Kiongozi. Sio kwamba nina maana ya kuwa siiamini lakini nasema ni bora kuipunguzia mzigo wakati ofisi zetu tunazo. Mimi ningeshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu basi ikafanyiwe hivyo kwenye ofisi yetu ndogo ya Bunge ya Zanzibar na wewe mwenyewe ukawa mshughulikiaji mkuu Mheshimiwa Spika ndiyo mfuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niipongeze ulinzi wetu na usalama. Kwa kweli mambo mengi tu ya uporaji ya wizi yaliyojitokeza kwenye Taifa letu. Lakini nashukuru ulinzi na usalama unafanya kazi yake. Nalipongeza sana Jeshi la Polisi na ninasisitiza hasa kwamba bado waivalie njuga iwe msitari wa mbele atakapotokea mporaji au wezi hawa kukamatwa basi wasiachiliwe ovyo wapewe hukumu ambazo zinazostahili. Kwa sababu vinginevyo Taifa letu litakuwa na dosari kubwa. Litakuwa ni Taifa la uporaji na wizi na uvivu kadhalika. Mimi naliomba Jeshi la Polisi liongeze juhudi yake ili tuondokewe na uporaji na wizi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nizungumzie kwenye hali ya ukame na upungufu wa chakula. Mimi naishukuru Serikali yetu au nataka nizishauri Serikali zetu

mbili kwa kweli hali ya ukame kwa Taifa letu hili hivi sasa ni ngumu sana. Nathubutu kusema kama ni Tanzania nzima sio baadhi ya mikoa tu iliyotajwa humu.

Lakini nathubutu kusema kama ni Tanzania nzima. Kuna haja ya Serikali zote mbili kukaa kitako ili wakazingatia suala zima la hali ya ukame wa nchi yetu hata tukisema tukizingatia kwamba kilimo ndio uti wa mgongo. Kwa kweli kwa sasa kilimo tunaathirika sana. Kuanzia toka Pemba mpaka kumalizia kote hali ya ukame ndiyo hii hii. Naomba kwa kweli Serikali zote mbili zitilie mkazo kwenye suala hili. Vinginevyo itakuja kutufikisha pabaya hasa tukizingatia mwaka kesho tutakuwa na uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nataka nivipongeze vyombo vyetu vya habari kama walivyogusia Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli wanastahili kwa sifa nzuri wafanyakazi wa vyombo vyetu vya habari ukianzia *ITV,* TVT, Redio Tanzania.

Mimi navipongeza sana kwa sababu kwa sasa hivi mimi nafaidika mpaka jimboni kwangu. *ITV* naipata, TVT naipata naishukuru sana na naipongeza na na waomba waendelee kupanua mitambo yao ili tuenee sote Tanzania nzima. Lakini kuna suala moja hili linalotolewa kwenye *ITV* "Usione So, sema naye".

Mheshimiwa Spika, kuna tangazo hili linalotolewa kwenye *TV,* Usione Soo, Sema Naye. Tangazo hili kwa kweli ni zuri na linatuelimisha vizuri, lakini masikitiko yangu ni kwamba lugha tu inayotumiwa ni lugha ya mjini, siye wa vijijini hatuifahamu lugha hii. Naomba Vyombo vya Habari vitafute lugha ambayo itakuwa ina fasaha nzuri, itakayofahamika kote nchini kwa sababu lengo ni kuelimisha Wananchi wote au Taifa zima, lakini kwa hii lugha inayotumiwa hapa mie naiita ni lugha ya mjini. Hii usione soo, sema naye wengine hatufahamu. Tutumie lugha nyingine kwani zipo lugha nyepesi tu za kufahamika zaidi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna na malalamiko ya Wananchi, sijui kama ni kweli kwa sababu sijafanya utafiti. Lakini mara nyingi nikipita kwenye vikao vyangu Wananchi wangu hunilalamikia kuhusu sarafu hii ya Shilingi mia moja. Wanasema hii kwa kweli ina dosari, mara nyingi ukiichanganya na vitu vingine ina tabia ya kutoa kutu, nafikiri nikisema Kiswahili hicho wengi mtanielewa.

Naomba wale wataalam wa suala hili walishughulikie kama ni kweli kwa sababu mie sijawahi kufanya majaribio, lakini nasema mara nyingi nikipita kwenye vikao vyangu Wananchi wangu hunipa malalamiko hayo hasa ukizingatia wao hawana vipochi vya kuweka fedha, pengine vipochi vyao ni mifuko yao, lakini wanasema wanapoisahau tu kwenye mfuko hata wakienda wakiitizama wanashtukia pengine pesa ile imekwishaanza kutoa kutu. Naomba suala hili lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hotuba hii kwa kweli inachambua mambo yote, ilikuwa haina haja ya kuchangiwa , lakini ndiyo tutimize wajibu tu. Sasa baada ya hapo, nataka nimwambie tu Waziri Mkuu kwamba choyo sina lakini moyo wauma. Kila Wabunge wenzangu wanaposimama hapa husema: "Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwepo Jimboni kwangu." Mie nasikitika kwamba hivi sasa ni mwaka 2004,

lakini mpaka leo hajawahi kunitembelea kwenye Jimbo langu. Nami namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu anisikie, tukimaliza Bunge afanye kwa makusudi tufuatane aje kwenye Jimbo langu na mie aone Wananchi wangu na maendeleo yangu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, narudia tena kusema naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesikia.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu. Kwanza naanza na kutoa mkono wa rambirambi kwa Wabunge wenzetu wote walioondokewa na wapendwa wao wakiwemo wazee, watoto na jamaa. Mwenyezi Mungu inshallah atazilaza roho za marehemu peponi. Amina.

Pili, natoa mkono wa pole kwa wale wote waliofikwa na maafa ikiwa ni ya ajali au kuporwa na majambazi. Mwenyezi Mungu atawasaidia inshallah.

Mheshimiwa Spika, naanza na kuipongeza Serikali ya Chama chetu tawala cha CCM. Ni Serikali ambayo iko makini na katu si Serikali ambayo ni ya danganya toto. Ni Serikali inayotenda mambo na mambo yanaonekana kwa wale wote ambao wana macho, waliokuwa hawana macho ni vigumu kuona, lakini wenye macho wote wanaona na Wananchi wetu ni watu ambao wana macho na wanaona Serikali yao inafanya kitu gani. *(Makofi)*

Ninaipongeza Serikali hii kwa kuwa ni Serikali sikivu, inayosikiliza kero za Wananchi wake na kutafuta ufumbuzi wa kero hizo. Ni Serikali hii hii na sote tunakubaliana na kuwa ni mashahidi kuwa imetandika huduma bora za kijamii, vituo vingi tu vya afya vimejengwa, madarasa mengi tu na mashule yamejengwa kupitia Mpango wa Elimu wa MMEM, maji safi na salama yamesambazwa vijijini kote, huduma za kiuchumi zimeendelezwa kama vile barabara na mengineyo. Kwa hiyo, nashangaa wale wanaosema Serikali yetu ni danganya toto, kwa kweli hawaoni na hawana macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukija katika mradi wa *TASAF,* jitihada za Serikali zinaonekana. Mradi wa *TASAF* umefanya mengi ambayo yanachangia katika kuondoa umaskini usio wa kipato kwa Wananchi wetu. Wananchi kwa kushirikiana na Serikali yao wameendeleza kujenga vituo vya afya, shule, maji safi na mambo mengine mengi kutokana na mradi huu na mradi huu hasa umewafanya watu wamekuwa na ile sense ya ownership kwa sababu ni wao wenyewe wameshirikishwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mradi huu ninaipongeza Serikali na ninaomba awamu ya pili ya mradi huu iendelezwe. Taarifa niliyonayo ni kuwa, awamu ya pili itashughulika pia na umaskini ule wa kipato. Mradi huu unaweza ukatoa vile vile mikopo midogo

midogo kwa Wananchi wenye kipato cha chini. Kwa hiyo, nasisitiza mradi huu uendelezwe na Wananchi wako imara kusaidiana na Serikali yao katika kujiletea maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilalotaka kuchangia ni kuhusiana na demokrasia. Ninaipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kulaza misingi mizuri tu ya demokrasia. Nchini kwetu kuna utaratibu mzuri wa kubadilishana madaraka kwa kupitia uchaguzi. Chaguzi zetu zinakuwa za amani kabisa na kama Wananchi wanakichagua mara zote Chama cha Mapinduzi ni kwa kuwa wanakiamini na wanajua Chama cha Mapinduzi kinafanya shughuli gani za kuwaletea maendeleo yao. Kwa hiyo, wale ambao hawapati bahati ya kuchaguliwa, wajifanyie wenyewe *post-mortem* wajue matatizo yao yakoje wajirekebishe na waende kwa Wananchi waeleze sera zao tuone Wananchi wataamua nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaenda kwa sheria na utawala bora. Katika kipindi chote sheria nyingi tu tumezipitisha hapa na zinaanza kutumika, si Serikali ya mitulinga, ni Serikali ya kisheria. Serikali yetu inaelewa maana ya jinsia na umuhimu wa kushirikisha jinsia zote katika maendeleo na imejitahidi kutoa elimu kwa Wananchi wetu juu ya mambo ya jinsia na kuonyesha kuwa wanawake wakipatiwa nafasi wanaweza kufanya kazi vizuri sawa sawa na wanaume. Kwa maana hiyo, ninaamini sana kuwa ifikapo mwaka 2005 Bunge letu hili litakuwa na idadi ya wanawake zaidi ya asilimia 30 kama ilivyokubalika katika Azimio la Beijing. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitembelea nchi moja ninaiweka kwenye mabano, idadi ya Wabunge wanawake katika Bunge lile ilikuwa ni chini ya asilimia tano. Nikamuuliza kiongozi mmoja mkubwa tu wa nchi: "Mheshimiwa wewe, kuna Azimio la Beijing linalosema idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi zifikie asilimia 30 angalau ifikapo 2005; je, ninyi mna mpango gani wa hilo?" Akaniambia: "Sahau kabisa suala hilo, hapa halipo! Ukimsimamisha mwanamke tu kugombea yaani Chama chako kimekufa kabisa. Kama hutaki kura basi msimamishe mwanamke na kama ukimsimamisha kura hupati na mwanamke huyo ataanza kuzomewa na kushambuliwa na vyombo vyote vya habari na kumkashifu." Kwa hiyo, Serikali yetu ndugu zanguni imepiga hatua kubwa sana ya kidemokrasia, tunaipongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu iko wazi kabisa. Sasa hivi kuna neno la kitaalam wanasema ni *E government.* Maelezo yote yako katika tovuti mbalimbali, tangu Bunge ina tovuti yake, juzi tu Waziri Mkuu ametuzindulia vile vile tovuti, mambo yote yanapatikana mle. Kwa hiyo, ni moja katika kuendeleza demokrasia. Tunapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja katika elimu ya juu. Tuko katika *era* ya utandawazi, wahitimu wetu wa vyuo vikuu ni wachache sana kulinganisha na nchi nyingine. Kwa mfano, natoa mfano wa Misri ambapo tumeenda kutembelea ni kuwa, kila mwaka wanatoa karibu wahitimu 700,000; lakini sisi hapa Tanzania tunatoa chini ya 20,000. Kwa hili, tukiendelea na mtindo huu huu, tutatolewa kabisa nje ya soko la ajira.

Ajira zetu na nyingine zitachukuliwa na watu wa nje na tutakuwa hatuna wa kuwalalamikia, wa kujilaumu ni sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na mipango mizuri ya MMES, ningeshauri Serikali kupitia Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ikaandaa mipango mizuri zaidi ya kushajiisha ujenzi wa vyuo vikuu, kushajiisha wawekezaji wa nje na ndani pamoja na ile nia nzuri ya kutoa mikopo kwa wanaotaka kuingia vyuo vikuu ili idadi ya wahitimu katika nchi yetu nayo iwe kubwa ili tuweze kupambana na wenzetu katika soko la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la UKIMWI. Nachukua nafasi hii kuipongeza *TACAIDS* kwa kazi nzuri inayoifanya ya kupambana na UKIMWI. Mwenyekiti Mtendaji; Meja Jenerali Mstaafu Lupogo na timu yake wanafanya kazi nzuri sana katika mapambano. Aidha, nataka kuipongeza *TAPAC* pia kwa jitihada inazofanya za kupambana na UKIMWI ikiwa ndani ya Bunge kwa kuchangia michango mbalimbali na nje ya Bunge vile vile. Waheshimiwa Wabunge sasa wamekuwa walimu, wakienda katika mikutano yao majimboni mwao moja katika agenda zao ni suala la UKIMWI. Kwa hiyo, ninaipongeza *TAPAC* pia kwa kazi nzuri inayofanya, lakini ningeshauri elimu hizi zikateremka zaidi vjijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninaipongeza Serikali kwa kuandaa huu Mpango wa *Care and Treatment* ya wagonjwa wa UKIMWI kwa sababu ilikuwa tabu kupatikana dawa hizo kwa watu wenye kipato kidogo. Lakini mpango huu ukisimamiwa vizuri na dawa zikitolewa vizuri na ukitolewa ushauri mzuri wa matumizi ya dawa, Wananchi wetu wanaweza wakanusurika na vifo vya haraka haraka. Pia, kuna watoto yatima ambao wanahitaji matunzo, tujitahidi kuwatunza, Serikali ikiungana na wanajamii wenyewe kwa sababu hawa hawakupenda, wamejikuta tu katika dimbwi hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni la Taifa, Mheshimiwa Waziri alituelezea ni kwa nini tunakopa na ninakubaliana naye, ili tuendelee ni lazima tukope kwa vile vyanzo vyetu vya ndani havitoshi. Hata nchi zilizoendelea pia zinakopa, ingawa wanakopa zaidi katika vyanzo vyao vya ndani. Kwa maana hiyo, deni letu limekuwa kubwa mno kwa vile tunakopa kila siku na tunawaachia burden kubwa vizazi vijavyo kuja kulilipa deni hilo. Ninashauri mikopo hii itumike kwa zile Sekta ambazo zitawezesha ku-*generate income* hapo baadaye ya kuweza kulipia hii mikopo, *otherwise* mikopo itakuwa hailipiki na wadai watakuwa na kauli kubwa. Kuna siku moja kwa mfano wanaweza kutuambia tuwape Kisiwa cha Mafia ili kulipia mkopo wao. Kwa hiyo, kuzuia jambo hilo tupange mpango mzuri tu wa kulipia mkopo.

Mheshimiwa Spika, suala la Zanzibar Mheshimiwa N'hunga hapa amelieleza vizuri. Suala la uchumi na mapato ya Zanzibar ni kweli kabisa hali ni mbaya na tunaelewa hali iko mbaya sana. Mimi nilikuwa kwenye Bodi ya Mapato kule Zanzibar, katika ile miaka niliyokuwa nikifanya kazi ya 1988 mpaka 1990 huko. Mapato yaliyokuwa yanapatikana TRA yalikuwa yanatosha kabisa kulipia mishahara na ilikuwa ni kama utaratibu yale hayaguswi, mwisho wa mwezi yanalipiwa mishahara, watu wote wanafurahi.

Mapato ya ndani, ile *hotel levy* na vyanzo vingine yanatumika kulipia mambo ya *OC,* lakini sasa hivi haipo hivyo. Ninashauri Serikali hizi mbili zipitie sera zetu, sheria zetu na taratibu zetu zinazogusa nchi zote hizi mbili kuona kwa makusudi namna gani Zanzibar inaweza ikasaidiwa kiuchumi, kama si hivyo hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda ungalipo nina suala lingine la utalii. Utalii ni chanzo kizuri sana na kikubwa katika kuleta mapato ya nchi. Ni chanzo ambacho hakina bughudha ya mkusanya kodi, kinataka tu kumshawishi mlipakodi ambaye ni mtalii, pesa atazitoa mwenyewe mfukoni, atasafiri atakuja kwenu kwa kumshawishi vizuri tu. Kwa hiyo, tuendelee na mipango mizuri ya kuwashawishi hawa na ikiwezekana tuwatumie Mabalozi. Ikiwezekana vitayarishwe vipeperushi vingi zaidi na kila anayekwenda nje hebu na achukue hicho kipeperushi kokote tu. Mfano amekutana naye huko kwenye ndege na rafiki yake naye ampe. Au umekwenda umetembezwa huko umepata nafasi mpe, pengine hiyo itasaidia pia.

Mheshimiwa Spika, sitaki tena kugongewa kengele na nimekwenda haraka haraka kama Mheshimiwa Pawa hapa, amenifunza kidogo kwenye mbio. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mie niungane na wenzangu kuwapa pole wale wenzetu wote waliofikwa na misiba mbalimbali. Aidha, nimpongeze rafiki yangu Danhi Makanga kwa kurudi tena ndani ya Bunge hili na nimtakie kazi njema. Ingawa mzee wangu mmoja aliniambia: "Ni vizuri mtu kuhamia ndani ya nyumba mpya tena akajifurahisha sana, lakini ni vibaya kuilaumu au kuidharau nyumba ya udongo ambayo alizaliwa na akalelewa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, pamoja na wasaidizi wake. Aidha, nimpongeze Kiongozi wetu wa Upinzani kwa kutuwakilisha vizuri katika kutoa maoni ya jumla ya Kambi yetu juu ya hotuba hii ya Waziri Mkuu pamoja na mambo mbalimbali yanayohusu nchi yetu. Baada ya hayo, sasa niseme machache tu ambayo nimekusudia kama mchango wangu katika hotuba hii. Dunia inabadilika na sisi kwa bahati nzuri sasa hivi tuko katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Hapa kwetu tunasema kuwa kuna pillars tatu tofauti kabisa. Ya kwanza ni Bunge, pili ni Serikali na tatu ni Mahakama. Lakini mimi nashtuka kuwa suala la Bunge bado kuliegemeza, amesema mwenzangu mmoja na naomba nisisitize na mie suala hili. Suala la Ofisi ya Bunge kuiegemeza kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa namna fulani ni kukidharau chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani hata kidogo Waheshimiwa Wabunge wote hapa ikawa bosi wetu ni Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu yanapokuja masuala ya fedha, hii ni hatari kidogo! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hatari!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Ndiyo, kwa sababu tunapotaka matumizi yoyote ni lazima tupate idhini yake kwa sababu pesa zote zinaombwa na Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Ningeomba suala hili liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, sisi tunatembea tembea na Wabunge wenzetu wa nchi nyingine hizi, hata wakitaja tu hali zao basi unaona tabu kidogo na wewe kujieleza. Ingawa Waandishi wa Habari nawashukuru kwa kazi yao nzuri, lakini wamekuwa wakieleza masuala ya Wabunge kana kwamba ni watu wanaopata saaana. Hii ni hatari kwa sababu ni kama sura mbaya hivi inachoreka baina ya Wabunge wa Wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dr. Aggrey, msomi mmoja kutoka Ghana alisema: "Ukimuelimisha mwanamke unaielimisha familia na unaielimisha jamii." Mimi nasema, ukimpa uwezo Mbunge basi unawapa uwezo watu wake ambao wamemchagua. Ni jambo la kawaida sana hapa Wabunge hicho wanachokipata mfukoni mwao basi asilimia kubwa inakwenda kwa Wananchi wao. Sasa hii lawama ya kila leo kuwa huyu anapata hiki, huyu anapata kile, nafikiri vijana wetu wa Vyombo vya Habari wangesema basi na yale ambayo Wabunge wanayafanya wenyewe kutoka mifukoni mwao, ingekuwa jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niseme basi kuwa ofisi hii inahitaji iongezewe. Ofisi hii ya Bunge inapitisha bajeti yetu ya zaidi ya Shilingi trilioni 3, yenyewe imepewa Shilingi bilioni 16. Si kidogo, lakini si nyingi kwa kazi ambazo Waheshimiwa Wabunge wanazo na mahitaji ambayo wanayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nije katika hotuba ya Waziri Mkuu na nianze moja kwa moja katika ile hoja ya kuwa vikosi vya ulinzi na usalama vinaongezewa uwezo. Mimi nasema naunga mkono hili na ninaomba nia iwe ni nzuri na tafsiri ya jambo hili iwe ni nzuri kwa sababu inaonekana tunatafsiri mambo kwa sababu kayasema fulani. Hapana, tusimuangalie aliyesema, tuangalie kilichosemwa kwa sababu sote tunawatumikia Wananchi na Wananchi wanafuatilia. Watanzania siyo wajinga kiasi hicho, linalosemwa Bungeni wanalifuatilia na pia wana uwezo wa kutafsiri hata maana ya lile lililosemwa. Tukisema vikosi viongezewe uwezo, mimi napenda viongezewe uwezo kwa sababu si tumesikia tu karibuni hapa Askari wetu pale Dar es Salaam wamevamiwa wakapigwa, tena wakapigwa na majambazi kwa silaha. Pamoja na kuwa wao walikuwa na silaha, lakini silaha walizokuwa nazo majambazi zilikuwa ni kubwa kuliko zao na matokeo yake vijana wetu wakapoteza roho. Binafsi naona wakipewa uwezo halitanisikitisha, lakini uwezo huu usiwe ni tafsiri ya kuwadhalilisha watu wengine. Hicho ndiyo ambacho watu wanakilalamikia, si jingine lolote.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nije kwenye suala la Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi ni kitu kingine ambacho kipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kweli juhudi ambazo zinachukuliwa za kutaka kuanzisha daftari la wapigakura pande zote mbili Zanzibar na hapa, nafikiri ni hatua nzuri na tuiombe Serikali basi haya mafungu ambayo Tume hii imeombewa iwape.Lakini ningeomba Tume ya Uchaguzi na Serikali kwa jumla ichukue jukumu la kuwaelimisha Wananchi juu ya elimu ya

wapigakura. Hii hoja tu ya kuwa Vyama vya Siasa vifanye kazi hiyo, ukizungumzia hivyo unazungumzia uwezo na unazungumzia uwezo wa kifedha. Vyama vingi vya Siasa vinapata asilimia ndogo sana ya pesa kama ruzuku na havina mitaji ya kuwawezesha, sasa si rahisi kutembea nchi nzima ukawaelimisha Wananchi. Kazi hii ningeomba ifanywe na Serikali tena kwa nia safi ya kuwafanya Watanzania waelewe jukumu lao hasa kwa sababu tunakuza demokrasia na utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nije kwenye ahadi ya Serikali ya kutoa pole kwa wale waathirika wa kadhia ile ya tarehe 27 Januari. Serikali imekuwa na maneno mazuri juu ya jambo hili, imetoa ahadi nyingi juu ya jambo hili, lakini ahadi tupu haiwezi kutelekwa ndani ya nyungu ikaliwa! Unamwambia mtu nitakusaidia kesho, nitakusaidia kesho kutwa, anapata moyo, lakini mwisho anakuwa hapati kitu. Ni vizuri kama kweli Serikali imekusudia kufanya jambo juu ya watu hawa, kuwapa msaada japo mdogo basi bora wawape kwa sababu wengine wanaathirika. Kuna watu wana risasi miguuni mwao, sasa akipata pesa atakwenda hospitali atalipa atatolewa, kuliko kila siku kuwa unamwahidi. Kuna mtu hana mguu, akipata pesa atanunua mguu wa bandia atatembelea. Nafikiri tuwe na nia nzuri juu ya watu hawa na ionekane kuwa tuna lengo kweli la kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kuna sehemu katika ukurasa wa 65 Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia vurugu. Mimi nasema kama alivyosema yeye, ninalaani sana vurugu katika wakati wa uchaguzi. Lakini vurugu hizi mimi kwa maoni yangu zinasababishwa na watu, lakini ni nani ni vizuri tukafanya post-mortem nzuri tukajua ni nani kwa sababu chaguzi zina watu wanaoziendesha ambao kwa bahati njema ndiyo waliopo sehemu zinakofanywa chaguzi. Waziri Mkuu wala Mawaziri wake hawako huko, lakini wale watu wadogo wadogo wanaoendesha chaguzi ndiyo ambao mara nyingine wanafanya vitu vinavyopelekea subitafaha. Ni vizuri basi na wao wakaelimishwa wajibu wao hasa kwa sababu tunaendelea kukua. Tumeanza 1995, tumekuja 2000 na tunategemea inshallah mwisho wa mwaka huu kufanya chaguzi za Serikali za Mitaa na 2005 Uchaguzi Mkuu. Ni vizuri tukajenga mazingira nchi yetu ikaonekana imekua kweli kidemokrasia. Lakini ukisema vurugu tu, mie siwezi kuelewa ni nani anayefanya vurugu. Ni mimi ninayesema kuwa kura yangu ihesabiwe hapo kwenye kisanduku au Askari anayekibeba kisanduku akaenda nacho kwa Mkuu wa Wilaya? Sasa kama vurugu ninafanya mimi ninayesema: "Yakhe hicho kisanduku usikiondoshe hapo bora tuhesabu tujue." Basi sawa kama hiyo ndiyo vurugu. Lakini ikiwa Askari anayekichukua akaenda nacho mahali nisipopajua mimi hiyo si vurugu, basi ni vizuri tafsiri hapa tukaiweka vizuri na tukalaani vurugu za namna zote mbili ili uchaguzi wetu ukawa wa huru na wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kawaida huwa sipendi kusema maneno mengi sana kwa sababu sitaki kengele zinililie hapa. Lakini jambo lingine ambalo napenda niliseme ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelisema hapa ni hali ya chakula. Ningependa niseme tu kwamba, sisi tunatembea tembea kidogo humu mitaani, inaonekana kuna tabia hii ambayo ni ya hatari kidogo, watu wanapovuna wanafurahi sana na wakifurahi sana na wakifurahi basi wanacheza ngoma na wakicheza ngoma, ngoma ina vishuo vyake ni lazima vipatikane vinywaji kidogo na mambo mengine, sasa chakula inaonekana

kinatumiwa vibaya. Napenda sana Mheshimiwa Waziri Mkuu awaombe Wananchi chakula wakihifadhi wasikitumie kwa kupika pombe za kienyeji ili baadaye mzigo wa Serikali wa kupeleka misaada mbalimbali ya chakula ipungue, vinginevyo nyimbo hii ya kuwa kila siku sisi hamtusaidii, mnapeleka chakula kidogo, watu wanapika mboga kwa ajili ya kuisonga ugali yatakuwa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niseme hali ya kwetu Zanzibar. Hali ya uchumi Zanzibar ni mbaya tena ni mbaya sana. Kwani uchumi ni nini? Uchumi ni makusanyo na makusanyo yanategemea biashara. Biashara kwetu Zanzibar imekufa, sasa ni vizuri basi vyombo vinavyohusika vikakaa vikaangalia, hivi kuna sababu gani ya mfanyabiashara ambaye alikuwa akishusha mzigo wake Unguja akalipa ushuru halafu watu wakaja wakachukua wakaja wakauza mahali pengine, leo anaona unafuu ashushe Dar es Salaam au ashushe Tanga, kulikoni? Sasa, ikiwa hapashushwi mzigo hapafanywi biashara, ikiwa hapafanywi biashara Serikali haikusanyi. Tutaendelea kulia matokeo yake hata kilio chetu mnatuchotea mnatupa. Cha kugaiwa chamalizwa haraka bwana, ni vizuri tukaangalia sheria zetu, tukaangalia kama kuna vikwazo vinavyowapata wafanyabiashara hasa njiani baina ya Zanzibar na kuja Bara katika kuleta mzigo mpaka mtu aka-*opt* kufanya biashara yake hapa tuviondoe ili hali ya nchi yetu irudie katika namna yake ilivyokuwa na Wananchi waweze kustirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja ya Waziri Mkuu. Kwanza nampongeza Waziri Mkuu kwa namna alivyotoa mada yake. Tumeisoma ni ndefu, ina mambo mengi ya kufanyia kazi. Kuna mambo mengine ambayo sitayaunga mkono, lakini nitamwomba Waziri Mkuu ayafanyie kazi. La kwanza, Msajili wa Vyama vya Siasa. Ofisi hii sijui iko kwa sababu gani! Mtu mzima, mwaka mzima anakaa pale kwa kazi ya kusajili Vyama. Kaishasajili Vyama vimefika sijui 20, utitiri wa Vyama katika nchi hii ni vurugu. Sasa cha kushangaza, kama yeye ni Msajili na ni Mwanasheria na anasoma Katiba za Vyama, anaachiaje udikteta unaingia katika Vyama? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nalizungumza hili kwa sababu kuna Chama cha *TLP,* Mwenyekiti anachukua pesa za ruzuku ambazo ni pesa za kodi yetu ananunua nyumba yake. Hili nalisema kwa sababu hii ni balaa!

**MBUNGE FULANI:** Ni balaa!

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mwenyekiti anakuwa yeye ndiyo mwenye agenda kwenye kichwa chake na bado Msajili anaona Chama hiki ni cha demokrasia, kwa nini asikifute? *(Kicheko/Makofi)*

Mimi nasema haya, nilikuwa Kilimanjaro tulikuwa na chaguzi kule, nimepata *experience* nzuri sana ya pesa za ruzuku. Pesa zetu za ruzuku ni pesa za kodi yetu, niliona jinsi zinavyonunua pombe! Unakwenda kwenye kijiji, sisi wengine ambao

ruzuku yetu ni kidogo hatuwezi kununua pombe tunazungumza kwa mdomo tu, lakini mwenzetu ananunua pombe kijiji kizima! Hii ndiyo demokrasia tunayotaka? Kwa nini Msajili alinde Chama kinachofanya mambo kama haya? Vyama vya namna hii ni vurugu katika nchi jamani! *(Makofi/Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Ni heri tuamue yaishe tuwe na vyama vichache. Hata Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alisema tuwe na vyama vichache ambavyo ni makini halafu tuunde Serikali ya umoja ili tujue tunakwenda wapi, ndiyo, mtapinga lakini ndiyo ukweli wenyewe. Wenzetu Malawi wamefanya na wenzetu Kenya wamefanya. Hii ni dunia tunazungukwa na watu wengine, hatuwezi kuendelea kusema tu sisi wote hapa ndani ni Wabunge, sisi wote *we are equal* hakuna haja ya kutukanana hapa. Sisi wote tunaweza kuchukua madaraka tuchanganyike tuwe wamoja. Kwa hiyo, hilo namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanyie kazi, ili vurugu hizi ziishe katika nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunazungumzia mambo ya kuondoa umaskini, tumefuta hata kodi kwa wale wafanyabiashara wadogo wadogo ili wawe wengi lakini hii kuna hatari. Mimi nasema baada ya mwaka mmoja, miaka miwili, tutaiona hatari. Vijana wote watakuwa Wamachinga kila mahali katika miji yetu. Miji yote itajaa machinga. Badala ya ku-*empower* watu wachache ambao wanaweza ku-*create employment. To employ* watu wafanye kazi, watu wapate *opportunities* za kufanya kazi. Una-*create* Machinga mijini, akiwa mgonjwa hawezi kupata chochote, ni lazima awe anatembeza na mikono yake ndiyo biashara tunataka kuzijenga katika Tanzania. Nchi zilizoendelea panakuwa na matajiri wachache lakini wana-*create employment* kwa watu wote. Tanzania watu wanaona ajabu mtu kama eti Waziri Mkuu, anakwenda benki anakopa shilingi milioni 50 ananunua nyumba kwa kujiendeleza wanaona ni dhambi, dhambi gani? Mimi nilitazamia Mawaziri wote na Wabunge wawe ndiyo mfano wa kuigwa. Ndiyo wawe matajiri wa kuweza kutoa ajira kwa watu wengine. Maskini atamsaidiaje maskini mwenzake? Lazima tuwe na matajri wachache ambao wata-*employ. (Makofi/Kicheko)*

Mimi binafsi naajiri watu zaidi ya 500 na 500 wanaajiri wengine *over 1000.* Sasa tukiwa nao watu wengi namna hiyo tukiwa na watu 10 katika kila mkoa shida ya njaa itakwisha *unemployment* itakwisha, lakini siyo ku-*create a Machinga's* katika miji hiyo haitatuletea maendeleo. Hilo ni wazi tutake tusitake lakini nchi zilizoendelea ni watu wapewe kazi. *(Makofi)*

Sasa tunakuja katika hali ya chakula. Hili niliwahi kulisema tena hapa Bungeni na nikachekwa, wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika nchi hii tuwaambie wawekeze katika kilimo. Kilimo *is a profession* tusifanye Watanzania wote ni wakulima eti ndiyo *profession* yao wanajua, hawajui ndiyo maana tuna njaa kila siku. Tulete watu wanaojua kulima wachache hata 10 tu Tanzania watalima chakula cha kutosha kulisha Tanzania nzima na kuuza chakula cha ziada. Lakini kwa nini hawaji? Tujiulize kwa nini hawa watu hawaji? Shauri ya *Land Policy. Land Policy* yetu ina matatizo kwa sababu

tunang'ang'ania *lease* hatutaki kuweka *free hold* na hawa wawekezaji wakija hawataki *lease* wanataka *free hold.*

Kwa nini nchi yetu ni kubwa tusitenge sehemu ya *free hold* na sehemu nyingine tukafanyie *lease* ili tu-*attract* watu hawa waweze kuja kulima na kutupatia chakula cha kutosha na cha kupeleka nje? Hili ni jambo rahisi tu. Lakini tunang'ang'ania tu watachukua, watachukua nini? Ikiwa mbaya sana yakija matatizo tuta-*nationalize* tuna uwezo huo. Bunge hili litakaa litasema hili tuchukue na tunaweza kufanya hivyo. Lakini tunataka tulete watu ambao ni wakulima wanaojua kilimo, Watanzania hatujui kulima, ndiyo maana tunakuwa na njaa mara kwa mara. Lazima tutafute njia ya kuondoa hii njaa. Tukisema tunategemea jembe la mkono, tunategemea wakulima 80% ya Watanzania eti walime chakula cha kututosha tunajidanganya. Ni wakati muafaka Waziri Mkuu, achukue hatua ya kuhakikisha *Land Policy* inabadilishwa na tunapata wawekezaji ambao wako *serious* ambao wanaweza kuendeleza kilimo katika nchi hii na tatizo la njaa litaisha. Wakulima hata wawili tu unawapa Bonde la Kilombero nchi hii itajaa chakula tele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme jambo lingine dogo, si dogo, lakini lina matatizo kwa sababu limeleta mauaji makubwa sana kule kwangu Moshi. *TANROADS* katika barabara ya Kiboriloni kuanzia mwaka jana 2003 mpaka leo wamekwishakufa watu 22 kwa kugongwa na magari. Nimefanya bidii kuwaambia *TANROADS* waweke matuta kwa kuwa ni sehemu ya mjini na watoto wanavuka barabara kwa wingi lakini ni zaidi ya miaka miwili hawajafanya chochote na watu wanaendelea kufa. Watu 22 wamekwishakufa katika kipindi ambacho hakijafika hata mwaka mmoja na wote wanagongwa na magari. Nimeandika barua mpaka nimechoka na hicho ni kilio cha watu wa Moshi. Mheshimiwa Waziri Mkuu tungeomba ulifanyie kazi, hayo matuta yawekwe na watu wapone na ajali hizo. *TANROADS* inafanya kazi nzuri sana. Lakini mtu akikufanyia kazi nzuri wakati mwingine anaharibu. Mimi ni mtu ninayesafiri na barabara, kuna vibao unaweza kukuta kibao cha shule kimeandikwa. Kibao kiko kwenye eneo la *road reserve, okay* lakini kile siyo kitu cha hatari unakuta kimepigwa alama ya "X" maana yake hakuna hata ile shule. Sasa kile kibao kinachoonyesha *direction* kina ubaya gani mpaka kinawekwa "X"? Sasa kama ni mgeni ametoka mbali anataka kwenda shule labda ya Kibaigwa au mahali pengine popote, akakuta kimewekwa "X" atakwenda kule au atarudi? *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Atarudi.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu ningekuomba jambo hilo vile vile uliangalie wewe mwenyewe unaona huko barabarani maana yake inakera. Hicho kibao siyo nyumba ni kibao cha shule na kiko kwa muda au kibao cha zahanati kinawekwa "X" maana yake nini? Ni vitu vidogo vidogo, lakini vinakera na vinakuwa havina maana.

Sasa labda nirudi katika Daftari la Wapiga Kura. Tumeambiwa hili ni Daftari la kudumu. Daftari la kudumu maana yake ni la kudumu, watu wanakufa na wanazaliwa kila siku. Sasa limepangiwa siku 21 kuandika, mimi hapa linaniletea matatizo, kila siku

watu wanafikisha miaka 18 na kila siku wanakufa watu. Sasa linapokuwa Daftari la kudumu halafu likapangiwa siku 21 kujiandisha, *the whole meaning* ya daftari la kudumu inakuwa halina maana. Vile vile kuna jambo lingine, nchi yetu ina utaratibu wa *administration* mzuri sana, maana tunakwenda mpaka kwenye kaya. Sasa hivi vituo vipya vimetengenezwa vya kuandikisha watu vya nini wakati vingeweza kutumia *the administrative structure* ambayo tunayo na tukapunguza fedha nyingi sana ambazo zingetumika? Nilikuwa nazungumzia Daftari la Kudumu na nikasema tuna *administrative structure* nzuri sana, mimi ningedhani tunge- *serve a lot of money* kama tungetumia hizi tulizonazo badala ya ku-*create* vituo vipya vya kuandikisha watu. Hili ni jambo la maana ni jambo la ku-*serve* fedha badala ya kupoteza fedha pasipo na sababu maana tuna mpaka kata ambako wanajua vizuri watu wa pale kuliko kwenda kuweka ka-*station* mahali fulani ili watu waje wajiandikishe pale, kwa kweli naona hiyo haitatufanikisha wala haitatuendeleza vizuri kwa sababu hata watu *fake* wataandikwa kwa sababu watakuwa hawajulikani katika sehemu zile. Lakini tungetumia vile vituo vyetu tulivyonavyo sasa vingetufanyia kazi nzuri sana. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama utazingatia hayo machache niliyosema nitakuwa sina ugomvi na hoja yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Msemaji wa mwisho kwa asubuhi hii....

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mimi namwita Mheshimiwa Grace Kiwelu. Naomba ukae chini ili aliyepewa nafasi ya kusema aweze kusema. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa napenda kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mpenzi. Ninaamini kabisa walimpenda lakini Mwenyezi Mungu alimpenda zaidi na tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena na kurudi katika Bunge hili. Hoja si kwamba amerudi kwa chama gani, hoja kubwa na kazi kubwa ni amerudi tena ndani ya Bunge hili kuja kufanya kazi ya wananchi na tushirikiane naye ili tuweze kuwawakilisha wananchi wetu vizuri. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wawili, walioko katika Wizara hiyo na Katibu Mkuu ambaye ni mwanamke na wataalam wote wa Wizara hii kwa hotuba yao nzuri. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ilikuwa ni nzuri na tunaomba yale yote aliyoweza kuyaandika katika hotuba yake yaweze kufanikiwa. Maana nchi yetu ni hodari kwa hotuba nzuri na mipango mizuri, tunajua kuiandika na kuipanga, tatizo ni utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa wana kamati waliopitia bajeti hii, lakini ninayo machache ambayo ninaomba nichangie. Nikianza na huduma za jamani upande wa elimu. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, kwa juhudi yake kubwa ya kutaka kuboresha elimu katika nchi yetu. Kwa kuwa tunaamini kabisa kwamba elimu ndiyo urithi pekee uliobaki kutoka kwa wazazi kuwapa watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zimetengwa fedha nyingi sana kwenye MEM na MMES lakini kama hatutakuwa na utaratibu mzuri wa walimu wengi na bora katika shule fedha hizi ambazo ni mkopo zitakuwa zinapotea na watakaokuja kulipa kama tulivyoambiwa ni wajukuu zetu. Tunajua kabisa kazi ya ualimu ni kazi ngumu na hii ambayo tunasema tutawapa mafunzo kwa kipindi cha mwaka mmoja wanafunzi wa kidato cha sita na kwenda kuwafundisha watoto inataka moyo, ukijua kabisa kwamba kumfundisha mwanafunzi mpaka ajue kusoma na kuandika inahitaji kazi kubwa, siyo tu kwa kuwa amemaliza kidato cha sita na kumpeleka anaweza kumudu kazi hiyo.

Hao wanaomaliza mafunzo baada ya mwaka mmoja na kupelekwa vijijini, kibaya zaidi wanafika kule wanakaa zaidi ya miezi 4 au 6 hawajapata mishahara yao, sidhani kama watakuwa na moyo wa kuweza kuwafundisha wanafunzi hawa na kuelewa vizuri. Hivyo tunaomba Mheshimiwa Waziri afuatilie jambo hili, tunajua nia yake ni njema lakini ajaribu kuangalia ni mpango upi ambao utakaofaa na ambao utaleta maendeleo kwa nchi yetu na katika elimu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizingatia katika vijiji vyetu tatizo la walimu ni kubwa, vijijini walimu wanaokubali kwenda kule ni wachache na wanafunzi wanakosa masomo yao ya kutwa kama inavyotakiwa kiratiba. Hivyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie hili kwa kuwa fedha hizo ni nyingi ziweze kuwa na mafanikio katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kulisema ni kuhusu Ukimwi. Kwanza niwapongeze *TACAIDS* kwa kazi yao kubwa ambayo wameishaifanya mpaka sasa. Lakini niwaombe muda wa semina, warsha, makongamano umetosha. Sasa twende vijijini kule ambako waathirika wengi wako wa Ukimwi ambao wengi wametoka mijini wamepelekwa vijijini wanakufa kwa njaa wameshapata ugonjwa huu tayari wana upungufu wa kinga mwilini, wengi wanakufa kwa sababu ya kukosa chakula. Fedha nyingi za ukimwi zinatumika visivyo. Tunaomba fedha hizi ziende kwa walengwa waathirika wa ukimwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tulilosikia ambalo tunaiomba Serikali, itupe ufafanuzi kama ni kweli kuhusu vitabu vilivyotengenezwa kwa ajili ya kutumika katika shule zetu. Tumeambiwa vimetengenezwa vitabu vingi ambavyo vimetumia mabilioni ya fedha ambazo zimetoka katika mfuko huu wa Ukimwi na vimeshindwa kutumika kutokana na kupungua mambo yaliyotakiwa kuwa ndani ya hivyo vitabu. Sasa tunaiomba Serikali kama ni kweli je, wale waliohusika wamechukuliwa hatua gani mpaka sasa? Maana yake fedha hizo zingekwenda vijijini kwa waathirika wa Ukimwi, nafikiri

wangeongeza muda wao wa kuishi kwa kupata chakula na wengi wanakufa kwa sababu ya njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuliongelea ni kuhusu utawala bora nikianza na rushwa. Tukubali, tukatae, suala la rushwa lipo katika nchi yetu, tatizo tunaogopa kuwajibishana. Tumesomewa hapa kwamba tuko kwenye *list* ya nchi ambazo zinapokea au kula rushwa, mimi sidhani kama ni sifa kwa Tanzania kuwa katika *list* hiyo. Ningefarijika kabisa kwamba Tanzania tusiwemo katika *list* hiyo ya wala rushwa. Hivyo tupige vita wote tushirikiane kwa pamoja tulishughulikie tatizo hili la rushwa ili nchi yetu iwe mfano wa kuigwa na nchi nyingine za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu utawala bora, mwezi uliopita tulikuwa kwenye chaguzi za marudio Kilimanjaro na haya tunayasema siyo kwamba tunazua au wazushi tulikuwepo na tumeona kwa macho yetu. Nimesikitika jana kuna Mbunge mmoja alichangia na kudai kwamba Vyama vya Upinzani wenyewe hatupendani na suala hili lilisemwa baada ya Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kupigwa kwenye kampeni. *(Makofi)*

Mimi sikatai hata kama kweli hatupendani lakini mhalifu ni mhalifu hata kama waliompiga Mheshimiwa Thomas Ngawaiya ni wa *TLP,* lakini sheria ingechukua mkondo wake kwani wanajulikana na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya aliripoti polisi na gari waliokuwa wanalitumia linajulikana na mmiliki wake anajulikana. Hii inatufanya tuamini kwamba kuna matabaka katika nchi hii. Wako Waheshimiwa wa Chama kingine wamepata matatizo kama haya wamevamiwa na vyombo vya dola vimefanya kazi yake na wale wahusika wamekamatwa. Kwa nini kwa Mheshimiwa Thomas Ngawaiya haya nayo yasifanyike? Wote sisi ni Watanzania na nchi hii ni nchi yetu wote. Tunaomba haki itendeke bila kubagua, maana kuwa kwenye Vyama vya Upinzani, si makosa, vyama vya upinzani viko kisheria na kama basi havihitajiki basi iletwe sheria hapa Bungeni vyama hivyo vifutwe. Tunasema haya kwa uchungu maana tulikuwa kwenye kampeni na tumeyaona yote yanayofanyika. Waheshimiwa wa Chama cha Mapinduzi, walidiriki hata kutumia magari ya umma.

**MBUNGE FULANI:** Mama yangu!

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Kwenye kampeni na mengine tumepiga picha na namba za gari tunazo na hapa ndipo pa kusemea na sisi ni Wabunge, tunayasema ndani ya Bunge hili na wananchi watusikie. Kama kweli tunataka uchaguzi wa huru na wa haki, basi tuhakikishe mambo haya hayafanyiki. Magari ya Serikali yaegeshwe tutumie magari yetu na tueleze sera zetu kwa wananchi bila kutumia ubabe, bila kutumia vyombo vya dola. *(MakofiKicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwenye mikutano ya viongozi wa Vyama vya Upinzani, ulinzi unakuwa mkubwa kuliko inavyotegemewa sijui kuna tatizo gani. Nategemea kabisa ulinzi huu ungeimarishwa kwenye benki zetu wizi unaotokea usingetokea. Tunaomba vyombo husika ulinzi huu uelekezwe kule kwenye fedha za

wananchi zilindwe ili majambazi wasiweze kupora pesa hizo. Nasi viongozi wa siasa ambao ni Watanzania na wote tunapenda amani. *(Makofi)*

Nilisema mimi sina mengi kwa kuwa mimi ni mmoja wa wana kamati waliopitia bajeti hii, haya niliyosema ndiyo yaliyonikera na ninaomba kukushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ni chaguo lako Mheshimiwa Teddy Kasella - Bantu kama dakika 10 zinakutosha unaweza kuanza, kama hazikutosha basi usubiri mchana, chaguo ni lako.

**MHE. TEDDY L. KASELLA - BANTU:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchana.

**SPIKA:** Haya. Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kwa mchangiaji mwingine kukamilisha hotuba yake sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni .

*(Saa 06.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba waliopata wa kufiwa na baba yao mzazi. Namwombea kheri na baraka aweze kupumzika kwa amani huko mbinguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kutoa pole kwa Wabunge wote waliopata ajali mbalimbali wakati wakija huku na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa wote wako katika hali nzuri ila mmoja ambaye yuko hospitali na tunamwombea aweze kupona haraka na kuungana pamoja na sisi hapa, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa aina ya pekee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuonyesha kwamba ni Waziri Mkuu wa sisi wote hasa leo alipopita mlango wa kushoto wa mkono wako. Ni kwa sababu sisi wote ni wapigakura wake kwa sehemu mbili na anatakiwa kutuonyesha kwamba sisi ni watu wake wote bila kujali itikadi na Chama tulichoingilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba basi kwa sababu yeye ni kiongozi wa Serikali wale Mawaziri wa miamvuli walioko chini yake wafuate utamaduni huo ili tuweze kuondoa itikadi katika Chama ambacho kimekuingiza katika Bunge, kwa sababu kuna *three pillars,* kuna Bunge, Serikali ambayo ni *Executive* na Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, akionyesha mfano huo, ni wa kuigwa na Mawaziri wengine. Naomba nizungumze sasa masuala fulani fulani kuhusu chama changu nikiwa kama Katibu Mkuu wa Chama na Mbunge pekee mwanamke, katika wadhifa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *whether* ukubali au usikubali mimi *size* yangu Ndugu Phillip Mangula. Kwa kukumbushana tu, Chama kilichotutawala ambacho ni *TANU* mwaka 1968 kilifukuza Wabunge wake wengi na wachache nitawataja hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, alifukuzwa Marehemu Choga, alifukuzwa Marehemu Stephen Kibuga, ambaye alikuwa Makamu Mwenyekiti wetu wa *UDP* tulipoanza *UDP.* Alifukuzwa Mheshimiwa Anangisye, Mheshimiwa Mwakitwange na Mheshimiwa Dr. Masha ambaye sasa hivi ni Makamu Mwenyekiti wetu pamoja na Marehemu Baba yangu Joseph Kasella-Bantu, pamoja na kwamba alikuwa mwasisi wa *TANU,* lakini alifukuzwa kwenye Mkutano wa *NEC* kule Tanga na hawakujali kwamba wale ni Wabunge wamepigiwa kura na wananchi, ni Ubunge wao walifukuzwa, walikuwa Wabunge kuanzia mwaka 1965 na wamalize mwaka 1970, lakini walifukuzwa.

Kwa hiyo, katika kukumbushana tu, siyo ajabu sisi *UDP* kuwafukuza Wabunge kwa sababu ni historia na tunafuata nyayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alifukuzwa Rais wa Zanzibar, Ndugu Abdu Jumbe mwaka 1972 na Urais wake wa nchi, lakini alifukuzwa na akakosa Urais na Umakamu Mwenyekiti. Hiyo ni kuwekana sawa tu.

Mwaka 1977 tuliungana *TANU* na *Afro-Shiraz Party* tukaunda CCM na baadaye mwaka 1978 walifukuzwa Wabunge wengine na Mawaziri nikiwataja wachache, Maalim Seif Sharif Hamad ambaye ni Katibu Mkuu wa *CUF* sasa, Mzee Mloo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ambaye sasa hivi ni Mbunge wa Kuteuliwa na Rais kutokana na muafaka.

**MBUNGE FULANI:** Alaa!

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haya, siyo kioja sisi *UDP* kufukuza kwa sababu tunafuata nyayo kutokana na chama kikongwe kilichotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie sasa katika mjadala wenyewe. Usalama wa raia kwa ajili ya mali zetu na sisi wenyewe. Sioni aibu mimi na ningependa wanachama wangu walioko Bariadi wasione aibu kwamba tumeshindwa na tumekiri kwamba tumeshindwa pamoja na vurugu zote na kutumia dola na dunia nzima ilikuwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko wastaarabu tunakubali kushindwa. Tunakubali kushindwa ili yaishe, lakini sasa tulivyoshindwa sisi sio tuonekane tena kwamba sisi ni malegelege.

**MBUNGE FULANI:** Mabwege!

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mabwege, palikuwa na kazi ngumu kule, ilikuwa ngoma nzito, wanajua wenyewe. Wale ambao hawakula ugali kwenye chungu kile, hawajui tulivyokuwa tunafinyana kule ndani ya chungu. Hivyo tuheshimiane, sio kudharauliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina furaha na ninatembea kifua mbele kwamba tulikuwa na msimamo na kwamba Chama bado kiko hai na bado watu wanatupenda na wana msimamo ule ule kwa hiyo, nawapongeza sana wote kwa ajili ya moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchaguzi huu wa Bariadi kuanzia katika Kata ya Nkomo, watu walipigwa sana na kuna binti mmoja Christina, yeye alipigwa mpaka mimba yake ikatoka. Nikaja nikazungumza hapa ndani ya Bunge, nikaenda nikazungumza kwenye *television* lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa eti kwa sababu tu ni Mwenyekiti wa UDP.

Lakini haki ni haki, mtu kama akimpiga mwenzake na mimba ikatoka, hatujui yule mtoto alikuwa Rais au alikuwa nani. Kwa hiyo, haya masuala yawe yanatazamwa pande zote kwa ajili ya usalama wetu. Awe wa CCM, wa UDP, wa CHADEMA au wa CUF akifanya kinyume na kuleta vurugu hatua zichukuliwe za Sheria, siyo ziwe upande mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyokupa kura yangu ukawa Waziri Mkuu wa Bunge hili basi shughulikia hii ili tutendewe haki sisi wote bila kujali itikadi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuja hapa, tukaitwa wadau wote wa Vyama vyote, Wenyeviti na Makatibu Wakuu wa Vyama vyote vya Siasa hapa wakati wa kumalizia Bunge la mwezi Aprili, cha kusikitisha, tulipendekeza pamoja na Mjumbe wa CCM ambaye alikuwa ni Mzee Paul Sozigwa, siku hiyo. Mimi mwenyewe aliniacha na hoi, sikuamini masikio yangu na macho kama tunakubaliana sisi wote. Lakini nikajua sasa tunaanza kuelewa demokrasia maana yake nini, Utaifa maana yake nini. Sisi wote tunataka nchi hii iwe na amani na ilete maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kujali itikadi zetu kwamba wagombea wa Vitongoji na Vijiji wawe *Private Candidates* wasiwe na itikadi yoyote kwa sababu kule chini tunataka maendeleo, hatutaki utawala wa kisiasa. Kwa hiyo, maendeleo yanakuja bila kujali itikadi ni lazima watu wenyewe wawe hawana itikadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana sisi wote na tuka-*sign* mimi *copy* ninayo, tukasaini sisi wote kwamba tuache Vijiji na Vitongoji vyote vikae, zigombewe na watu ambao hawana siasa ya itikadi ya aina yoyote wanaotaka maendeleo kule na tulijua

kwamba wako wengi *retired officers* wanaorudi kijijini na wanaweza kusaidia sana maendeleo ya kule kijijini kufuatana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana vile vile Daftari la Wapiga kura, tusifanye uchaguzi huu mpaka daftari liwe tayari na tukaambiwa kwamba daftari hili litakuwa tayari mwezi Januari, 2005. Sasa cha kushangaza ni kwamba pamoja na kutuleta sisi tukae hapa, sisi viongozi ambao ni wadau wote na kulipwa *per diem* pale hakuna kilichochukuliwa na sisi tulipitisha maazimio na tukasaini wote bila kubaguana hata wa CCM naweza nikatoa barua ile tuliyosaini kama maazimio ya siku hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumza vile vile juu ya Tume Huru ya Uchaguzi na hili tulizungumza kwa sababu kule Zanzibar wamepata Tume Huru ya Uchaguzi. Lakini huku kwetu mimi sioni aibu kusema Tanganyika, kwa sababu Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na watu lazima wajue hiyo, ndiyo tunapata Tanzania.

Kwa hiyo, tulikubaliana kabisa na sisi tuwe na Tume Huru huku ili uchaguzi wetu wa Wabunge ambao wanaingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wote tuchaguane katika utaratibu unaoeleweka wa sawa, siyo kungoja mpaka tuuane kama walivyouana kule Pemba kuleta muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejifunza kwa hiyo naomba, tuko mahodari sana katika kusuluhisha kwa hiyo na sisi tujisuluhishe wenyewe. Tusifike mahali ambapo tunaweza kuleta hatari. Tupate Tume Huru ili tuingie wote kwa amani katika uchaguzi huu, katika Bunge hili kwa usawa na utaratibu unaokubalika. Tusiwe na Tume Huru Zanzibar na huku kwetu hatuna Tume Huru. Hakuna sababu.

Mhesihmiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nasisitiza hilo tuwe na Tume Huru kabla ya Uchaguzi ili wote tuingie, tushinde, tushindwe lakini tuwe na Tume Huru wote pamoja. Kwa sababu tunaingia katika Bunge moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida yetu huwa tunatoa ushauri mara ya kwanza na Serikali inatekeleza na ikitekeleza tunaweka vema. Wakati alipokuwa anagombea Urais mwaka 2000 Mheshimiwa John Cheyo tulizunguka nchi nzima, tukazungumza, tukasema tukipata Urais, tutatoa elimu bure na afya bure. Watu wakatuambia aah, mtapata wapi pesa ninyi. Tukasema pesa zipo ndani ya dumu, tutalipasua na zitapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kweli tumeingia hapa, elimu imeshatolewa bure kwa shule ya msingi. Lakini sisi tulikuwa tunataka mpaka sekondari na sasa hivi tunakwenda kwenye sekondari. Kwa hiyo, hapo napenda kuipongeza Serikali na kuipa vema. Hakuna sababu ya kubisha kwa sababu ni kweli ni sera yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naongeza tena ushauri mwingine, asililimia mia moja ya wanafunzi waende *secondary school* na jinsi ya kufanya ni kujenga darasa moja moja kila mwaka. Mwaka huu lijengwe darasa la *Form One,* mwaka kesho na mwaka

kesho kutwa lijengwe la *Form Two* na *Form Three* na kuendelea. Kwa hiyo, madarasa tutapata kufuatana na mwaka unavyofuata na nyumba za walimu wanakijiji watajenga kila mwaka kwa darasa na nyumba za walimu kula mwaka. Halafu vile vile Serikali itoe mabati kama inavyotoa kwenye MMEM. Kwa hiyo, tutakuwa tumeshapata *secondary school* kwa ajili ya wanafunzi wote na wote watapata haki. Vile vile wakimaliza hapo wataendelea *Form Five* na *Form Six* kwa wanaojiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu utaniambia kwamba kuna walimu. Walimu watatoka kwa wanafunzi wanaotoka *University* wote wapewe *compulsory* kufundisha *Primary School* na *Secondary School* kwa miaka mitatu kama Cuba ilivyo. Kwa hiyo, tutakuwa tumepata walimu wa kutosha na tutazuia vijana wetu ku-*hang,* watapata ajira na mikopo yao wanayopata ya kusoma watalipa kutokana na mishahara wanayopata, umaskini utatoka. Wapiga debe wasomi watapatikana wazuri kwa sababu wana elimu na vile vile wanafunzi wanaomaliza darasa la 12 watakuwa vijana wakubwa wa miaka 17, 18 na 19 na kuendelea na hivyo wanaweza kujitegemea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tumemaliza suala la ajira na vijana wazururaji. Likipatikana hili na likitendeka, sina sababu ya kubisha, nitaweka vema. Tutakuwa tumeshaondoa umaskini, ukiangalia nchi zingine kama Mauritius wana miwa na utalii tu peke yake na ni matajiri na sisi tuna miwa, utalii, pamba na tuna kila kitu, hakuna sababu ya kuwa maskini. Kwa hiyo, naomba tufuate mifano ya Mauritius, tulime miwa yetu, tufanye utalii wetu, tulime pamba ya kutosha na tuuze tupate mapesa kibau.

Mheshimiwa Naibu Spika, njaa itaondoka kwa sababu maji yako mengi sana. Tuna Mito mingi sana na Maziwa mengi sana kila kona na ukipita wakati mwingine wakati wa mvua maji yanatiririka hovyo. Hakuna anayefikiria kuya-*save* yale maji. Hakuna mtu anayefikiria ku-*harvest* maji katika nyumba zake.

Tukilima na kukifanya kilimo cha umwagiliaji naamini hatutakuwa na njaa na hatuna sababu ya kuwa na njaa. Kwa hiyo, hayo yote tutakimbiza umaskini kabisa na tutajaa mapesa kibao. *(Kicheko)*

Naomba nimalizie Kiswahili. Kiswahili ni lugha ya Taifa. Lakini hatuithamini hii lugha ya Taifa. Lakini unakwenda kama nchi ya China au Japan, unafika pale Mawaziri au Wabunge na watu wote wakubwa/viongozi, wanazungumza Kichina halafu kuna mkalimani anazungumza na kueleza kwa Kiingereza, wanajua Kiingereza. Lakini wanataka kuwa *proud* na lugha yao, pia Kijapan wakina Mkalimani, anazungumza Kiingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba na sisi tuwe *proud* na Kiswahili ili tuweze kuzungumza na vile vile tuta-create jobs kwa wakarimani ambao wanaweza kuzungumza lugha zingine wakifanya hivyo wakati wao wana-translate na hali na sisi tunajua Kiingereza ni mgawanyo wa kazi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutafanya ajira tena kwa wakalimani wetu na hivyo kuongeza upungufu wa kazi. Sitaki nigongewe kengele ya pili lakini nakushukuru

na naomba tukubaliane tuwe Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika *style* ya kuingia wote sawasawa na kuheshimiana, kama tulivyo watani sasa hivi CCM na *UDP*. Tuko watani wa jadi sasa. Tunaheshimiana kama vile Mnyamwezi alivyokuwa anamheshimu Mhehe kwa sababu walikuwa *heroes* wote na sisi tuko *heroes,* hakuna kutunyanyasa kwa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J.R. IWVATTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie. Lakini kabla sijafanya hivyo, naomba niungane na wenzangu waliotangulia kuzungumza kwa kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba uliowapata kwa kufiwa na baba yao mpendwa. *Inshallah* Mwenyezi Mungu aiweke roho yake Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba niungane na wenzangu niwape pole Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali hususan Mheshimiwa Mama Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa kupata ajali wakati wakija katika Bunge hapa na mwisho naomba nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, yeye pamoja na Madiwani wenzake waliogombea kwa tiketi ya CCM na hatimaye kuweza kupata ushindi wa kishindo. Nampongeza sana na tunamkaribisha Bungeni. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imeeleza mambo yote kiwazi wazi. Kwa kweli mimi napenda kusema tokea awali kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa nilikuwa naomba tu nizungumzie suala moja ambalo katika eneo langu la uchaguzi kwa kweli ni kero. Limekuwa likileta usumbufu na wakati mwingine likitishia amani. Nina imani kubwa kwamba Serikali hili tatizo italishughulikia. Lakini huko tuliko watu hawana uhakika litakwisha lini kwa sababu linaleta usumbufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu la Uchaguzi tuna mgogoro na majirani zangu Wilaya ya Sikonge tuna mgogoro wa mpaka, kuna kijiji kinachogombewa. Sisi wa Manyoni tunasema cha kwetu na wenzetu wa Tabora wanasema ni cha kwao na imekwenda hivyo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufumbuzi wa tatizo hili mimi naona si mkubwa sana, iwapo kama Serikali itaamua tu kukubali kutukutanisha pande mbili zinazohusika kwa maana ya Viongozi na wananchi wa upande wa Sikonge na Manyoni tukasaidiwa kuonyeshwa kwamba mpaka kati yenu ninyi Manyoni na Sikonge unapita hapa na baada ya kufanya hivyo, kama Serikali itaweka mawe ya mpaka kubainisha mpaka kati ya Sikonge na Manyoni ninaamini kabisa kwamba hilo litakuwa limemaliza matatizo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwa likileta matatizo kidogo. Nakumbuka mwaka 2001 tuliitwa mimi na Mheshimiwa Said Nkumba kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tukaelezwa juu ya matatizo ya mpaka. Ilikuwa tarehe 20 Juni, tulipokwenda pale wenzetu wa Tabora walikuwa wanadai vijiji vitatu vya Wilaya ya Manyoni na hivyo vijiji ilikuwa ni Makare, Mitundu na Kalangale.

Baada ya kufika pale Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alianza kumwuliza mwenzangu Mheshimiwa Said Nkumba, akamwambia bwana, hebu tuambie bwana hivi vijiji wewe unavifahamu? Kwa kauli yake akasema kwamba hivi vijiji mimi sivifahamu wala sikupigiwa kura na baadaye aliniuliza mimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikamwambia hivi ni vijiji ni vyangu na nimekuwa nikipigiwa kura toka mwaka 1990. Sasa kwa sababu mwenzangu alikubali kwamba haviko kwake na mimi nikakubali kwamba vilikuwa kwangu na hatukuwa na ubishi. Mimi nilitegemea kwamba hilo tatizo lingeisha. Sasa baada ya hicho kikao iliandikwa barua tarehe 20 Oktoba, 2001. Namba zake ni *RALG-C/D.70/S.PART A/42* na nyingine iliandikwa 15 Novemba, 2001 na Namba ya barua hiyo ni *RALG-C/D.70/6/5* ya 15 Novemba, 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi barua kimsingi zilikuwa zinabainisha kwamba tatizo la mpaka lilikuwa linaletwa na Tangazo la Serikali Na. 349 lililokuwa linaunda eneo la utawala katika Wilaya ya Sikonge na Gazeti Na. 260 ambalo lilikuwa linaunda Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge katika hayo maeneo. Sasa *GN. No.249* ndiyo ilikuwa inamega vijiji vya Wilaya ya Manyoni kwenda katika Wilaya ya Sikonge. Lakini kimsingi barua zote hizo mbili zinaeleza kwamba mpaka kati ya Wilaya ya Manyoni na Sikonge kwa sababu ulikuwa unatokana na mpaka wa Mikoa ya Tabora na Singida ambayo zamani ilikuwa *Central Province* na *Western Province.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo barua zilikuwa zinasema kwamba huo mpaka kimsingi haujabadilika, upo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 27 la mwaka 1961 lilikuwa halijabadilika. Sasa baada ya hiyo barua maelezo mengine yalikuwa yanafuata ni kwamba katika ile barua ya tarehe 15 Novemba, 2001 hiyo barua kati ya mambo yaliyoandikwa humu miongoni mwao ilikuwa inawaeleza wenzetu wa Wilaya ya Sikonge waache kukusanya ushuru kutoka katika hivyo Vijijiji ambavyo viko Manyoni na sisi watu wa Wilaya ya Manyoni tukaambiwa tuendelee kutoa huduma katika hivyo vijiji na hizi barua zote mbili zilikuwa zimeandikwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Baada ya hizo barua na ule mkutano ambao tulikuwa tumefanya, mimi nilitegemea kwamba haya mambo yangeisha na ilikuwa ukienda ziara watu wanakuuliza mbona kuna matatizo ya mpaka? Tunawaambia jamani, kuweni na subira. Serikali inalishughulikia hili tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mwezi wa saba, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wakati anawasilisha hotuba yake ya Bajeti akatoa tamko katika ukurasa Na. 11 Ibara ya 25. Naomba kwa ruksa yako

nisome sentensi mbili za mwisho zinavyosema. Zinasema: “Mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya Manyoni na Sikonge umetatuliwa kwa kuhakiki maeneo ya mipaka na kubaini kuwa hapakuwepo na tatizo la mpaka. Hivyo kijiji cha Kalangali kilichodaiwa kuwa kipo katika Wilaya ya Manyoni kitaendelea kuwa katika Wilaya ya Sikonge.”

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi sikuwepo, nilikuwa nimesafiri na Wanakamati wenzangu. Niliporudi Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge kwa mapenzi tu kwa sababu ni ndugu yangu, jirani yangu. Akaniambia bwana Mheshimiwa Waziri, aliniandikia ki-*memo* akaniambia, Bwana Mheshimiwa Waziri ameandika kwamba kile kijiji cha Kalangali badala ya kuwa Manyoni sasa kipo Sikonge. Akaniuliza kiko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii ikawa pia inaleta hali ya utatanishi, kama kipo Sikonge mimi naamini kabisa kwamba Mheshimiwa Said Nkumba alipaswa kukijua. Mimi nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tarehe 22 Julai, nikamwambia aangalie upya na nikamwambia kwamba hiki kijiji toka zamani kipo Wilaya ya Manyoni, kina uongozi wa Serikali ya Kijiji uliopatikana kwa kusimamiwa na uongozi wa Wilaya na Mkoa wa Singida na nikamwambia kwamba hiki kijiji kimeandikishwa katika Mkoa wa Singida na namba zake ni *SI/KIJ/365.* Hati ya tarehe 8 Septemba, 1993 na nikamwelezea juu ya zile barua kwamba zilishatoa uamuzi kwamba hiki kijiji kiko Manyoni, imekuwaje tena uamuzi unabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia au nikamwomba nikasema njia ya pekee ya kumaliza hili tatizo ni kutukutanisha viongozi na wananchi wa Wilaya hizi mbili kisha tuweze kuonyeshwa mpaka. Suala la kudai kwamba hiki kijiji kiko Manyoni ama kiko Tabora kabla hatujaonyeshwa mpaka nafikiri itakuwa si sahihi.

Sasa ni muda mrefu toka nimeomba, sasa kwa sababu wananchi mpaka sasa hawako katika hali ya utulivu kutokana na hii ya mpaka kutoeleweka, ndiyo nilikuwa namwomba sana sana, nilikuwa naiomba sana Serikali ijaribu kushughulikia hili tatizo na hii barua niliyoandika bahati nzuri nilimpa nakala Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimpa nakala pia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi na nikampa nakala Mheshimiwa Mkuu wangu wa Mkoa, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na viongozi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa maelezo haya ya Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba hiki kijiji kitaendelea kuwa Sikonge. Hivi mimi nikiuliza swali niseme kama kitaendelea kuwa Sikonge lakini leo kipo Manyoni, tumejenga shule na ukifika pale unakuta mabango yameandikwa Shule ya Msingi Kalangali, Manyoni. Kilitokea nini hiki kijiji kikatoka Sikonge au Tabora kikaja Manyoni na wakati kinahama toka huko kilihama kwa utaratibu gani kama leo tunakigombea kilihama kwa utaratibu gani na kama wenzetu hawakuridhika wakati kinatoka Tabora kuja Manyoni walichukua hatua gani? Je, Wizara ina malalamiko yoyote kwamba wenzetu wa Tabora wamenyang’anywa kijiji na watu wa Manyoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mimi yalikuwa ni maswali ambayo naomba niyaulize na nipate majibu na mwisho mimi naamini kabisa kwamba Serikali isingependelea kuona kwamba siku moja watu wanagombana kwa sababu tu ya kugombea kijiji. Kwa sababu nchi yetu ni ya amani, mimi naamini kwamba Serikali itashughulikia hili. Lakini nilikuwa naiomba basi iharakishe hili zoezi la kuonyesha mpaka. Vinginevyo wenzetu wamekuwa hawana imani na hasa wenzetu baada ya kusikia kwamba Waziri amesema kwamba kile kijiji kiko Tabora, wenzetu wale wa kijiji cha pili au ule uongozi wa Kata ya Kipili umekuwa wakitumia nguvu kuingia hata katika maeneo mengine kwa kisingizio tu kwamba hiki kijiji, Waziri ameshatamka kwamba kiko Tabora.

Sasa mimi nilikuwa naiomba sana Serikali ifanye kila lnalowezekana tukaonyeshwa huu mpaka mapema iwezekanavyo ili kulinda hali ya amani kwamba isije ikatokea siku moja watu wakagombana bila sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nikatoa mchango mdogo lakini narudia kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe maoni yangu kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza ningeomba tu na mimi niungane na wenzangu kwa kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa tatizo lililowapata la kufiwa na mzazi wao. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kushinda na kuwa Mbunge tena ila safari hii kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni hotuba nzuri, imenifurahisha, ni pana, ina kina, imegusa maeneo yote ambayo ni ya msingi ila nitachangia yale ambayo napenda yaongezewe ili nami yanihusu na kutatua matatizo kufuatana na eneo ninalotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa juhudi aliyoifanya kwenda Geita na kutatua tatizo la siku nyingi la wakazi wa Geita kuhusiana na dhuluma ya fidia ya maeneo yao wakati mgodi ukitolewa. Nampongeza na namwomba sana awe na juhudi hiyo, asirudi nyuma kwa sababu kuna maeneo mengi tutamuomba aingilie kwa sababu yeye ndio kinara wa katikati, aingie katikati, atatue matatizo haya ili pale panapokuwa na ucheleweshaji, mgogoro, uzembe, naomba sana awe na juhudi na moyo huo wa kuingia katikati haraka na kusaidia kutatua matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianzie na suala hili la madini, katika ukurasa wa 21 suala la uchimbaji na migodi ya madini limejadiliwa na pia imesemwa wazi kwamba kuna hii Tume ambayo inazunguka na kuangalia kero ili ipatikane suluhu na uamuzi wa pamoja kuhusiana na masuala haya. Kitu ambacho naomba kieleweke hapa ili watu walio katika maeneo haya nao pia waone tuko pamoja nao, unapozungumza na watu

wa Geita, Nzega kitu cha kwanza ambacho bado wanauliza kwa karibu ni nini Halmashauri zao zipate kwa namna ya mrabaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tunalisema waziwazi kwa sababu limeshatekelezwa hapa hapa nchini kwa watu wengine. Tunapoona watu wa maeneo ya Ngorongoro wanapata mrabaha kutokana na mbuga za wanyama, tunapoona watu wa Kilimanjaro wanapata mrahaba kutokana na Mlima Kilimanjaro kwa kweli hili jambo hatuwezi kuacha kulizungumzia litakuwa linarudiwarudiwa mpaka uamuzi na taratibu sahihi zifanyike ambazo zitaturidhisha wote tuonekane kwamba tuko sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba suala la mrahaba sasa uliingilie kati, kipindi kimefika, ulitolee uamuzi. Hatuoni sababu sijui ni uchoyo, ubaguzi mimi sielewi kwa sababu wengine wanapata, wengine wanaambiwa hapana. Naomba sasa jambo hili liingiliwe kati, liamuliwe mara ya mwisho ili tuweze kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika utaratibu huo huo, watu wa maeneo hayo, wanapenda kujua Sheria ya Madini kumruhusu Kamishna awe na madaraka peke yake kuamua nani akachimbe wapi, yeye ndiye anagawa eneo bila kuwahusisha watu wa eneo hilo, ndio moja ya maeneo ambayo yanazalisha sana matatizo na migogoro kati ya wachimbaji na wananchi wa maeneo hayo.

Sasa sheria hii imefikia wakati wake iangaliwe kwa karibu kwa sababu kama ingefanyika hivyo, nina imani watu waliokwenda kuchimba Geita wangeonana na wananchi wa Geita, waliokwenda kuchimba Nzega wangeonana na wananchi wa Nzega, waliokwenda kuchimba Mwadui wangeonana na wananchi wa Mwadui ili wawekeane makubaliano na labda hata tatizo hili lisingekuwa limejitokeza. Kwa hiyo, naomba sana sheria hii iletwe Bungeni, iangaliwe upya, ili tuoanishe hali hii isije ikawa inaleta migogoro hii na wananchi wapewe haki yao ya kuamua, kwa nini wanyimwe haki ya kuamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kuhusiana na madini ni suala la hawa wanaochukua migodi hiyo, tuwe nao na tufanye kazi pamoja na njia ya kufanya hivi ni namna gani watuuzie hisa katika maeneo hayo, sisi tununue hisa kama Watanzania, kama wananchi wa maeneo hayo. Nina imani watu wa Geita watanunua hisa kwenye migodi ya Geita, watu wa Mererani watanunua hisa kwenye migodi ya Mererani, watu wa Mwadui pia watafanya hivyo hivyo na watu wa Nzega watafanya hivyo hivyo.

Naomba suala hili lifanyiwe kazi na namna gani hisa hizi zinaweza kuuzwa kwenye *Dar es Salaam Stock of Exchange* na pia watumie njia nyingine kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanashiriki na wanashirikishwa ili tufanye kazi pamoja na hawa wenzetu kwa sababu na sisi tunahitaji maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la ubinafsishaji suala ambalo kwa kweli mpaka sasa bado linatuyumbisha na hoja nyingi zinajitokeza lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza vizuri. Kitu kimoja ambacho napenda kieleweke ni kwamba ubinafsishaji wetu hapa sisi kwa kiwango hicho cha mitaji hiyo na uwezo wa pesa

mkubwa huo unatuengua sisi wananchi. Hoja hii ya ubinafsishaji unapoizungumzia kwa Waingereza, Wajerumani, kazi watafanya wao ndani ya nchi yao sisi tunapata watu wa nje kuja kufanya kazi hapa ndani wananchi wetu hawana nafasi ya kushiriki katika ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Shirika letu la Ndege *(Air Tanzania)* tulilibinafsisha lakini tumelijadili sana hapa na kujaribu kuweka vigezo kwamba ikaeje ikiwa ni pamoja na kusema kwamba hata ile alama ya Twiga ibakie kwenye mkia wa ndege. Ndege imeandikwa *Air Tanzania* rangi yake nyeupe sijui inaashiria weupe lakini suala zima ni kwamba yule Twiga hayupo tena kwenye mkia wa ndege zaidi ya pale hata juzi nimepewa tiketi ya *Air Tanzania* lakini imeandikwa *South Africa.* Ukipita kwenye viwanja vya ndege kwenye maeneo ya *hangar* huoni ndege zikiingia kufanyiwa *service* wakati sisi tukiwa *Air Tanzania* tulikuwa na Wahandisi wa ngazi hizo sasa huduma hizo hazifanyiki pale, hawa watu ajira zao zimekwenda wapi? Haya ndio mambo ya msingi ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uyaangalie kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kamati za Bunge kwa mfano Kamati ya Biashara na Uwekezaji, ukiituma kwenda kuangalia ili ikuletee taarifa bila shaka itakuletea taarifa ambayo ni sahihi, haina upande, ya wazi na ya kina. Naomba jambo hili liangaliwe kwa karibu kwa sababu tunapofanya hivi tunaweza kujikuta tunajisahau hatua kwa hatua mwishoni tunafika mahali ambapo Shirika linapotea hivi hivi na tunajikuta tupo katika hali ngumu. Kwa hiyo, ufuatiliaji wa mashirika haya ufanyike kwa namna ya makubaliano ya kuyabinafsisha ili mkono wa Tanzania kama Serikali yetu ubaki kama mkono wa Tanzania ndani ya shirika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la Utawala Bora limeelezwa vizuri hapa na nia yetu kubwa ni kwamba watendaji wawasikilize wananchi na waelewe kwamba watendaji wanawafanyia kazi ya wananchi. Matatizo haya yamezuka sehemu nyingi na katika maeneo hayo tuna matatizo ambayo yanasababishwa na uzembe, kutojali, kutomsikiliza mwananchi kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano jambo hili ambalo tunalirudia kama mfano suala la namna gani akinamama hasa katika kipindi cha kujifungua anapokwenda hospitali wale wakunga hawamjali, wanamjibu vibaya na wanamwambia maneno mengine ya kejeli kwamba kwani mimi nilikulazimisha. Sasa ile haihusiani na jambo lenyewe anachopaswa yeye kufanya ni kumpokea yule na kumwelekeza cha kufanya. Sasa umahiri huu wa Serikali ndio tunaotaka uingie ndani ya watendaji katika Serikali yetu hii. Serikali sasa inafanya mambo mengi makubwa yanaeleweka, imefanya vizuri kwenye elimu, barabara na kwenye nyanja zote na tunaona mtu ambaye anakataa anakataa kwa makusudi lakini inaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili napenda kusema kwamba ugumu huu na kasoro hizi katika eneo langu kama Mwanza Mjini kuna suala lililoletwa na watu wa *TANESCO,* ofisi ya *TANESCO* imewaandikia wananchi na kuwaambia kwamba maeneo fulani fulani waondoke ili waache nafasi kwa ajili ya nyaya za umeme ambazo ni za nguvu ya juu. Katika hilo wenyewe wamekwenda mbali zaidi na kusema kwamba kama

watu hawa hawatabomoa nyumba zile basi *TANESCO* wenyewe watakwenda kubomoa nyumba zile. Hii ni makosa, *TANESCO* hawana uwezo wa kwenda kubomoa nyumba ya mtu, huu ni uzembe wa utendaji kwa sababu kanuni na taratibu zinaeleweka wanapaswa wawasiliane na Halmashauri ya Jiji, Halmashauri ya Jiji ndio imegawa viwanja vile, inajua fulani anakaa sehemu gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wangejitoa katika suala hili kwa sababu limewababaisha, wananchi wanajaribu kuandikia kila mtu wapate msaada hawaelewi nani awasaidie. Wameandika barua kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Polisi bahati nzuri na mimi wamenipa nakala, ninazo hapa nyingi sana huku ni kubabaisha watu taratibu na kanuni zinaeleweka.

Naomba *TANESCO* wajiondoe kwenye suala hili, wafuate taratibu naona wanachotaka kukwepa hapa ni kulipa fidia, *actually* ni kumwonea mwananchi, inapaswa walipe fidia kama wanataka kutumia eneo hili na wafuate taratibu na kanuni za nchi zilivyo *TANESCO* hawana haki kusema wanakuja kubomoa nyumba za watu, hizo taratibu hatuna hapa. Naomba Waziri Mkuu ulielewe ili hizi taasisi za maeneo ambayo yanakwenda kinyume cha utaratibu basi uingilie kati ututatulie matatizo ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo inaelekea kujitokeza ambalo tumejaribu kulizungumzia na kuliweka sawa lakini naona linajitokeza kwa sura nyingine malalamiko ya wananchi yanatokana na kutosikilizwa katika sehemu zile ambako wanapaswa kusikilizwa na watendaji, sasa wanaanza kuhangaika wengine wanaandika hata magazetini. Kuna gazeti limeandika hapa kuhusiana na ugumu na taratibu mbaya za kugawa viwanja katika eneo la Ibanda, Jijini Mwanza hii sio sawa kwa kweli. Wakurugenzi wanapaswa kuelewa kwamba wananchi ndio wanapaswa kuwatumikia na wawasikilize kwa karibu, wawaelewe na waweze kufanya yale ambayo wananchi wamejaribu kuyaleta kwao kama hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hizi wanaandika kwa kila mtu wanahangaika, hawajui waanzie wapi na katika kanuni na taratibu za utawala bora tunataka ziendane na Sera za Chama cha Mapinduzi, ziendane na mwelekeo ambao Chama cha Mapinduzi kinaipa Serikali, zifanye kama tunakotaka kwenda kama Serikali ni ya utendaji bora.

Naomba sasa haya yaanze kufanyiwa kazi kwa karibu na hawa wanaokwenda kinyume waanze kukamatwa mmoja mmoja hata kama ni kufukuzwa kazi wafukuzwe ili watu wapate nafuu, hii ni shida kubwa. Watu wanakaa na wasiwasi kwenye eneo lao kwa nini na watumishi wameajiriwa pale kufanya kazi hiyo kama mtu anaona hawezi kufanya kazi ile vizuri aondoke mapema apatikane mtu mwingine ili huyo mtu mwingine afanye kazi ya wananchi na wananchi waridhike na lile linalofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya nayasema kama mfano hai kabisa watu wanalalamika na utawala bora ambao tunaujenga hatutaki mtu alalamike kwa namna hii. Wanatafuta kila mahali kumwambia kila mtu wakati ofisi inayohusika iko karibu pale kwa nini ofisi hiyo isishiriki kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipongeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa mpangilio ule walioufanya wa namna ya kuondoa vile vizibo ambavyo vilikuwa vimewekwa kati ya nyumba na nyumba. Wamefuata kanuni sawasawa, wakawaarifu watu, wakaanza kutekeleza na taasisi inayohusika kama Halmashauri ndio ilifanya kazi zile sasa hapa *TANESCO* inataka kufanya kazi ambayo siyo yao kinyume kabisa na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili likomeshwe mara moja ili mtu mwingine asirudie likatuharibia tulikofika maana tumefika mbali kazi yetu ni nzuri na vitendo vinaonekana, wananchi wameanza kuwa na imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nasema, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa wote ambao wamepata matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi mkubwa alioupata. Huo ni ushindi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla wake, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ilizofanya wakati inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000-2005. Kazi nzuri imefanyika nchi nzima lakini Jimboni kwangu yako mambo mengi ambayo yamefanyika kama vile elimu, barabara na sasa hivi tumeingizwa kwenye mpango wa maji wa Benki ya Dunia, *TASAF,* umeme Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuja kuuzindua na nimewasiliana na watu wa *Celtel* hivi karibuni wanakwenda kuweka mitambo. Ukiona mambo mengi ya namna hii yamefanywa na Serikali lazima uipongeze Serikali iliyoko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya kusifia ni mengi na nikiendelea kuyasifia yatanipotezea muda wangu kwa sababu yanaeleweka na wananchi wanayaona. Kazi yangu nikisimama hapa ni kuishauri Serikali na ndio kazi ambayo nimekuja hapa kuifanya hili la kusifia kazi zilizofanywa nafanya huko vijijini hapa ni kuishauri Serikali itekeleze wajibu wake ipasavyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu Wapinzani napenda mlielewe hili kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanapoishauri Serikali msidandie hizo sio hoja zenu wanaishauri Serikali ipate meno zaidi ya kutekeleza wajibu wake, sio hoja zenu hizo ni hoja za Wabunge wa CCM wanatekeleza wajibu wao. Sasa ukimwona Mbunge wa CCM anaishauri Serikali unasema anaiponda Serikali inaonekana wewe hujui siasa rudi darasani ukajifunze siasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo machache ya kuchangia, nianze na hotuba hii ya Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, hotuba ambayo imechukua sifa kwamba ni hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Yaliyomo humu nilikuwa nayaangalia, sikutegemea Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kuwa na maneno kama haya ya mbuzi kwenye gunia, usione soo, sikuyategemea haya kwa sababu nimeyaona aah, naendelea kuwapa pole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile inanikumbusha hadithi moja, kulikuwa na Daktari mmoja ambaye alipewa vijana fulani ambao walikuwa wana matatizo kidogo awatibu. Amewatibu siku moja akataka kuona kama matibabu yake yamefanikiwa au namna gani. Akafunga mlango akachora ukuta mkubwa sana akaweka na komeo la kuchora mlango umefungwa unaonekana, akawaambia haya hebu fungueni mlango mtoke.

Mmojawapo akatoka akaenda pale kwenye mlango uliochorwa ameacha huu mlango kaenda kwenye mlango uliochorwa anang'ang'ana na ukuta pale ili afungue, atoke, mwingine alikuwa anacheka sana, Daktari akafikiri kwamba huyu inawezekana amejua mlango ulipo. Akamwambia bwana hebu rudi wewe vipi mbona unacheka sana? Akamwambia mimi nacheka sana huyu bwana anakwenda kufungua mlango funguo ameacha kwangu. Akajua kabisa kwamba hawa wanahitaji kuendelea na matibabu. Haya ndio mambo ambayo Watanzania wanatakiwa wayaone wenzetu bado kushika madaraka ya kuongoza nchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kidogo suala la rushwa. Rushwa haipo tu kwa sababu CCM inatawala, hiki ni kitu cha kihistoria kipo na sisi wana CCM, viongozi wa Vyama vya Upinzani wa kisiasa na Watanzania wote lazima tuikemee rushwa mahali popote pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndani ya CCM tuna utaratibu mzuri sana na mfano mzuri ni wa mwaka 2000 baadhi ya watu walioonyeshaonyesha harufu ya rushwa waliondolewa, hawakushiriki kwenye uchaguzi. Nawaomba na viongozi wa Vyama vya Siasa vya Upinzani waige mfano huu mzuri wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwepo wakati wa kutunga huu utaratibu wa takrima, lakini kwangu binafsi nauona ni kero. Naiomba Serikali ianze kuangalia utaratibu mpya wa kuondoa utaratibu huu kwa sababu unawachafua wanasiasa. Wengine hawatoi lakini kwa sababu neno takrima lipo linawachafua wote. Kwa nini wewe usubiri wakati wa uchaguzi ndio upike pilau, kwa nini usubiri wakati wa uchaguzi ugawe fedha kwenye bahasha kwa mradi gani hawa wananchi watakupa kama sio rushwa? Naomba Serikali iliangalie suala hili. Nimesema, nitasema kweli anayechukia achukie lakini ndio utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kidogo madai ya Walimu, inasikitisha sana. Tunazungumzia mpango wa MMEM, ni mpango mzuri sana lakini kama hujawawezesha hawa wanaofanya kazi ya kuwafundisha wanafunzi hawa,

unawaacha, Walimu wetu hapa wanaidai TAMISEMI zaidi ya shilingi bilioni 13, Serikali ipo? Wizara ya Elimu shilingi bilioni 4, Bima zilizokwishaiva Walimu wetu wanadai shilingi bilioni moja. Mheshimiwa Waziri Mkuu hii ni kero.

Naomba Serikali ichukue hatua za makusudi kumaliza tatizo hili. Hawa ni wapiga kura wetu, wanatusaidia mambo chungu nzima katika masuala ya Kitaifa, kwa nini sisi hatuwawezeshi kupata maslahi yao ambayo yako kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazo taarifa kwamba wako Walimu wameajiriwa toka Januari mpaka leo hawajapata mishahara. Hii ni aibu! Binti wa kike unampeleka Tutuo pale Sikonge, anakaa pale hana mshahara miezi sita anakula nini, analishwa na nani, unamtakia heri huyu? Acheni kutuharibia mabinti bwana, mtu anakwenda anakaa pale kama amejitosheleza hawezi kupata vishawishi, sasa mtu hana uhakika wa kula jioni Masanja amepita pale anacho chakula anafanyaje sasa? *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Waambie.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Serikali imesikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la hifadhi ya pori la Ugalla. Tunalo pori la Ugala ambalo linajumuisha Wilaya za Urambo, Sikonge na Mpanda. Wapo wananchi wetu ambao kwa kweli kwa miaka mingi wameendelea kupata maslahi yao ya kiuchumi katika yale maeneo ambayo wamepangiwa. Nimeshamwambia Mheshimiwa Zakia Meghji hapa mimi sina utaratibu wa kugombana na watendaji wa Serikali, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu ninakuomba huyu mtu mliyemweka pale kama Meneja wa Pori, muondoeni. Mimi sisomi *Al- badil,* wala sifanyi nini isipokuwa vitendo ambavyo anavifanya huyu Meneja vya kuwanyanyasa watu, kuwabambikia kesi, kukata mipaka bila kuwashirikisha wananchi, naomba aondoke kama mnampenda sana mpelekeni maeneo yenu nako si kuna mapori? Kama hamsikii basi sisi tuna utaratibu wa kijadi huko, ipo siku mtaamka pori halipo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kidogo tu, simjibu Mheshimiwa Ismail Iwvatta, isipokuwa nimewajibika kusema kwa sababu nimetajwatajwa sana.

Naomba ieleweke kwamba kazi ya Mbunge ni kuwaongoza wananchi ambao yeye amegaiwa na Serikali. Mipaka inawekwa na Serikali kwamba wewe Mheshimiwa Mbunge utaongoza eneo hili, sio kazi ya Mbunge. Kazi ya Mbunge sio kukata mipaka. Mimi hapa siwajibika kukata mipaka wala Mheshimiwa Ismail Iwvatta.

Jambo hili lilikwishazungumzwa tukaliacha kwenye Serikali, liko Serikalini lakini ajabu sana Mheshimiwa Ismail Iwvatta na *DC* wake wameingia kwenye eneo la Mkoa wa Tabora, kazi hii wataalam walishafanya kazi yao, wameenda kwenye eneo la Mkoa wa Tabora ndani, nani amewapa mamlaka ya kuanza kukata mipaka ndani ya Mkoa wa Tabora, nani amewapa mamlaka? Viongozi wote wa Tabora hawapo, jamani

mimi nashangaa sana. Mimi naomba mnisaidie jambo hili liishe, mimi sing'ang'anii maeneo, hivi kijiji kimoja unaweza kuking'ang'ania?

**MBUNGE FULANI:** Kinaongeza kura ngapi?

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Kinaongeza kura ngapi? Mimi nina watu ambao pamoja na kazi yangu ya usiku na mchana nashindwa kumaliza shida zao. Serikali naomba sana fanyeni kazi bila kujali wanasiasa wanasema nini, hatugombei mipaka hapa, mipaka inawekwa na Serikali tuiachie ifanye kazi hiyo, eneo unalopewa ndio hilo, tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo hii inatosha, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami naomba kutoa pole zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mpendwa baba yao, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pole kwa maumivu aliyoyapata Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi. Pia natoa pole zangu kwa kijana wetu Mheshimiwa Dr. Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali aliyoipata ambapo anaendelea kutibiwa huko Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nimpe pole Mheshimiwa Estherine Kilasi, kwa kunusurika katika ajali ya gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kushinda kwa kishindo huko Bariadi Mashariki. Namwambia karibu sana Bungeni na hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu katika hotuba yake ameelezea jinsi Serikali nzima ilivyofanya kazi yake kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha wa 2003/2004 na niseme kwamba kwa kweli inaridhisha sana tena sana japokuwa akumbuke kwamba binadamu si mkamilifu, kwa hiyo, kuna wale ambao watasema hajafanya kazi, lakini ninachotaka kumhakikishia kwamba kazi waliyofanya chini ya uongozi wake ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mimi najikumbusha kabla ya mwaka 2001 kulikuwa na kilio cha wazazi wengi sana kuhusu michango ya aina mbalimbali kwa maana ya kuchangia shule. Lakini kwa vile Tanzania ilijaribu kuweka sera zake nzuri na

kurekebisha mfumo wake wa uchumi, wakubwa walituweka Tanzania katika kundi la *HIPC* waliweza kusaidia kuweza kupata misaada ambayo imekwenda kuboresha mambo mengi tu ya huduma za jamii kwa mfano elimu, maji, afya, barabara, mazingira na kadhalika. Ni kweli kabisa kwamba katika uboreshaji wa elimu ya msingi ni mojawapo ya njia sahihi kabisa ya kuweza kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi napata moyo kwamba kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri Joseph Mungai, wakati akijibu swali langu kwamba pia kuna mpango sasa hivi ambao utaruhusu wale wanaomaliza shule ya msingi kwa mpango huu MMEM wa sasa hivi ifikapo mwaka 2009 kwamba hata kwenye shule za sekondari basi Serikali itajitahidi kadri iwezekanavyo kuwasaidia wanafunzi wengi zaidi waweze kumaliza kidato cha nne ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapomaliza shule wanakuwa na umri wa miaka 18 na hapo kuweza kujitegemea katika kujiajiri na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo bado yapo pale pale, naelewa kabisa kwa mfano, mambo ya madawati na kadhalika, lakini Serikali imejitahidi kwa hilo. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuwasaidia wazazi kuwaondolea matatizo ya michango ya elimu ya msingi. Sasa hivi mzazi anachochangia ni nguo za mtoto, chakula, malazi na nauli pale inapolazimika ya mtoto kwenda shuleni na kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji kwenye Jimbo langu la Kinondoni kumekuwa na matatizo mengi sana ya maji lakini nashukuru sana kwa ushirikiano wa hali ya juu na namshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa na *DAWASA,* wametusaidia sana katika Jimbo la Kinondoni kupata maji. Sasa hivi maji ni mengi mno kinachotakiwa ni kuyarekebisha yakae sawasawa. Lakini nikigusia kidogo kwa hilo nashukuru sana kwamba Mheshimiwa Edward Lowassa alitembelea Cairo, Misri hivi karibuni. Cairo mimi nilibahatika kuwepo kwa muda wa miaka mitano. Wenzetu hawana ardhi, wanategemea *land reclaimation* kwa maana ya kupata eneo la kuweza kuweka udongo wa kisasa na kuweza kulima kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachofanya wenzetu ni kupata hayo maeneo ambayo yamekuwa *reclaimed* na kupeleka vijana wao pamoja na miundombinu mbalimbali kama shule, hospitali na kadhalika na kwamba watoto wao wanapomaliza Chuo Kikuu wanapelekwa huko na kwa muda wa miaka mitano hawa vijana wanalipwa mshahara lakini pia wanapewa mikopo ya nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka mitano hizo nyumba zinakuwa ni mali yao. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba kuna kivutio kuwatoa watoto kwenye Miji mikubwa kama Cairo, Alexandria na kwenda kwenye *Satellite Township* ili waweze kuishi huko na ndivyo ninavyoiomba Serikali yetu hapa kwamba kwa maana hiyo hiyo Serikali yetu isiendelee kuzungumzia kilimo cha umwagiliaji bila kutafuta miundombinu ya vijana wetu kurudi Mikoani. Sisi bahati nzuri tuna ardhi na maji, kwa maana hiyo basi Serikali ifanye kila liwezekanalo kuweka vivutio vya makusudi kabisa ili vijana wetu warudi Mikoani huko wakafanye kazi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie matatizo ambayo yapo kwenye Jimbo la Kinondoni na niseme Jiji la Dar es Salaam. Hapa juzi tumeambiwa kwamba Serikali itatoa fedha zaidi kwa maana ya vitendea kazi ili kudhibiti hali ya uhalifu nchi nzima na hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi wa mwaka kesho. Lakini ningependa kuongezea kwamba mojawapo ya kitendea kazi basi iwe ni taa za barabarani maana yake giza la barabarani ni vichaka vya wabakaji. Tunaomba Serikali izisaidie Manispaa na Jiji la Dar es Salaam kuwapatia fedha za kuweza kuweka taa barabarani, ni muhimu sana ili kupunguza majambazi kuvamia wananchi wakati wa usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Serikali kwa kurudisha tena mpango wa kuwapa wazee ambao walichukua fedha zao za mkupuo za pensheni miaka kadhaa iliyopita. Akina Peter Kabisa hapa, nashukuru sana kwa hilo, lakini labda tu kama nilivyosema kwenye maandishi yangu kwamba *beggars can't be choosers* kwa maana mwombaji huwezi kuchagua, lakini nadhani kuna haja ya Serikali kwa ukarimu huo huo na hekima zao basi hawa wazee wapate angalau kima cha chini cha hiyo cha mshahara kuwa ndio pensheni. Naomba sana Serikali iwasaidie kwa kujaribu kuwapatia hiyo pensheni ya kima cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwamba Hospitali ya Mwananyamala ambayo ni Hospitali ya Wilaya ya Kinondoni yenye wakazi zaidi ya milioni 1.08 wapatiwe *X-ray* nzuri kwa ajili ya hospitali hiyo. Sasa hivi tuna *X-ray machine* ambayo inafanya kazi kwa watu 20 tu kutwa ambapo kinachotakiwa iwe zaidi ya watu 100. Sasa tunaomba Serikali kwamba itusaidie katika hilo kwa maana ya TAMISEMI na wote wanaohusika katika kuhakikisha kwamba hali ya huduma ya afya katika Wilaya ya Kinondoni inakuwa nzuri. Tunaomba sana mtusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika nikiongezea katika hilo hilo kwamba nimesikitishwa sana kwamba hapa Dodoma hospitali ya Serikali kuna mhudumu mmoja tu wa mifupa *(Physiotherapist)* (Mama Cheza). Ningetegemea kwamba kwa hospitali ya hapa kwa kuwa wengi tupo hapa basi kungekuwa na wahudumu angalau watano wa *Physiotherapy* na watano *Orthopaedic* lakini kuna kijana mmoja tu ambaye anafanyakazi zote hizo na kweli anatingwa na kazi. Tunaomba Serikali ilitazame hili kwamba, Mji Mkuu wa nchi ya Tanzania Dodoma basi inapatiwa hao wahudumu wa *Physiotherapy* na *Orthopaedic* mapema iwezekanavyo angalau tuwe na wafanyakazi watano au sita hivi kwa kila idara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa Madiwani wetu. Labda niseme tu kwamba sisi tumechukulia nafasi ya Madiwani kama vile wanavyochukuliwa wenzetu Waingereza. Tanzania siyo sawa na Uingereza, Diwani wa Uingereza anafanya kazi hii tuite ni *civic duty or civic responsibility,* mtu ambaye ametajirika, ana uwezo mkubwa tu anajimudu mwenyewe lakini hapa kwetu Diwani ni mwenzetu, anasimamia kazi kwa makini kabisa na kwa masaa mengi sana. Naomba kabisa kwamba hawa Madiwani wenzetu pia wafikiriwe kuwezeshwa kupatiwa kama ni mkopo wa magari na kusamehewa kodi ya magari ili wafanye kazi zao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie kwa haraka sana kuhusu shule moja inayoitwa *Kambangwa Secondary School.* Shule hii inakabiliwa na matatizo

ya kutokuwa na maabara kwa maana ya chumba na vifaa vya maabara pamoja na chumba cha kompyuta. Tungeomba Serikali hasa kwa upande wa Wizara ya Elimu iangalie katika mgao wake wa fedha basi kuipatia vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kwamba Serikali itazame na uwezo wake itakavyoweza kutusaidia kujenga daraja la kati ya Tandale-Manzese-Ndugumbi na Mwananyamala daraja la Manjunju ambalo ndiyo kiungo kikubwa sana kwa watu ambao kila siku wanapita pita kwa vivuko vya hatari hatari watu kama laki nane kwa kutwa. Tunaomba Serikali ilitazame hilo kwa sababu Manispaa ya Kinondoni haina uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara zetu mara kwa mara tunapata malalamiko ya wananchi kuhusu Mahakama, Polisi na Hospitali kwa maana ya rushwa. Sijui kama Serikali ina majibu, mimi sina jibu lakini naomba kwa kweli pale ambapo mnapata taarifa za wahalifu hawa basi tafadhali sana myahifadhi majina yao hao watoaji taarifa, vinginevyo taarifa zaidi hazitatoka. Kwa hiyo, tunaomba sana mjaribu kuangalia hayo kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana katika eneo la Kigogo ambalo linatokana na mabadiliko ya Mto Msimbazi kutoka sehemu ya SUKITA kule daraja la Mandela. Kuna *embankment* moja ambayo inaunganisha tawi la Mapera na Kigogo Kati. Huo mmomonyoko unatisha sana, naomba Serikali iliangalie hili na kuweza kutusaidia, litazamwe na wataalam na liweze kupatiwa ufumbuzi wake. Lakini eneo hilo hilo pia lina matatizo kwa watembea kwa miguu kati ya Kinondoni Mkwajuni kuelekea barabara ya Mandela kuna eneo linaitwa Jaba, wananchi wanakerwa sana na mwananchi mmoja ambaye anafunga maeneo kwa kuwakataza wananchi wasipite maeneo hayo. Tunaomba Serikali iingilie kati na itusaidie kulimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba sana kwamba *TANESCO* wajaribu kurekebisha *tariffs* zao. Kinachoendelea sasa hivi ni kwamba *TANESCO* wanataka sisi Watanzania tuvune miti yetu yote kwa ajili ya mkaa na tulete jangwa katika nchi hii. Hiyo haitatusaidia, naomba Serikali iingilie kati kuhakikisha kwamba wananchi wanaweza kutumia umeme kwa maendeleo kuliko kuendelea kukata miti na kutengeneza mkaa kwa ajili ya matumizi ya majumbani mwao. Naomba sana Serikali ilitazame hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme tena kwamba mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nawapongeza sana kwa kazi wanayofanya. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa jioni ya leo ili nichangie hotuba ya Waziri Mkuu. Kabla sijaendelea nami natumia utamaduni ule ule wa kuwapa pole wenzetu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kufiwa na mzee wao. Vile vile nawapa pole wale ambao walipata bahati mbaya katika safari ya kuja Dodoma,

walioanguka na gari na walioporwa na majambazi ili kuhakikisha kuwa na wao wanapata nafuu na subira katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea mbele naomba nimpe hongera au shukrani nyingi Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kuchaguliwa kuja tena katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi hiki cha kumalizia, kumalizia ni kutamu kuliko kuanza. *(Kicheko)*

Katika mchango wangu wa leo kwanza najielekeza moja kwa moja katika mfuko wa *TASAF*. Mpango huu kwa kweli ni mzuri sana na umeanza katika *speed* nzuri na kwa kweli una faraja na mafanikio makubwa kwa wananchi. Ni mpango ambao kwa kweli umewashirikisha wananchi toka mwanzo mpaka kumalizia kwa miradi yao. Kwa hiyo, nashukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hili kwamba wameweza kuhakikisha kuwa *TASAF* imeenea na itaenea katika sehemu zote ambazo malengo yake ni kuondoa umaskini kwa jamii yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa linalotukabili hivi sasa katika mfuko wa *TASAF* niliseme tu kuwa ni suala la Bajeti, Bajeti ambayo wanaiweka wakicheleweshewa pesa kidogo tu, kwa jinsi bei za vitu zinavyopanda inaleta usumbufu na matatizo kwa wale ambao wanafuatilia shughuli za mradi. Kwa hiyo, naomba kwa suala hili *TASAF* wajitahidi kutoa zile fedha kwa wakati kwa sababu wakichelewesha vitu vinapanda bei na mradi unakosa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vile vile niseme kuwa naomba *TASAF* ilizingatie kwa makini katika huu mradi ambao unaanzishwa. Kuna miradi inaanzishwa lakini inafikia mahali unakuwa na jengo zuri bila matumizi. Kwa mfano, kama unaanzisha shule, inamalizika lakini shule hiyo inamaliziwa jengo tu hakuna vifaa vya aina yoyote, inakuwa haina faida.

Kwa hiyo, kama kuna uwezekano au ipo fedha ya kutosha basi ipo haja kama shule basi imaliziwe na madawati na vifaa vingine, kama hospitali ipatiwe na vile vifaa vya kuhakikisha kuwa inakamilika na inaanza kufanya kazi. Matatizo kama haya tumeshayaona na tunayakabili katika Majimbo yetu kuwa majengo tayari lakini hivi sasa yanashindwa utekelezaji kutokana na ule mradi wenyewe haujakuwa tayari kutumika kwa sababu ya kuwa umekosa vifaa vya kufanyia kazi kwa wakati ule. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kama upo uwezekano mfuko wa *TASAF* basi ile Bajeti yake iwekwe mpaka kuhakikisha kuwa ule mradi unamalizika na unaweza kufanya kazi. Hilo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kulizugumzia ni kuwa katika hotuba ya Waziri Mkuu amezungumzia kuhusu suala la ulinzi. Amelizungumzia vizuri tu kuwa katika shughuli za ulinzi tutaimarisha vikosi vyetu na kuhakikisha kuwa tunajenga makambi au vituo vya Polisi. Hili ni jambo zuri na kwa kweli kwa kipindi tunachokwenda ni zuri sana katika harakati zetu hususan kwa shughuli za uchaguzi. Kuweka Polisi wetu mahali ambapo kuna usalama zaidi ni shughuli ambayo inataka kufanyika kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tuliuliza swali kuhusu Mkoa wa Kaskazini una vituo vya Polisi yaani tumerithi toka wakati wa ukoloni mpaka leo ni miaka 50 lakini vinashindwa ukarabati na Mheshimiwa Naibu Waziri aliposema, amezungumzia kuwa fungu lililotengwa limepelekwa Zanzibar. Tatizo la Zanzibar ukilipeleka fungu la Muungano na ile ni miradi ambayo haijapangwa, inapangwa ile miradi ambayo mtu anaiona hii inaweza kumletea faraja au inamletea sifa yeye mwenye. Kuna mambo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazungumzia hili kwa mifano hai. Tunaomba siku zote hapa fedha ya Kambi ya Jeshi la Wananchi Potoa, Waziri hapa anajibu pesa zimepelekwa, lakini hiyo fedha inayopelekwa inapelekwa Zanzibar. Ikishapelekwa Zanzibar ugawaji wake anaujua Brigedia yeye mwenyewe na watu wake, kule ambako inahusika haiendi ipasavyo. Kwa hiyo, hili ni suala kwa kweli ambalo lazima liangaliwe. Kwa yale mafungu ambayo yanatengwa katika vitengo vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kule Zanzibar tuhakikishe kuwa zinafika katika zile sehemu ambazo zinakusudiwa. Kwa maana hiyo niseme kuwa kama Kituo cha Polisi cha Mkokotoni hakikufanyiwa ukarabati ambacho ni Makao Makuu ya Polisi Mkoa, basi kitakuwa na hali ngumu na hivi sasa kinaendelea kuvuja, hakuna pa kukaa, wanafanya kazi katika mazingira magumu na wanaishi uraiani.

Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli hivi sasa lazima lifanyiwe kazi na tuhakikishe kuwa hii fedha ambayo imepelekwa Zanzibar basi inafika kule ambako imekusudiwa kufanyiwa kazi kama Kituo cha Polisi cha Mkokotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni kwamba, tunapozungumzia suala la Ukimwi watu wanaona hivi sasa kama si jambo ambalo ni karaha tena kama pale mwanzo lilivyokuja. Hivi sasa limekuwa kama ni *fashion* tu, ukilizungumzia, ona soksi, ona nini, mambo ambayo kwa kweli yanakuja na kupita kama misimu tu ya maneno na kupita yanaanza, yanakwenda na kuishia.

Lakini kwa kweli ni suala zito, juzi hapa nimeuliza swali kuhusu sheria ambayo inazuia jambo hili la ngono, tukapigwa chenga na Waziri kwamba tutaweka sheria. Lakini kwa kweli sheria iliyokuwepo imepitwa na wakati lazima ifanyiwe marekebisho. Tuhakikishe kuwa tunaziba ile mianya ya kuhakikisha kuwa ngono zinaendelea kiuzembe na tuhakikishe kuwa kama hatutoziba ile mianya basi Ukimwi hautokwisha, kwa hiyo tuhakikishe kuwa tunaiziba ile mianya kwa sababu sheria ya Ukimwi kwa jinsi tunavyodai kuwa haki za binadamu hatuwezi, lakini tuweke zile sheria ambazo zinahakikisha kuwa tunamdhibiti mtu ambapo hawezi kutembea uchi, hawezi kufanya ushoga, hawezi kufanya ubasha au mambo ambayo yatahakikisha kuwa yanaweza kumfanyia karaha binadamu ambaye mwisho anaweza kupata Ukimwi. Hili jambo kwa kweli si mzaha na tusilifanyie mzaha na tunapolisema tunasema kama ni la kubabaisha babaisha tu lakini kwa kweli ni hatari kwa jamii yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona katika Wizara kuna kifungu kinawekwa cha kutoa mafunzo ya Ukimwi lakini taratibu au mafunzo yanayopatikana kwa wafanyakazi

hayaeleweki na Ukimwi unazidi siku zote kwa wafanyakazi. Sasa utajiuliza ile pesa inakwenda wapi? Inazuia au inaongeza Ukimwi?

Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli linashangaza na kusikitisha sana. Kwa hiyo, suala hili lazima tulifanyie au tuweke utaratibu au mkakati ambao tunahakikisha kuwa tunaweza kuhakikisha kuwa linapungua. Kama misemo ya Kiswahili tupunguze semina, makongamano au warsha kwa sababu katika mambo haya kama utawaachia watu binadam tulivyo yule afisa au mtu ambaye anawapikia wakimbizi anataka yeye siku zote wawepo pale ili apate mshahara. Mwuza majeneza anataka siku zote watu wafe ili ahakikishe kuwa anauza majeneza na hivi Vyama vya Hiari au watu ambao wanashughulikia haya masuala ya Ukimwi wao siku zote wataomba uendelee kwa sababu wanataka wapate pesa za semina. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli halijakuwa na nguvu katika jamii kuhakikisha kuwa linaangaliwa kwa uangalifu yaani ni suala zito kwa kweli tusilifanyie mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nilizungumzie suala zima kuhusu taarifa ya Waziri Mkuu, ukurasa wa nne alizungumzia sana suala la Muungano jinsi tunavyouenzi Muungano wetu, waasisi wetu walivyokuwepo walivyouenzi na nashukuru sana na viongozi waliokuwepo madarakani hivi sasa wanauenzi Muungano. Kwa kweli nawasifu sana kwa hatua hiyo wanauyenga yenga angalau tuwe nao kwa kipindi hiki. Lakini tatizo kubwa ambalo tunalipata hivi sasa ni suala zima kuwa Zanzibar hakuna Ofisi ya Makamu wa Rais, ni suala zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jinsi ya kufanya kazi Zanzibar suala hili ni zito kwa sababu tatizo la Zanzibar hakuna idara yoyote ambayo inashughulikia masuala ya Muungano, hakuna idara ambayo inashughulikia umaskini, hakuna idara ambayo inashughulikia mazingira, ni hiyo hiyo *Private Office* ya Mheshimiwa Makamu wa Rais inashughulikia mambo yote ambayo yanahusiana na Muungano, ambalo ni tatizo. Ni mzigo mzito ambao wanaupata wafanyakazi wale ambao hawana maarifa wala ujuzi wa kuendesha shughuli hizo lakini wanafanya shughuli hizo katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kuwa kuna tatizo lingine kuhusu sheria zetu. Sheria ambazo zinalenga masuala ya Muungano ni sheria ambazo kwa kweli zinatuhangaisha Wabunge wakati ambapo tunajadili Miswada mara nyingi sana ikiwa kwenye Kamati au kwenye Bunge. Kuna sheria utaikuta ambayo inahusiana na mambo ya Muungano, ukimwuliza Waziri hii umemhusisha Waziri wa Zanzibar anakwambia tumemshirikisha toka mwanzo mpaka mwisho. Lakini ukifika Zanzibar anakwambia sisi hatujashirikishwa wala hatujaonyeshwa hiyo sheria yenyewe na imepitishwa bila sisi kushirikishwa. Kwa hiyo, mambo kama haya kama hatutayachunguza sana kwa kweli yanaharibu hii sifa tuliyonayo ya Muungano. Kwa hiyo, ipo haja ya kuwa kama sheria inahusiana na shughuli za Muungano basi zishirikishwe pande zote mbili ili kuuondoa huu utata uliopo. Sababu hata sisi Wabunge wa Zanzibar ukifika kule wale Mawaziri wanakupiga chenga au danadana, wanakwambia bwana wewe hawajawahi hata kutushirikisha katika sheria hii na zinakuwa ngumu kutekelezwa au utekelezaji wake unakuwa mgumu. Kwa hiyo, kwa hili naomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilione, toka mwanzo hatua zote za ile Miswada tuhakikishe kuwa wanashirikishwa na wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho nilielekeze katika Ofisi ya Bunge. Tunajitahidi sana kushiriki katika shughuli zetu za michezo na tunaulizia hapa masuala mengi ambayo yanahusiana na michezo lakini hakuna motisha kwa wale wachezaji na sisi tunajitahidi sana kuwachangia wenzetu ambao wanakuja kutaka misaada juu yetu Wabunge au timu ya Wabunge. Lakini hii timu ya Wabunge mbona haipati hata uhisani au ufadhili hivi kutoka nje angalau kuwekewa basi la Scandinavia kutembelea Kenya na Uganda?

Kwa hiyo, kwa hili angalau mlione kwa hii timu yetu kwani tunatoa jasho jingi bila mafanikio ambapo tumeshawachangia watu wengi tu sisi kama wachezaji. Kwa hiyo, Ofisi ya Spika ihakikishe kuwa angalau siku moja tunapelekwa nje, tunahakikisha kuwa tunafaidika na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa wasaa wa kujumuika na wenzangu kuichangia hoja iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kama ilivyo kawaida yetu naomba nichukue fursa hii niwape pole wenzetu wafiwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpenzi. Mwenyezi Mungu aiweke mahali pema roho yake. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpe pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na binti yake na yeye vile vile Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya rambirambi hizo ningeomba vile vile niwape pole wenzetu ambao kwa njia moja au nyingine walipata maafa yakiwemo ya ujambazi pamoja na ajali. Mwenyezi Mungu awape subira na awaepushe na mambo mengine mabaya kama walivyosalimika kutokana na maafa hayo.

Zaidi naomba nichukue fursa hii kuwapongeza tena Waheshimiwa viongozi wetu ambao wamechaguliwa kutuwakilisha katika Bunge la Afrika hususan nimpongeze sana tena sana Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella ambaye amechaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika akiwa ni Rais wa kwanza katika shughuli hizi. Nimefurahi sana kwamba Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella sasa hivi hayupo kwa sababu utakapomsifu mtu ikiwa yupo, hutakuwa unamsifu bali utakuwa unamsema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nataka nichukue nafasi hii kumsifu siyo kumsema kwa sababu hayupo. Wale ambao wamebahatika kuwa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella wameshuhudia ni jinsi gani mama yetu huyu anavyoshirikisha na anavyojitolea kwa hali na mali katika kulileteа sifa Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimebahatika kuwa naye na kwa hiyo sifa hizi si sifa za kimasihara, ni sifa za ukweli na namwombea azidi kubarikiwa na azidi kutuwakilisha katika hali ya fahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ningependa nitoe maelezo kidogo kufuatana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba Rais wetu mpendwa Rais Benjamin William Mkapa anamaliza kipindi chake, sifa zake hatuishi kuzihadithia na katika ujio wake amekuwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tatu na kila Awamu imekuja n utaratibu wake. Kwa bahati Rais wetu huyu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Sasa kutokana na mwenendo wake huo naamini wazi Mawaziri wake, Askari wa Miavuli wamechukua kila juhudi kwa kadri ya uwezo wao kufuata wosia wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Akiondoka kesho kutwa pengine ni sisi sisi hapa tunataka Urais. Kwa hiyo, ningetoa ushauri kwamba wale watakaokuja kutaka Urais tafadhali na wao wafuate nyayo za Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa pamoja na Askari wake wa Miavuli, kama hatatokezea mwingine hapo, wasisahau kufuata nyayo za Rais wetu mpenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, ningependa nizungumzie kuhusiana na suala la Bunge. Hivi sasa mnajua Bunge letu ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa nikuulize kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri tumepewa bendera za aina tatu. Bendera ya mezani, bendera ya kwenye gari na bendera ya kuweka ofisini, hivyo kati yetu ni wangapi waliotundika bendera zao ofisini na ikiwa kama hiyo ndiyo hali hasa kule Zanzibar hakuna au ni Waheshimiwa Wabunge wachache waliopata fursa ya kutundika bendera katika ofisi zao na sababu ni kwamba hawana ofisi. Sasa kuna utaratibu wa Serikali wa kutujengea ofisi Waheshimiwa Wabunge. Kwa upande wa Zanzibar tunaambiwa kwamba shughuli hii inashughulikiwa na Ofisi ya Waziri Kiongozi sijui kama wenzetu tayari wameshapata au bado, lakini kwa kusema kweli kwa mwenendo wa utaratibu na polepole uliokuwepo itachukua muda pengine karne nzima ya kuja kuona kwamba Mheshimiwa Mbunge anapeperusha bendera kwenye ofisi yake Zanzibar.

Kwa hiyo, ningeshauri sana Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati tunapolizingatia suala la kuzijenga ofisi wazungumze ipasavyo kwa kila hali na mali ili kuona kwamba ofisi hizi zinapojengwa kule Zanzibar na Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lishughulike kwa kiasi fulani ili kuona kwamba ofisi zile zinajengwa sambamba kama zitakapojengwa Tanzania Bara na kule Zanzibar vilevile zijengwe ili na sisi isiwe bendera zile tukaziweka kama ni mapambo tu ya baadaye ukimaliza muda wako unakuja kuona kwamba hii ilikuwa ni bendera ya Bunge. Kwa hiyo, ningeomba sana suala hili nalo tulizingatie ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la uchumi. Tukubali au tusikubali kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa Zanzibar unategemea Tanzania Bara na hali ya uchumi kwa Zanzibar ni mbaya. Kama tumesikiliza hata Bajeti kwa taarifa ya safari hii ni kwamba ina upungufu wa asilimia 5.5, hii inatokana na kipato cha Zanzibar. Kwa hiyo, nawashauri sana wenzetu wa Tanzania Bara tukawa na ushirikiano wa makusudi wa kuona kwamba tunadumisha biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara ili nayo iweze kusaidiwa kama zilivyokuwa zinasaidiwa sekta nyingine katika kuimarisha uchumi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, hali hii ionekane ili na wale wenzetu kutoka Zanzibar hasa wafanyabiashara ndogo ndogo na wao wawe wanafaidika kwa zile biashara ambazo wenyewe watakuja nazo ili tupunguzie bughudha pale wanapofika angalau pale gatini ili waweze kufanya biashara zao na kupata uchumi kwa kiasi fulani wanachoweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusiana na hali ya Ulinzi na Usalama. Naomba nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya kwa Zanzibar. Lakini nilikuwa na dukuduku moja ambalo leo naona niitumie nafasi hii angalau lieleweke. Katika Jeshi letu la Polisi tunajitahidi kuona kwamba tunawapa ajira akinamama na wao wafanye kazi sawasawa na wanaume katika Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la kushangaza kwa ushahidi uliokuwepo ni kwamba kuna vitendo ambavyo hujitokeza kudhalilishwa Askari Wanawake ikafika hadi kupigwa na matokeo kwa ushahidi kamili mpaka leo inakaribia mwaka hatujui kesi hii imekwenda vipi. Matokeo yake mhusika baada ya kutoa maelezo amepata uhamisho wa Idara ile amepelekwa katika Idara nyingine. Sasa ikiwa kama hali itakuwa kama hii nafikiri hii inaweza ikatufikisha mahali pabaya.

Kwa hiyo, naomba sana Jeshi letu hili la Ulinzi nalo likakaa tukawapa hadhi sawasawa akinamama kama tunavyowapa hadhi wanaume ambao kwa njia nyingine wanaweza kujitetea lakini mwanamke na yeye akikusudia anaweza akajitetea. Kwa hiyo tusingojee ikafikia hatua hii kuna haja ya kuona mambo kama haya tunayachukulia kila hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu Mpango wa Elimu. Kuna utaratibu mzuri tu kwa wenzetu wa Tanzania Bara, Mpango wa Elimu ya Msingi na tumeshuhudia hasa mimi mwenyewe nikiwemo katika Kamati ya Huduma za Jamii nimeona jinsi gani Wizara ya Elimu na Utamaduni inavyojitahidi kunyanyua elimu ya msingi.

Vile vile nimeshuhudia katika Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu. Lakini kinachonisikitisha ni kwamba bado walimu katika Wizara hii wana masikitiko makubwa sana. Kuna haja ya dhati kuona kwamba kwa kweli wanafikiriwa. Sasa hii ni kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar kweli shughuli hizi si za Muungano. Lakini kwa suala la Elimu ya Juu tunasema ni suala la Muungano. Sasa

wenzetu mna mpango wa MMEM, kesho mna mpango wa MMES, lakini mpango wa MMES ni matayarisho ya Mpango wa MEVYU yaani Mpango wa Elimu wa Vyuo ambao pengine mtakuja kuutayarisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba sana kuwe na ushirikiano wa kutosha kati ya Tanzania Bara na Wizara ya Elimu iliyokuwa Zanzibar ili twende sambamba katika kuona kwamba tunawaweka katika hali ya elimu vijana wetu katika hali ambayo inastahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo maelezo machache, naomba tena nichukue fursa hii kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mimi nianze kwa kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na mzazi wao. Pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa kufiwa na binti yake, tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Pia Mheshimiwa Anne Kilango, pole kwa yaliyokupata. Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere poleni kwa ajali. Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere huko uliko hospitalini tunamwomba Mwenyezi Mungu upone haraka uje kwenye Bunge hili tusukume jahazi hili la nchi yetu.

Mheshimiwa Danhi Makanga hongera karibu tena hapa Bungeni lakini kubwa zaidi karibu kundini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wake wawili wa Nchi, Katibu Mkuu, dada yangu Rose Lugembe, Manaibu Makatibu Wakuu katika Wizara hiyo pamoja na Maafisa wote walioko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri na yenye matumaini iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niwatoe wasiwasi, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya hotuba yake Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali. Serikali ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu akiwa kiongozi wake na kusema kweli yeye kama Waziri Mkuu amevunja rekodi kwa sababu kati ya watu waliokaa katika ofisi ile nafikiri yeye ndiye aliyekaa katika ofisi ile kwa muda mrefu kupita wengine. Hongera kwa kuweza kuhimili muda wote huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu imefanya makubwa na ya kihistoria, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamekwishasema wenye macho hawaambiwi tazama, yanaonekana wazi, wananchi wetu wanaona wazi.

Sasa mimi kwa sababu ya muda ni mfupi sitarudia yale makubwa ya kihistoria mengi ambayo Serikali hii imeyafanya nitasema machache tu. Uchumi wetu unaonyesha kila dalili za kutengemaa, kuna *Macro Economic Stability,* mfumuko wa bei ndiyo hiyo katika miaka mitatu mfululizo kati ya asilimia 4 mpaka 5, Sekta ya Ujenzi kuna maajabu na makubwa yanayoendelea kule, kwa mara ya kwanza sisi tunatengeneza barabara za lami kwa kutumia fedha zetu wenyewe. Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo yapo makubwa yanayofanyika kule tunatumia maji ya *Lake Victoria* kwa mara ya kwanza kupeleka maji katika Mkoa wa Shinyanga. Elimu MMEM wamekwishasema wenzangu mambo makubwa sana yanafanyika katika Taifa nzima tunangojea MMES. Wizara ya Afya yapo mengi makubwa yanayofanyika katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitakachofanya tu nitatilia mkazo katika yale maeneo machache ambayo naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali yake wakiyafanyia kazi kikamilifu basi uchumi wetu utapaa vizuri na kufikia kile kiwango cha asilimia 8 ambayo tunategemea ifikie katika kipindi kifupi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo hayo ni nini? Wamesema kuna umuhimu tuiangalie Sekta ya Kilimo izae matunda ambayo tunataka izae. Sasa sitasema mengi katika Sekta ya Kilimo. Niseme moja tu kuvalia njuga suala hili la kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo ambayo itaweka mkazo kwenye Sekta ya Kilimo.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda, alisema hana matatizo Serikali imeamua kuanzisha Benki hiyo. Lakini leo asubuhi kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, amesema Serikali imeamua kuanzisha Benki ya Kilimo sasa sijui kama ni Benki ya Kilimo pamoja na Benki ya Maendeleo zote mbili, lakini hata kama zote mbili zikianzishwa tutasema *Alhamdulillah* tuendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonitia wasiwasi mimi ni pale Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, aliposema bado kuna utafiti unaotakiwa kufanywa kabla ya kuanzishwa kwa Benki hiyo ya Maendeleo. Sasa nikajiuliza utafiti huo ni wa nini tena? Nchi yetu ya Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo haina benki ya Maendeleo, nchi nyingine zote ninazozielewa mimi zina Benki ya Maendeleo kwa ajili ya kusukuma sekta muhimu katika nchi zao hata Marekani wanayo *EXIM Bank* kwa ajili ya ku-*promote exports* za Marekani nje na hiyo *EXIM Bank* ni ya Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanayo *Overseas Private Investment Corporation* kwa ajili ya ku-*promote investments* za Wamarekani nje ya nchi ni ya Serikali hiyo, wanayo *Small Business Administration (SBA)* kwa ajili ya ku-*promote* biashara ndogo ndogo hizi hasa ile ya ku-*empower the black Americans.* Sasa sisi tuliambiwa tutoke kwenye Sekta ya Biashara, Sekta ya Uchumi tukatoka *Livestock and Barrel* tukaachie zetu zife tulifanya makosa. Sasa makosa hayo tuyasahihishe upesi. Hatuna sababu ya kungojea Mheshimiwa Waziri Mkuu, mifano iko mingi ni suala la kuchagua mfano gani tunautaka tuanzishe Benki hiyo ya Maendeleo msukumo uletwe katika Sekta ya Kilimo na zingine ambazo tunazihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunapofanya hivyo basi tujue kwamba kitu kinachotakiwa ni benki hizi zitoe *concessional loans.* Pale popote palipotokea *green revolution* imetokea baada ya Serikali zao kuamua kutoa *concessional loans* kwa ajili ya sekta zao muhimu. Sasa hiyo tuifanye kazi mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *Mortgage Finance,* hii ndiyo nchi pekee tu ambayo haina *Mortgage Finance Facilities.* Tunajenga nyumba zetu kwa kulipa *cash,* wapi inafanyika duniani kitu kama hicho. Milioni 70 *cash* kujenga nyumba haiwezekani, tusiwaweke watu wetu kwenye majaribu au tuhakikishe kwamba hizi *Commercial Banks* zinahamasishwa ili ziweze kutoa *Mortgage Finance Facilities* ambazo ni za muda mrefu kuanzia miaka 15 mpaka 30 au kama hizo hazitafanya kazi hiyo basi sisi wenyewe tuanzishe *Housing Finance Banks.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu akishughulika na hilo kikamilifu atatuondolea adha hii tuliyonayo. Nawasifu na kuwapongeza kwa hatua ya Serikali ya kuwakopesha watumishi wetu nyumba za kuishi. Endeleni na hiyo, hiyo ndiyo njia ya kuwawezesha Watanzania. Nataka pia zile nyumba za *National Housing Corporation* wapangaji wote wanaokaa ndani ya zile nyumba wakopeshwe zile nyumba. Pale Arusha kwangu nina nyumba zingine zipo *Cuban Quarters,* maghorofani wote wauziwe hizo nyumba. Lakini unavyowauzia hivyo uwe umekwishaanzisha *Housing Finance Institution* kuwawezesha wao kuweza kuzinunua hizo nyumba. Vinginevyo utawaweka tu katika hali mbaya ile tutakuwa tunagongana hapa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba mzingatie hilo mtuondolee hii adha ambayo ipo na ukiangalia kusema kweli katika nchi yetu tuna hatimiliki karibu 86,0000 hazijafanya kazi kufufua hii sekta ya Ujenzi. Kwa watu milioni 34 hatimiliki hizi tu hatujafanya kazi bado tunasingizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Land Bank* tunaambiwa sasa hivi ina *seven hundred and forty three pieces* yenye *2.6 hectors* hizi ndiyo zingekuwa msingi mkubwa kabisa wa kuweza kuzifanya hizi *Housing Finance Institutions* kuneemeka, kushabikia, kusukuma uchumi wetu uweze kufikia kwenye ile asilimia 7 na 8 ambayo tunaitaka sisi. Naangalia tena nyumba zilizouzwa mwaka 2003 ni 759 bado *really estate market,* Tanzania bado iko duni sana. Sasa tuweke mkazo wetu pale tutengeneze mazingira mazuri ili sekta hii nayo iweze ku-*play its role* katika kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni hili la *IPTL, TANESCO* na gharama kubwa ya umeme Tanzania. Katika Bajeti hii katika vile vitabu tulivyopewa Wizara ya Nishati na Madini, *Sub vote 3001* imetengewa shilingi bilioni 126 na hizo tunaambiwa ni kwa ajili ya gharama za *IPTL.*

Sasa nakaa najiuliza kidogo kile kinachoelewa juu ya *IPTL* ni kwamba mtambo wote ule haukuzidi *120 million US dollars* kwa kutengeneza mtambo wote ule hauzidi hivyo. Sasa sisi kwenye Bajeti ya mwaka moja tunaweka bilioni 126 kwa ajili ya kugharimia gharama za mwaka mmoja ni biashara gani hii jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu livalie njuga hili uchumi wetu unabeba mzigo ambao haustahili kupewa na hakuna sababu ya kupewa mzigo wa namna hiyo. Mimi ninachoambiwa sasa hivi ni kwamba wale *shareholders* wa *IPTL* sasa hivi wako kwenye harakati za kutaka kuuza ile *investment* yako kule na ku-*refinance the whole package.* Tunajua *the whole package was financed* sehemu kubwa imekuwa *financed* na Benki ya Malaysia inaitwa Danaharta ambayo ni ya Serikali na hiyo Kampuni naambiwa iko tayari ku-*write off* sehemu ya lile deni.

Sasa nasema huu ndiyo wakati wa sisi kama Serikali kuchangamkia tatizo hili ili tulisimamie, tulidhibiti na tuhakikishe kwamba uchumi wetu unaokolewa kutokana na mzigo huu mkubwa tunaoibebesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama hizi za umeme *fixed charge* ni shilingi bilioni 3 kwa mwezi kwa mwaka mzima ni bilioni 36. *Life* ya Mkataba ule ni miaka 20 sasa sijui kama hiyo *fixed charge* ni kwa ajili ya *life* nzima ya Mkataba ule wa miaka 20 kama ni hivyo basi utakuta tunabeba mzigo *at the end of the day* hatuna sababu ya kubeba mizigo ya namna hiyo, tufanye hatua za dharura na za haraka za ku- *arrest the situation* na zipo njia. Njia tu ya kusukuma mazungumzo kwa nguvu kabisa ya kuhakikisha kwamba tunanunua mitambo ile kutoka kwa hao waliowekeza tuachane nao tuanze upya na kujipanga na kutumia mitambo yenyewe.

Sasa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili ulivalia njuga wanasema katika Ofisi yako kuna *fast track,* kuna *slow track,* hii uiweke kwenye *emergency track.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengine mengi huko ndani ya Mkataba huu. Wanasema ule umeme unaozalishwa pale na ule ambao unaingia kwenye gridi yetu kuna asilimia kati ya 15 mpaka 30 ya umeme ambao unapotea njiani, lakini tunakuwa *billed* pamoja na ule umeme ambao unapotea hapo *on transmission.*

Sasa nasema haya Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba uyakalie kwa uzito wake, yafanyieni kazi na mimi ninaamini wakati huu ndiyo muafaka wa kuisimamia hiyo na mkija kwenye *Mini-Budget* hapa mtuambie kwamba hili tatizo mmeweza kulidhibiti na mimi naamini kwa sababu mna hiyo historia ya kufanya makubwa na ya kihistoria mpaka sasa hivi mtatufikisha hapo pazuri.

La mwisho kabisa kabla muda wangu haujaisha. Arusha pia Geneva ya Afrika inaomba kuwa Jiji, tunaomba hilo mlikamilishe kabla ya mwisho wa mwaka huu tuwe Jiji la Arusha, tuweze kupanga maeneo yetu kama tunavyotaka kuyapanga. Ukifanya yote hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi ninaamini itakapofika mwaka 2005 utazidi kupeta zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hiyo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu. Kwanza, nianze kwa kuwapa pole sana wenzetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Vile vile Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan kwa kufiwa na mtoto wake. Vile vile napenda niwape pole wenzetu waliopata ajali Mheshimiwa Anne Kilango, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki. Mheshimiwa Danhi Makanga, mimi namwona ni kama shujaa kwa sababu namfananisha kama Bwana mmoja alikuwa na kichaa akamwona kobe anaharibu mazao, akamwambia kobe nikupe adhabu gani, kobe akasema nitupe kwenye maji, sasa kumtupa kwenye maji kumbe ni mahali pazuri zaidi kwa kuwa kobe huishi vema majini kuliko nchi kavu. Sasa Mheshimiwa Danhi Makanga yuko CCM, anaishi mahali pazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii kwa upande wa Upinzani kwa kweli imetoa fundisho kwamba Vyama vya Siasa viendeshwe kwa kidemokrasia na hii itazidi zaidi kuweza kujenga imani kwa wananchi. Mheshimiwa Danhi Makanga, ameonyesha umahiri mzuri sana na kwa kweli tulikuwa tunamtamani kwamba ni namba nzuri akicheza katika uwanja wa CCM. Kwa hiyo, Mheshimiwa Danhi Makanga karibu sana. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, napenda nimpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri yeye pamoja na wasaidizi wake ni kazi nzuri ya Awamu ya Tatu, wanafanya vizuri kwa kweli. Mtu mmoja hawezi kufanya kazi vizuri namna hii. Mafanikio tunayoyaona namna hii yametokana na umoja walionao Waheshimiwa Mawaziri wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa sababu yote mazuri tunayoyaona kunakuwa na kasoro kwa sababu kuna mazuri unaona kunakuwa na kasoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli timu nzuri yote inafanya vizuri, japokuwa niseme kwamba kuna baadhi kama Askari wawili, watatu wa miavuli wao bado wamening'inia kule juu, lakini wengi wanafanya kazi nzuri na tunaziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulisema hili napenda nisema kwamba sitaweza kuwataja, lakini nasema kwamba kazi nzuri hamwezi kuifanya wote mkafanana, hata vidole vinapishana, kuna watu warefu, kuna wembamba, kuna wanene na kadhalika. Kwa hiyo, kwa maumbile ya namna hiyo yanatoa hata tofauti ya utendaji kazi. Lakini kazi nzima inafanywa vizuri na Serikali ya Awamu ya Tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwasifu vizuri sana kuna kasoro ndogo ndogo ambazo ni vyema sisi tujaribu kama kuziainisha na kuweza kusaidia. Nisingependa kurudia ambayo wenzangu wameshayasema, lakini kuna suala ambalo tunapaswa kulipa kipaumbele ni la kilimo. Kwa sababu kilimo siku zote tumekuwa tukiimba ni uti wa mgongo, ni sekta kiongozi, sijui kwa vile uti wa mgongo uko nyuma ndiyo maana hauonekani basi unabaki hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Mtanzania ambaye anaishi kijijini na anategemea kilimo kwa asilimia 80 ni vyema tuweze kuwapatia uwezo. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula najua angependa kufanya kazi vizuri sana, lakini vile vile tuangalie uwezo wa Serikali tumemwezesha namna gani? Nchi yetu ni kubwa tukilaumu sana hatutasaidia lakini tumpe mkakati mbadala kwamba tungependa kuona kwamba tunapoazimia katika Bunge la Bajeti mwaka 2004 tumepanga ufafanue kilimo cha umwagiliaji au tulime kwa mpangilio huu, tuweze kuleta pembejeo, basi kazi iweze kufuatiliwa vizuri zaidi na iweze kuzaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu uchumi wetu unategemea sana kilimo. Pamoja na hayo kilimo hakiwezi kwenda sambamba na mambo mengine. Lazima tukumbuke mambo ya umeme watu wa nishati ni muhimu sana. Sasa unakuta *TANESCO* wanashindwa kufanya kazi za kusambaza umeme vijijini hawana fedha. Lakini ukisema unazungumzia nishati lazima uzungumzie maliasili, wananchi wasipoweza kupata nishati ya umeme watakata miti tunaharibu mazingira na tunaharibu maliasili. Kwa hiyo, sekta hizi zote lazima ziende sambamba. Hii ningependa kusema kwamba tungependa kuwa mtazamo mzuri sasa wa kuainisha Bajeti yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wako hapa kwa nyuma wanasikiliza kwenye *gallery* pale. Lakini Bajeti hii sijui kama inaingia kwenye *action plan* kwa sababu tutatoka hapa watarudi mikoani mwao utekelezaji wake unaanza kutofautiana kutoka mkoa hadi mkoa. Lakini tungekuwa tuna *team work* kwamba baada ya Bajeti kupita hapa kila mikoa ukaweza kuwa na *action plan* na wakafuatilia vizuri sana utekelezaji wa Bajeti hizi na *format* nzima ya utendaji kazi ikawa katika mtiririko mzuri naamini kwamba tutakuwa tume-*achive* kitu kizuri sana na sio kutelekeza Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanapenda kusema kwamba Bajeti ni ya porojo, sio porojo, hapana. Sasa hivi tuna fedha. Huko nyuma tulikuwa na porojo sana. Mheshimiwa Basil Mramba amejitahidi kuanza kurekebisha Hazina yake, amedhibiti mapato, amekusanya mapato, anakuja hapa anatuambia kwamba tusiwe na wasi wasi, mnaona sasa tunataka nini zaidi. Waziri wa Fedha anasema kwamba lazima tuendelee. Hata kama ni kula majani tutaendelea. Ndiyo!!.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda niwapongeze sana lakini bila ya kuwa na *system* ya kufanya kazi bado tutakuwa hatutekelezi majukumu yetu vizuri zaidi. Mawaziri wote hapa ni wazuri najua wananiangalia vizuri lakini wote ni wazuri hakuna mbaya. Nikianza kuainisha mmoja mmoja Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi ukimwona jinsi alivyo na Wizara yake ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wanafanya vizuri sana, hakuna matatizo. Tunampongeza na lazima tujenge utamaduni, mtu akifanya vizuri tumpongeze sio kumponda kwamba aah, mtu akifanya vizuri tumpongeze, akifanya vibaya tumkosoe na tumsahihishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mimi ambacho ningependa kuzungumzia ni suala la Uwanja wa Ndege Mwanza. Mwanza ni Jiji, ni kitivo kikubwa sana cha biashara kwa Ukanda wa Ziwa na katika nchi za Maziwa Makuu. Ningependa sana Mheshimiwa

Profesa Mark Mwandosya, anafanya kazi nzuri sana amejitahidi sana. Kazi zake ni nzuri kwa kweli kwa Wizara yake na ameanza mkakati wa kujenga Uwanja wa Mwanza uwe kwenye hadhi ya Kimataifa. Ni kitu ambacho ningeomba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi ni kwamba azidi kuweka mkazo. Tusingependa hadithi hizi zikabaki kuwa zina-*hang hang.* Ni mchapakazi mzuri sana na naamini kwamba kabisa azma yake ya kufanya Uwanja wa Ndege wa Mwanza uwe wa Kimataifa itatimia. Wanamwanza tunakushukuruni sana kwa kazi hiyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo napenda kulizungumzia licha ya Uwanja wa Ndege wa Mwanza ni suala la mafao ya wastaafu. Unakuta kwamba mstaafu anapokuwa mtumishi yuko chini ya Utumishi anapostaafu anapelekwa Hazina.

Mimi ningeshauri kwamba kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Hazina, ile kazi ya suala la Utumishi wangeliangalia kwa makini zaidi. Ningeshauri kwamba suala la pensheni zote za watumishi wastaafu ziende Wizara ya Utumishi ambako kuna kumbukumbu za kutosha ili kusudi wazee wetu hawa wanapostaafu kazi walipwe mafao yao kwa muda wanaostahili. Sasa hivi ni usumbufu mkubwa sana. Kuna watumishi wa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kati wanadai, kuna wazee wengine wamestaafu tena kule Vijijini wanadai kila leo. Wakienda Hazina unaambiwa hakuna takwimu, mara hakuna *file,* mara hakuna nini. Sasa yote haya ni usumbufu ambao hauna maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependekeza kwamba bado sasa hivi tuna mambo ya mtandao ni vyema zaidi takwimu zote hizi zikawekwa mahali pamoja iwe *one stop centre* ili kusudi watumishi watakapokuwa wanadai madai yao wafike kama ni Wizara ya Utumishi basi waweze kupata mafao yao bila ya kucheleweshewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili ningependa Mheshimiwa Basil Mramba, ajaribu kumsaidia Mheshimiwa Mary Nagu , kwa sababu imekuwa ni kero na tusingependa kuendelea na kero hii wakati mwaka kesho tunaingia kwenye uwanja wa mapambano. Wazee wetu tuwaenzi wamefanya kazi nzuri ya kutumikia nchi hii na wanastahili vile vile kuweza kuheshimiwa kwa kazi hiyo na mchango wao katika kujenga kazi hii.

Suala lingine ambalo napenda nizungumzie hapa ni suala la upanuzi wa demokrasia. Tumekuwa mara nyingi tukisema kwamba asubuhi hapa kuna swali limeulizwa kwamba kwa nini Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa asiteue Madiwani kwa kila Halmashauri waweze kusaidia katika Halmashauri zile. Majibu ikaonekana kwamba hapana. Katiba imeshafuta hilo na mwenye mamlaka ya Katiba sasa hivi ni Mheshimiwa Rais peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawa wateule wanaoteuliwa sasa na Mheshimiwa Rais wanafanya kazi gani na wanawajibika vipi. Mheshimiwa Rais ana kazi nyingi sana, wanasema jimbo lao ni Ikulu. Sasa Ikulu nani wanaripoti kwake. Mimi ambacho ningesema ni kwamba kwa wale *Constitutional Officers* wote waweze kuteuliwa na Mheshimiwa kama ni Rais apewe Mamlaka hayo kuweza kuongeza wigo wa kuchagua watu anaowataka lakini waletwe Bungeni hapa wathibitishwe na Bunge ili

uwajibikaji wao uweze kuwa umepata *back up* ya kidemokrasia. Tusiue demokrasia. Mimi nafasi kumi za eti kuteua watu sipingi nasema ni sahihi zaidi kwa sababu anahitaji kuwapa watu kumsaidia katika kuleta mawazo ya Kitaifa zaidi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini vile vile pengine tutoe nafasi nzuri zaidi kwa kuwawajibisha watu hawa. Leo hii tunakuwa tuna watu kama Msajili wa Vyama vya Siasa. Huyu mtu ameteuliwa, amepewa ofisi na anashughulikia maslahi ya nchi lakini sasa tunamwajibisha namna gani akifanya makosa.

Mimi ningependa kwamba Bunge lizidi kupewa Mamlaka na katika Katiba marekebisho yanakuja hili suala tujaribu kuliangalia kwa makini zaidi. Pengine hata nafasi tano za Madiwani kule watasaidia ku-*balance* na kuweza kutoa ushauri mzuri kwenye Halmashauri zetu watu ambao pengine hawawezi kugombea nafasi za Udiwani lakini wana uwezo mzuri wa kufikisha mawazo yao katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ningependa kuzungumzia suala la utalii. Katika Ukanda wa Ziwa kuna utalii mkubwa sana. Ile *Western Corridor* inayotoka Arusha kuja Mwanza, mimi ningependa hiyo iweze kupewa msukumo wa pekee. Msukumo huu utasaidia sana kufungua nchi yetu. Leo hii tunasema tunajenga barabara safi sana, tunafanya sekta za maji Mheshimiwa Edward Lowassa ametuletea maji kutoka Ziwa Victoria tulishayakosa miaka nenda rudi, Shinyanga watakunywa sasa hivi na shughuli itaendelea kule Shinyanga. Lakini vile vile tujaribu kufufua vitu vingine ambavyo vitasaidia kuweza kuendeleza uchumi wa nchi hii. Hatutegemei kilimo lakini sekta ya utalii ni sekta muhimu sana. Kule katika ukanda wa *Western Corridor* ni karibu sana mtu akitua Mwanza kwa ndege kwenda Mbuga ya Serengeti ni kilomita 135 ambapo ni karibu sana. Kando kando kuna ufukwe mzuri sana ambao ungeweza kuchochea ujenzi wa mahoteli na kuongeza ajira na kuongeza Pato kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mimi ningependa katika mkakati huu hili suala tujaribu kulipatia kipaumbele na Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie kwa sababu yeye ni kiongozi na amefanya kazi zake vizuri sana, lakini vile vile bado tunahitaji azidi kuongoza akiwa kama kiranja wa Mawaziri wenzake. Nchi hii ni yetu sote hakuna mwenye hatimiliki. Kilichopo hapa tunagawana wote kwa uwiano sawa. Kinacholeta kugomba ni kwamba kuna baadhi ya sehemu zinaonekana kwamba zinapendelewa zaidi katika kugawana keki ya Taifa. Labda zina hatimiliki lakini naamini kwamba wote tuna hatimiliki ya nchi hii. Kwa hiyo, mimi ningependa sana suala hili tujaribu kulipatia kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho ambalo ningependa kumsifu tena Mheshimiwa Basil Mramba kwa sababu mimi nilidhani Mheshimiwa Basil Mramba, ukimwona jinsi alivyo na anayoyafanya havifanani lakini kwa kweli kazi yake ni kubwa sana. Wizara ya Fedha huyu mzee naona sasa anaipeleka vizuri. Kwa sababu Mapinduzi makubwa na uwezo wote huo, Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli, anajenga barabara ni kwa sababu ya Mheshimiwa Basil Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwona Mheshimiwa Gideon Cheyo pale anapima viwanja kwa sababu ya Mheshimiwa Basil Mramba. Ukimwona Mheshimiwa Wilson Masilingi anatamba na rushwa yake ni kwa sababu ya Mheshimiwa Basil Mramba. Sasa ni lazima tumpongeze huyu mzee. Ukiona mambo ya Afya ya Mheshimiwa Anna Abdallah anakwenda vizuri ni shauri ya Mheshimiwa Basil Mramba. Ukimwona Mheshimiwa Andrew Chenge anakaa ametulia hapa ni kwa sababu ya Mheshimiwa Basil Mramba. Sasa na Bunge kwenda vizuri ni kwa sababu ya Mheshimiwa Basil Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Watanzania tujenge utamaduni wa kuwapongeza watu wanaofanya vizuri kwa sababu hatuko hapa kwa ajili ya kukosoana peke yake na wenzetu huku wanaopiga porojo, tungependa kuwashauri kwamba pale ambapo Serikali imefanya vizuri muwe mstari wa mbele kuunga juhudi za Serikali sio kupinga kila kitu. Najua ninyi *agenda* yenu mnasema kwamba iweje iweje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu hivi sasa kwa mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kutokana na kufiwa na baba yao na Mwenyezi Mungu aiweke pema roho ya marehemu peponi. *Amin.*

Vile vile niwape pole Wabunge wenzetu wote ambao walipata maafa ya ajali za barabarani au kwa kuvamiwa na majambazi. Hiyo ni *challenge* pia kwa upande wetu na kwa upande wa Serikali kuona hili tatizo la ujambazi katika nchi yetu na pia matatizo ya ajali nini cha kufanya ili kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke hapo pia nisimsahau Mheshimiwa Danhi Makanga, nimpongeze kwa kutuletea ushindi Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja katika maeneo ambayo nilikuwa nakusudia kuchangia ambayo naamini yataweza kusaidia katika hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa natanguliza masikitiko yangu madogo. Wenzetu wa Kambi ya Upinzani waliowasilisha pale maoni yao lakini haya maoni sijui yataisaidiaje hotuba hii. Kwa sababu naona yalirushwa makavu makavu hivi, hayakulainishwa na chochote kiasi ambacho yameacha lawama tupu bila kutoa ushauri nini kifanyike. Zaidi ya hayo kulikuwa na kejeli za ajabu ajabu.

Kwa mfano wanasema mtu mzima atishiwi nyau, danganya toto, kuuziwa mbuzi kwenye gunia, Serikali kung’aka mithili ya koboko na maneno mengine mengi ya ajabu. Pia kuna kejeli nyingine katika ukurasa wa 16 wanasema: “Enzi za kuamini kuwa kuna

mtu aliyeumbwa kutawala milele au riwaya za akina Thabiti Kombo eti mtu kutoka eneo fulani hawezi kutawala Zanzibar zimepitwa na wakati." Mimi nadhani hii hoja ndiyo imepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mzee aliyetajwa hapa ni muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa kama riwaya zao zimepitwa na wakati kwa mtu ambaye kabla hajafika Zanzibar anaweza kidogo akajiuliza riwaya hizo zipi. Lakini riwaya zao wao hawa ni yale majengo ya Michenzani, Kilimani, kuweka elimu bila malipo. Sasa hizo ndizo kazi walizozifanya hawa na zile nyumba za Michenzani zote zile zilitolewa bure hakuna ambaye amenunua zile. Sasa baadhi ziko mikononi mwa Serikali mpaka hii leo lakini hakuna hata moja sijui kodi yake kwa uhakika lakini inayofikia kodi ya shilingi 10,000/= nyumba zile mpaka hii leo tunapozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama riwaya hizo zimepitwa na wakati nadhani anayezungumza yeye atakuwa amesha-*expire*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu hawa Rais Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi aliwahi kuwaambia. Rais Mstaafu Mzee Mwinyi alisema "Ukitaka kutukana mbele za watu kwanza uangalie hakuna aliyekuzidi."

Sasa athari iliyopo hapa wanatukana ovyo ovyo hawaangalii kuna watu wazima humu, mtakuja tukana baba zenu hatari iliyoje. Sasa busara ni vyema itawale katika kusema. Kwa hiyo, hakuna suala la kutishiwa nyau, ni kuelezwa hali halisi ilivyo. Sasa mtu mzima anasema anatishwa mimi naona kwamba hapa kuna utu uzima labda tofauti iliyopo kuna wengine wamezaliwa zamani lakini bado hawajawa watu wazima. Sasa ipo tofauti kama umezaliwa zamani na kuwa mtu mzima, utu uzima busara. Sasa bora niondoke hapo na niendelee na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee katika eneo la kukuza uchumi na kupambana na umaskini. Katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea mengi mikakati ambayo ipo katika kupambana na hali hii. Serikali imechukua hatua mbalimbali. Kuna mikopo midogo midogo mingi ambayo inatolewa hivi sasa kwa madhumuni ya kunyanyua hali za wananchi. Lakini vile vile tuangalie sasa hivi kuna wahitimu wa Vyuo Vikuu ndani ya Tanzania sasa hivi hawana ajira.

Sasa hao kwa kusema mikopo midogo midogo hatuwasaidii sana hawa kwa sababu hii mikopo midogo midogo itawasaidia hawa akinamama, tuseme labda hizi ajira ndogo kina mama ntilie, biashara ndogo ndogo, hawa wanaoranda na maduka mgongoni, hizi zitawasaidia mikopo midogo midogo. Lakini hao ni kiungo muhimu sana katika uchumi wa nchi. Kwa hiyo, kungekuwa na utaratibu wa mikopo hawa wakaingia katika sekta ambazo zitawafanya watakuwa ni tegemezi katika uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano sekta za utalii waweze kushirikiana kujenga mahoteli, haitapendeza kuona katika fukwe zetu zote zinachukuliwa na wageni kwa asilimia kubwa ambapo wenyeji wakawa hawana nafasi kuendeleza uwekezaji katika maeneo kama hayo. Kwa hiyo, kutakapokuwa na mikopo ya muda mrefu na mikopo

mikubwa mikubwa hiyo ndiyo itakayosaidia kukuza ajira kwa watu wetu, kwanza kuwa na *investors* ambao ni wazalendo ambapo kutakuwa kuna uhakika kwamba asilimia mia moja la pato pale halitatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sekta zile zitaajiri na wazalendo wengi pia itasaidia kwa kiwango kikubwa sana kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ukurasa 24 ameelekeza kwamba masuala mengi ya kuelezea kuhusu utaratibu ule *I mean* kuhusiana na namna zile harakati za kupunguza umaskini pia hapa amezizungumzia. Pia amesisitiza kwamba tubadilike hata katika utaratibu wetu wa kilimo tutumie teknolojia ya kisasa. Lakini kwa huyu Mtanzania wa kawaida wa Kijijini ili atumie teknolojia ya kisasa maana yake aingie kwenye trekta na vifaa vingine vya kisasa. Lakini katika hali ya sasa hivi hawa hawawezi kubadilika lazima wasaidiwe kubadilika ndivyo ambavyo walivyofanya nchi za wenzetu miongoni mwa nchi za ulimwengu wa tatu wanasaidia watu wao ili waweze kubadilika wenyewe kwa wenyewe hawawezi kubadilika. Kwanza kuna wengine hata wazo la kufikiria vitu hivyo bado ni geni vichwani mwao. Kwa hiyo, tubadilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali ya sasa hivi tuliyonayo mifumo yetu ya Benki nayo pia haiwezi kutubadilisha sana kwa sababu ukiangalia taratibu zao za mikopo pia nazo hazieleweki vyema au ni mikopo zaidi inalenga katika mikopo ya muda mfupi. Lakini vile vile katika kitabu hiki kinachozungumzia *Monetary Policy Statement* nikiangalia ukurasa 28 inapozungumzia *credit policy* inazungumzia, naomba kunukuu hapo: *"The Bank of Tanzania in collaboration with Government will continue to follow up only restructuring and all privatisation of remaining state on bank including NMB, The People's Bank of Zanzibar, Tanzania Postal Bank and Tanzania Investment Bank particularly with the view to further improving to availability of credit to key sector of the economy."*

Vipi hayo yatafikiwa? Tunaelekea kwanza tunasema kuziboresha au kuzibinafsisha. *NMB* tumeshabinafsisha, nadhani katika zile zitakuwa zimebakia tatu sasa hatujui mwelekeo hapa kwamba nazo tunazibinafsisha au vipi. Kama tutabinafsisha vipi zitachangia hiyo *improvement* ya *economy* kwa hizo njia za *credit* tutatoa vipi hizo *credit.* Ni vyema basi tunafikiria sasa hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyozungumzia kubadilisha hizi Benki. Kuna Benki zinataka kuanzishwa kwa madhumuni ya mikopo kwa wakulima kwa nini tusibadilishe hizi tukazielekeza huko. Ukianzisha Benki leo mpaka ifike huko chini kabisa kwa mwananchi ukiondoa Dar es Salaam na hii miji mikubwa mikubwa huku kwingine zitafika lini. Nadhani hapa kidogo tunajigongagonga ni vyema tukaweka sawa hapa tutumie Benki zilizopo kuzibadilisha ili hilo lengo liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hizi Benki hata tukiangalia ule utaratibu wa riba katika Mabenki ambayo tuliyonayo sasa hivi nataka kutoa mifano ambayo inaonesha katika hali ya sasa hivi ya Benki zetu si rahisi kubadilisha maisha ya Mtanzania. Katika kitabu hiki cha *Bank of Tanzania* ili toleo la Machi, 2003 ukurasa wa 17 nime-*note* pale

naomba kunukuu: *"Average interest rate quoted by Commercial Bank or domestically insemination."*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitanukuu kipande cha pili ambacho kinachoonyesha ile mikopo wanayotoa na *interests* wanazotoza: *"Landing rates quoted by the Commercial Bank on all domestic currency denominated loans decline expect those for short loans of up to one year which increased from 15.9 percent in December, 2002 to 16.4 percent in March, 2003."*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ambapo wale wanaoweka fedha zao wao *interests* wanayopewa ni 3*% up to 2.5% only.* Sasa wao wanapotoa mikopo hizo Benki ni hizo *interests* ambazo nilizozitaja kwa kweli hakuna ule uwiano na kwa hali hi sidhani kwamba hizi Benki katika hali ya sasa hivi zinaweza kutukwamua vinginevyo tubadilishe mfumo. Kwa hiyo, hilo nalo ningeliomba ukalipekua na kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapobadilika hivyo ndipo itaweza Tanzania kuingia kwa mbwembwe katika yale mashindano ndani ya *East African Community* pale kuna maelekeo mengi tu kuna *Custom Union, Common Market Free Movement, Monetary Union Political,* vinginevyo tunaweza tukajikuta Watanzania tukawa manamba wa watu hawa jirani zetu. Kwa hiyo, ni vyema tubadilishe mifumo yetu kuwawezesha watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi ni soko, soko ni watu kwa hiyo, tutakapokwenda huko maana yake tumeingia kwenye soko pana zaidi lakini je, tunaweza kushindana kwenye soko? Ukienda kwenye soko huna cha kuuza itabidi mwisho wake utauzwa wewe mwenyewe uliokwenda kwenye soko. Kwa hiyo, tubadilike tusije tukaenda kuuzwa sisi ndani ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naondoke hapo. Nchi yetu ina bahati ya kuwa na madini. Katika mtiririko huu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameahidi kwamba Serikali itashughulikia hili tatizo linalolalamikiwa kuhusu madini, lakini bado tuna tatizo lingine hili la mafuta. Mafuta tumo katika tafiti lakini bado inaelekea kwamba bado Serikali zetu hazijafika mahali pazuri pa makubaliano. Nina mifano hai ambayo imezungumzwa na kulalamikiwa na Waheshimiwa Wabunge lakini majibu ambayo huwa yanajibiwa kwa kweli bado hayajatufikisha pazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano katika kitabu hiki ambacho Mheshimiwa Daniel Yona alikiwakilisha katika Bunge hili. Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, aliuliza Serikali ya Muungano inafanya maandalizi ya kuanza kutumia gesi ya Songosongo lakini hakuna kiongozi yeyote kutoka Serikali ya Zanzibar ambaye ameshirikishwa katika suala hili angalau kwa mazungumzo ya awali.

Mheshimiwa Waziri alijibu hivi: "Taarifa ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi yaliyowasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri mara tatu na kwa maana hiyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilishirikishwa." Sawa, sasa tujiulize Mawaziri wangapi wanaingia

katika Baraza la Mawaziri, ni Rais wa Zanzibar anaingia. Sasa mtendaji sio Rais katika suala hili. Waziri na Waziri ndio wazungumze.

Sasa tatizo limekuja Waziri wa Zanzibar hivi karibuni mwezi Mei tulikutana nao tukazungumza kuhusu suala hili la mafuta mnafanya nini, mnakwenda kwendaje, anasema nimepokea barua kutoka Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona. Lakini anasema mimi nimepokea barua nifanye nini na barua inazungumza ni kama ruhusa kuanza utafiti ule uchimbaji ile Kampuni nadhani *Shell.* Anasema mimi nimesitisha nataka kujua nitakapokuja kuulizwa nitajibu nini na hawa wananchi wa Zanzibar, nini kinaendelea.

Sasa ninachotaka kukizungumza hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu tuna tatizo la ile mikutano ya ushirikiano. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais alizungumza katika hotuba yake ya 2003/2004.

Nakwenda mbio mbio niwahi muda alisema hivi, Ushirikiano umeongezeka kati ya Wizara za Muungano za SMZ na SMT, Wizara hizo ni Afya, Ustawi wa Jamii na nyingine chungu nzima ametaja ambapo ratiba imepangwa kukutana angalau mara mbili kwa mwaka tayari vimeshafanyika vikao 15 katika vikao hivi masuala mbalimbali ya ushirikiano yamejadiliwa ikiwa ni pamoja na kuanisha sera, kubadilishana utaalamu, ushirikiano na SMZ katika Mikutano ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haya yanakwenda sawa sawa tatizo liko wapi? Sasa kwa hiyo, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu suala hili uliingilie kati na halafu ni vizuri utuarifu Wabunge kama vikao vilifanyika vingapi, wapi na kilijadiliwa nini, mlikubaliana nini, utekelezaji ukoje? Nadhani tutafika mahali na sisi Waheshimiwa Wabunge tunataka tusaidie hatupendi kuona hii mivutano ambayo haimsaidii yoyote kwa sababu unapoanza kuzungumzia kitu madini ambayo hujayachimba unaanza kujadili unavutana unagombea nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kuweza kutoa pole nyingi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pia nitoe pole nyingi kwa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kwa kuvamiwa na majambazi pale Morogoro na pia nitoe pole nyingine kwa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa ajali mbaya ambayo ameipata, tunamwombea Mwenyezi Mungu amsaidie ili apone haraka kwa sababu tunahitaji mchango wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane moja kwa moja na wenzangu kuipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kweli hotuba yake imekuwa nzuri ambayo imeainishwa vizuri na iko katika mpango mzuri. Lakini kabla ya kuanza kuchangia hotuba hii kwa kuwa sikupata nafasi ya kuchangia katika hotuba ya

Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji basi nianzie huko.

Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo ameweza kukusanya kodi kwa kutumia Idara ya *TRA* vizuri. Wamefanya kazi nzuri kazi ambayo Watanzania leo tunajidai. Lakini kikubwa kabisa niseme wazi kwamba wale watu wamefanya vizuri. *TRA* wamefanya vizuri na tuwe na utaratibu wa kuwapongeza. Mtu anapofanya vizuri lazima apongezwe pale pale na ikiwezekana apewe motisha kwa sababu kawaida sisi Watanzania huwa tunamwaga pongezi nyingi mtu anapokuwa anazikwa hasikii amefariki, unamwagia sifa nyingi sana. Lakini hawa kwa kuwa wako hai basi tuwape motisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa motisha, kuna mwenzetu mmoja pale Ubungo aliweza kuokoa nchi hii ili isiteketee kwa moto. Lakini kwa taarifa ambazo sina hakika nazo inasemekana yule bwana amepata cheti kizuri sana na shilingi 200,000/=. Kwa kweli yeye nafikiri afikiriwe, ile inatia moyo kwa sababu yule bwana aliingia katikati ya moto na kuweza kuokoa Watanzania. Kwa hiyo, kuwe na utaratibu wa kupeana motisha ili tuwe na moyo wa kuipenda nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu ubinafsishaji. Leo hii kama unasema kwamba wewe hujaona faida ya ubinafsishaji, mimi nakufananisha kabisa na yule mtu ambaye alikwenda kwenye baa na gari yake akai-*park* nje. Akaingia kunywa pombe, alivyorudi akaingia kwenye gari akapiga simu Polisi kwamba ameibiwa usukani, *dash board* pamoja na redio. Kumbe aliingia mlango wa nyuma. Kwa hiyo, wale ambao hawaoni yaliyofanyika na Serikali hii ya CCM basi nataka niwaambie kwamba wameingia mlango wa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo imefanywa na Serikali kule Wilaya ya Kilolo ukiwaambia watu faida ya ubinafsishaji wanaielewa, lakini kama punguzo la mbolea halitaonekana hawataelewa maana ya ubinafsishaji. Kwa hiyo, ubinafsishaji ungelenga sehemu za uzalishaji wa kilimo kwenye kupunguza bei za pembejeo.

Mimi naamini kabisa Serikali ilikuwa na nia nzuri lakini haikuwa imejiandaa. Nitatoa mfano mwingine, kuna mtu mmoja ni rafiki yangu ambaye yuko hapa siwezi kumtaja. Alishtukizwa kuja kuwa mgeni rasmi kwenye semina fulani, sasa akawa ameomba kujiandaa kwa sababu alikuwa hajajiandaa. Lakini akatoka nje, alivyotoka nje anaandaa hotuba anaandika andika kuna Mheshimiwa fulani siwezi kumtaja pia ambaye ni mama akamkuta akamwuliza wewe vipi mbona unahangaika? Hii semina ndogo tu, lakini una wasiwasi! Akasema, aah mimi bwana hivi vitu nimezoea sana bwana, mimi ni mwanamme wa shoka, huku anatengeneza tengeneza tai yake. Akamwambia tena, mimi nafikiri umechanganyikiwa, mbona sasa uko huku kwenye choo cha akinamama? Kumbe jamaa alichanganyikiwa akasahau hata choo, akaingia kwenye choo kingine. Kwa hiyo, ni vizuri tukaweka maandalizi mazuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia habari ya ongezeko la kodi. Tumeongeza bei ya vinywaji *(soft drinks)* kwa mfano, soda. Nafikiri suala hilo Mheshimiwa Waziri angeliangalia vizuri kwa sababu kwa mfano soda imeongezeka asilimia 6.7. Sasa asilimia 6.7 maana yake soda mpaka ikifika kule Siha au kule Kilolo itauzwa kwa shilingi 700/=. Kwa hiyo, ni vizuri tukaiangalia hiyo sehemu kwa sababu wanaokunywa soda ni watoto wadogo, wazee, wagonjwa na wale watu ambao wana kipato cha chini. Maana yake ni kwamba, baadaye watu watajikita kwenda kunywa ulanzi hasa kule kwetu wakaacha kunywa soda ambazo kama bei ingekuwa chini watu wangekunywa sana soda na Serikali ingekusanya sana kodi.

Sasa matokeo yake kwa ongezeko hilo watu hawatakunywa soda na Serikali haitakusanya kodi, uzalishaji utapungua na wafanyakazi watapunguzwa. Kwa hiyo, hali hiyo itatuathiri kwa aina fulani. Nafikiri wangeweka *flat rate* kwenye bei kama walivyoweka kwenye bia, *five percent, five percent, five percent*, ingeweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoulizwa na Wananchi wa Kilolo kwa nini tumefutiwa kodi, moja ya kigezo nilichokisema ni kwamba suala la ubinafsishaji tumelifanya vizuri na nikawaambia kwamba tofauti ile ya kodi kama ambavyo Mheshimiwa amekuwa akituambia italipiwa na watu kama *Tanzania Breweries* ambao wao sasa wanatuingizia mapesa mengi sana.

Lakini sasa kuna suala la sheria, sheria ya muda wa kunywa hicho kinywaji chenyewe (bia) irekebishwe kwa sababu sheria zimepitwa na wakati. Sheria ya muda wa kupata kile kinywaji ilifanyiwa *amendment* mwaka 1971. Kwa hiyo, ili tuendelee kukusanya kodi kwa uhakika na ili Wananchi wetu wasilipe kodi tena, maana tulizipitia zile sheria ili watu wawe huru wanywe kama wanavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao nawalinganisha kabisa na kuku anayetaga mayai ya dhahabu. Ukishapata bahati ya kupata kuku anayetaga mayai ya dhahabu hutakiwi kumsumbua sumbua kwa sababu ataacha kutaga. Kwa kuwa sisi wanaotutagia mayai ya dhahabu ni wanywaji, basi tusiwabughudhi, waache wanywe. Sisi kazi yetu kubwa itakuwa ni ulinzi. Nina uhakika kabisa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kazi hiyo anaiweza, majambazi sasa hivi haponi mtu, wanashughulikiwa kikamilifu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitoe shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamshukuru kwa sababu ameamua kutoa *helicopter* ikae Kilolo kwa kazi maalum, lakini amesahau kwamba Wilaya ya Kilolo haina gari hata moja. Nashukuru pamoja na upelekaji wa *helicopter* ile kwenda kulinda lile eneo, siwezi kusema ni la nini, lakini basi atoe na gari angalau moja au mbili ziende zikakae kule ili kazi ile ifanyike kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nitoe shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuwa sisi tulikuwa tunaishi kwa matumaini, lakini sasa tunaishi kwa uhakika kwa sababu ameniambia kwamba si muda mrefu

kutakuwa na simu pale Ilula na Mahenge. Kwa hiyo, ni lazima nimshukuru maana moyo usio na shukrani hukausha mema yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Benki ya Maendeleo. Pamoja na kazi nzuri yote ambayo imefanyika, kama benki hii haitaanzishwa mapema itakuwa bure hata kwa ule ufutaji wa kodi za leseni ya biashara. Inabidi tufanye jitihada za hali ya juu ili wale watu wenye kipato kidogo nao basi waweze kukopa, maana bila kukopa huwezi kupata maendeleo. Kwa hiyo, hilo lifanyike mapema ili tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu suala la ukame. Hakuna kitu kibaya kama tukiendelea kuwa omba omba kwenye chakula. Sisi Watanzania hatuna sababu ya kuomba chakula kwa sababu tuna maeneo mazuri sana. Mikoa ile ambayo imepewa ruzuku ni Mikoa ambayo kwa kawaida ni ya mvua. Kwa hiyo, suala ni kuimarisha zile barabara. Tukiimarisha barabara zile tutakuwa tumefungua jambo kubwa kabisa katika kilimo na nina hakika kabisa njaa haitakuwepo. Kwa mfano, barabara za Wilaya ya Kilolo, barabara ya kutoka Ilula, Mlafu, Wotaisori, Mkalanga, Ipalama, Kising'a na Kilolo ikifunguliwa mambo yatakuwa mazuri. Pia, barabara ya Dabaga, Idete, Muhanga, Mbingu kuelekea Morogoro ikifunguliwa mambo yatakuwa mazuri pia. Tutazalisha chakula cha kutosha na kwa kweli njaa haitakuwepo tena. Pia, barabara ya Boma la Ng'ombe, Indingula, Masisiwe na Idete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo ikifanyika nakuhakikishia njaa itakuwa hamna, hata kule Tunduru kama ukipata njaa tutakupa tu chakula. Pia, niishukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa suala la kutoa chakula wakati wa njaa, kwa sababu kwa kweli mtu akiwa na njaa akili huwa haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa nitoe shukrani ni kwamba, nawashukuru sana watu wa *SUA* kwa kuamua kufanya semina za kuondoa umaskini kwenye Wilaya ya Kilolo. Lakini ushauri wangu ni kwamba, ni vizuri sasa badala ya kutoa zile semina basi wangejitika moja kwa moja kwenda kupeleka zile fedha kwa Wananchi kupitia barabara ziende kwenye mpango wa barabara kama vile *TASAF* wanavyofanya kazi nzuri, wakapitisha pia kwenye ruzuku ikaenda kama ruzuku kupunguza bei ya mbolea. Nina hakika kabisa hawakufanya utafiti wa kina kwa sababu watapoteza pesa nyingi kufanya semina ambazo kwa kweli Wananchi wa Kilolo sasa hivi hawazihitaji, wanachohitaji wao ni bei za pembejeo zipungue ili ziwafikie na waweze kupambana na umaskini vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa nimpongeze Waziri anayeshughulikia mambo ya Utawala Bora, Mheshimiwa Wilson Masilingi. Kazi imefanyika, mabadiliko yapo na rushwa imepungua. Lakini kikubwa ni kwamba sisi tunapiga kelele tu rushwa, rushwa, rushwa, rushwa, lakini kazi yetu ni kumshauri tunafanyaje kwa sababu malaria kwa mfano inaambukizwa na mbu na mbu wapo. Sasa ukiacha kununua chandarua kwa kutegemea kwamba mbu watakufa wenyewe itakuwa ni matatizo. Suala la rushwa tunamshauri vipi Mheshimiwa ili rushwa ikome?

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nataka niwahakikishie kwamba, katika watu wanaochukia rushwa basi Mheshimiwa Wilson Masilingi ni mmojawapo, akifuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi. Anakuna kichwa mpaka nywele zinapungua kwa sababu anajua atapambana vipi na rushwa. Kwa hiyo, niwapongeze sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie habari ya njaa. Sisi Tanzania hatuna sababu ya kusema tuna njaa kwani tuna mabonde mazuri ambayo tungeyatumia vizuri. Maji yaliyo mengi yanatoka Kilolo, pia kuna Bonde la Rufiji, bonde la Ruvu na Bonde la Wami. Yale mabonde ni mazuri kwa sababu ni mabonde ambayo maji yake yanajikusanya kabla ya kuingia baharini. Sasa mabonde yale yana madini ya aina ya *Alluvial.* Madini aina ya *Alluvial* ni madini ambayo kwa kweli ndiyo yenye rutuba kuliko madini yoyote. Sasa tungetumia vizuri mabonde hayo yangetuondoa kwenye tatizo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mabonde ambayo yako kule Malagarasi au kule Kagera kwenye bonde la Ngono na Pangani, hizo ni sehemu nzuri sana za umwagiliaji. Nazifananisha na sehemu zile za Nyanzwa na Ruaha Mbuyuni ambazo pia Serikali iangalie uwezekano wa kusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Ruaha Mbuyuni kabla ya kuingia Mkoa wa Morogoro kuna vitunguu vingi sana vinalimwa ...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hapo ndipo tumefikia mwisho wa michango yetu na muda umebaki dakika tano tu hatuwezi kumpa mwingine. Sasa, baada ya kufika hapo sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,
tarehe 23 Juni, 2004 saa tatu asubuhi)*